# شرح المنظومة الحائية

# في

# عقيدة أهل السنة والجماعة

[*Upambanuzi wa shairi kuhusu ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah*]

***Mwandishi:***

الإمام صالح بن فوزان الفوزان

Imaam Swaalih bin Fawzaan al-Fawzaan

***Tarjama:***

Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush

# Yaliyomo:

01. Utangulizi wa "Sharh al-Haa-iyyah" ....7

02. Wasifu wa mtunzi wa kitabu Ibn Abiy Daawuud ....10

03. Shikamana na Qur-aan na Sunnah ....11

04. Umoja unapatikana kupitia Qur-aan na Sunnah ....13

05. Allaah ametahadharisha mfarakano na tofauti ....14

06. Aina mbili za uongofu ....16

07. Usiwe ni jitu la Bid´ah lenye kuzua ....19

08. Maana ya Bid´ah kilugha na Kishari´ah ....21

09. Radd kwa wenye kusema kuna Bid´ah nzuri ....23

10. Unataka kufaulu? - basi shikamana na mambo haya matatu ....26

11. Sunnah ni Wahy wa pili ....28

12. Radd kwa Qur-aaniyyuun ....30

13. Msimamo wa maimamu wa nne pale maoni yao yatatofautiana na dalili ....34

14. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya Qur-aan ....37

15. Mtiririko wa mlolongo wa Qur-aan ....38

16. Radd kwa Ashaa´irah kwamba Qur-aan imechukuliwa kutoka Ubao uliohifadhiwa ....43

17. Vitabu vyote vya mbinguni ni maneno ya Allaah na hayakuumbwa ....44

18. Ambaye hazungumzi hastahiki uola na uungu ....45

19. Qur-aan sio maneno ya Allaah - njama za kiyahudi ....47

20. Haya ndio malengo ya wenye kuwatetea Ahl-ul-Bid´ah ....48

21. Ufalme wa kihakika ni wa Allaah ....49

22. Msimamo wa kusimama katika masuala ya kuumbwa kwa Qur-aan ....51

23. Msimamo kuhusu matamshi ya Qur-aan ....53

24. Matamshi ya Qur-aan yameumbwa au hayakuumbwa? ....................54
25. Kutofautiana kwa watu juu ya Kuonekana kwa Allaah....................56
26. Baadhi ya Aayah zinazothibitisha Kuonekana kwa Allaah Aakhirah....................58
27. Kumtakasa Allaah kutokana na mtoto na baba....................62
28. Radd kwa wenye kumfanyia Allaah kuwa na watoto....................65
29. Sema kama alivyosema Mtume (´alayhis-Salaam) ....................70
30. Allaah ana sifa za kidhati na za kimatendo ....................72
31. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya mikono ya Allaah....................75
32. Radd kwa wanaokanusha Allaah kuwa na mikono....................77
33. Radd kwa wanaoifananisha mikono ya Allaah na ya viumbe....................79
34. Mikono miwili ya Allaah yote ni ya kuume ....................80
35. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya kushuka kwa Allaah....................82
36. Radd kwa wanaokanusha Allaah kushuka kwenye mbingu ya dunia....................84
37. Radd kwa baadhi ya shubuha zinazotumika juu ya kushuka kwa Allaah ....................86
38. Maana tatu ya Jabbar....................88
39. Allaah hushuka mbingu ya chini ya dunia kila usiku ....................90
40. Muislamu isikupite fursa hii kubwa....................91
41. Jahmiyyah, Mu´tazilah na vifaranga vyao wameangamia....................95
42. Kuwa mlinganizi wa haki - usiwe mlinganizi wa upotevu ....................97
43. Fadhila za Maswahabah na Radd kwa wale wenye kuwaponda ....................98
44. Mpangilio wa fadhila za Maswahabah.................... 102
45. Haya ndio malengo ya wenye kuwatukana Maswahabah .................... 104
46. Makundi yenye kuwatukana Maswahabah .................... 106
47. Tofauti iliyopo kuhusu ni nani bora kati ya ´Uthmaan na ´Aliy .................... 107
48. Baadhi ya fadhila za Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anh).................... 109

49. Baadhi ya fadhila za ´Umar (Radhiya Allaahu ´anh) ... 111

50. Baadhi ya fadhila za ´Uthmaan (Radhiya Allaahu ´anh) ... 113

51. Baadhi ya fadhila za ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) ... 115

52. Fadhila za Maswahabah kumi waliobashiriwa Pepo ... 118

53. Kuzungumza maneno mazuri juu ya Maswahabah wote ... 120

54. Baadhi ya fadhila za wajukuze, wana na wakeze Mtume na Mu´aawiyah ... 124

55. Baadhi ya fadhila za Muhaajiruun na Answaar ... 126

56. Fadhila za baadhi ya maimamu wa Ahl-us-Sunnah ... 128

57. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya Qadhwaa´ na Qadar ... 132

58. Utafiti juu ya Qadhwaa´ na Qadar ... 134

59. Utafiti juu ya Qadhwaa´ na Qadar II ... 136

60. Utafiti juu ya Qadhwaa´ na Qadar III ... 142

61. Kujigonga kwa Jabriyyah ... 147

62. Kuamini Qadhwaa´ na Qadar hakupingani na kufanya sababu ... 148

63. Baadhi ya faida za kuamini Qadhwaa´ na Qadar ... 150

64. Mwenye kujilipua na kujiua haamini Qadhwaa´ na Qadar ... 154

65. Utafiti juu ya Qadhwaa´ na Qadar IV ... 155

66. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah - watu wa kati na kati siku zote ... 157

67. Utafiti juu ya Qadhwaa´ na Qadar V ... 158

68. Kutumia Qadhwaa´ na Qadar kama hoja? ... 159

69. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya kuamini siku ya Mwisho ... 162

70. Radd kwa makafiri wenye kupinga kufufuliwa ... 164

71. Maana ya kuamini siku ya Mwisho ... 167

72. Nasaha za Imaam Ibn Abiy Daawuud ... 169

73. Uhalisia wa hali ndani ya kaburi ... 172

74. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya hodhi ya Mtume ........ 175

75. Wataokunywa na kuzuiwa na hodhi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ........ 177

76. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya mizani ........ 178

77. Mtazamo wa Mu´tazilah juu ya mizani siku ya Qiyaamah ........ 179

78. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya waislamu waliokufa katika dhambi kubwa ........ 180

79. Mtazamo wa Khawaarij na Mu´tazilah juu ya mtenda dhambi kubwa ........ 182

80. Tofauti ya uombezi kwa Allaah na kati ya viumbe ........ 184

81. Aina mbili ya uombezi ........ 187

82. Khawaarij na Mu´tazilah ndio wanaopinga uombezi ........ 189

83. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah kuhusu uombezi ........ 190

84. Mtazamo wa Khawaarij, Mu´tazilah na Murji-ah juu ya mtenda dhambi ........ 195

85. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya mtenda dhambi ........ 197

86. Tahadhari na maoni ya Khawaarij yatakuangamiza ........ 199

87. Ndio maana mafusaki wanayapenda madhehebu ya Murji-ah ........ 201

88. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya imani na Radd kwa wanaoonelea kinyume ........ 203

89. Dalili juu ya kwamba imani ni maneno, kuamini na vitendo na kwamba inazidi na kupungua ........ 207

90. Muumini mwenye nguvu ndiye anapendwa zaidi na Allaah kuliko dhaifu ........ 210

91. Ni yepi marejeo wakati wa mizozo na tofauti? ........ 211

92. Msimamo wa maimamu wa nne pale maoni yao yatatofautiana na dalili II ........ 214

93. Radd kwa watu wa vyombo vya khabari wenye kuonelea kurudi katika dalili kuna neno na ni kuwabana watu ........ 216

94. Usiwatukane Ahl-ul-Hadiyth ........ 217

95. Watu walioifanya dini yao kuwa ni pumbao na mchezo ........ 218

96. Sampuli ya kwanza ya Ahl-ul-Hadiyth ........ 219

97. Sampuli ya pili ya Ahl-ul-Hadiyth ........ 221

98. Uwajibu wa kuamini ´Aqiydah hii mwanzo wa maisha hadi mwisho ........ 223

99. Uwajibu wa kutendea kazi yaliyotajwa na mwandishi ........ 224

100. Hitimisho........ 225

بسم الله الرحمن الرحيم

## 01. Utangulizi wa "Sharh al-Haa-iyyah"

Himdi zote zinamstahikia Allaah. Swalah na salaah zimwendee Mtume wetu Muhammad, kizazi chake na Maswahabah zake wote.

Amma ba´d:

Huu ni upambanuzi wa shairi la Abu Bakr bin Abiy Daawuud as-Sijistaaniy (Rahimahumaa Allaah). Ndani yake mna ´Aqiydah yake na yale anayoonelea na kwamba ni mwenye kuwafuata Salaf katika hayo.

Waislamu katika kizazi cha kwanza, kuanzia karne za Maswahabah na karne bora zilizokuja baada yao, walikuwa wakiamini yaliyomo katika Qur-aan na Sunnah pasi na kuwa na wasiwasi na mashaka. Kwa sababu walikuwa ni wenye kumuamini Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) imani ya kweli na yenye nguvu. Hivyo wakaamini yaliyokuja katika Qur-aan na Sunnah. Kila kilichomo ndani ya Qur-aan, Sunnah na mambo yote ya dini walikuwa ni wenye kuyaamini. Hawakuwa ni wenye kuyatilia shaka. Ni mamoja yawe yanahusiana na mambo ya ´Aqiydah, ´ibaadah, mu´amala, adabu, tabia na hukumu za Kishari´ah za halali na haramu. Hawakuwa wanakomeka juu ya kitu katika hayo. Kwa kuwa imani inapelekea kufanya hivo. Walikuwa wameamini kihaki na kikweli. Hawakuwa na mashaka kwa yale yaliyothibiti katika Qur-aan na Sunnah katika maudhui yote na katika maelezo yake juu ya mambo yaliyopita na yaliyoko mbele. Hawakuwa wanavua kitu katika mambo yaliyokuja katika Qur-aan na Sunnah isipokuwa wanakiamini imani ya kukata kabisa. Hivi ndivyo inavyopelekea imani.

Baadae mwishoni mwa zama za Maswahabah kukajitokeza mapote potevu. Kwa mfano Khawaarij, Shiy´ah, Murji-ah na Qadariyyah. Haya ndio mapote yaliyodhihiri. Wakati wa karne bora wenye nayo walikuwa wanajificha na hawafichui uendaji kinyume huu. Ilikuwa yule ambaye anafichua kitu katika hayo basi anachukuliwa hatua na kukemewa. Endapo anafikia katika kiwango cha kuritadi basi alikuwa anauawa ili kuilinda dini hii isije kuchezewa na wachezaji hawa.

Pindi karne bora ziliisha na kukaingia tamaduni za kigeni katika miji ya Kiislamu. Mfano wa tamaduni hizo ilikuwa ni za kirumi na wagiriki. Hapo ndipo kukatokea makosa na walinganizi wa upotevu wakapata uchangamfu kueneza upotevu huu. Kuanzia wakati huo ndio wanachuoni nao wakapata uchangamfu wa kubainisha ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah waliokuwa wakifuata Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), Taabi´uun na waliokuja baada ya Taabi´uun. Wakaiandika ´Aqiydah hiyo kwenye vitabu. Kipindi hicho walikuwa wakiita "Iymaan", "ash-Shariy´ah", "as-Sunnah" na "Tawhiyd". Wakaiandika wakiwaraddi wenye kwenda kinyume. Huu ni upole wa Allaah juu ya Ummah huu ili dini yao iweze kubaki. Allaah katika kila zama huwateua walinzi ili wailinde. Imaam Ahmad (Rahimahu Allaah) amesema:

"Himdi zote ni za Allaah ambaye amefanya katika kila wakati, kipindi ambapo Mitume hawawepo, kunabaki wanachuoni wanamwita yule aliyepotea katika uongofu na wanawavumilia juu ya maudhi. Wanahuisha kwa Kitabu cha Allaah wale waliokufa na kwacho wanamfanya kuona yule ambaye ni kipofu na kwa nuru ya Allaah wanamfanya kuona ambao ni vipofu. Ni wengi waliyoje waliyouawa na Ibliys wamewahuisha! Ni wapotevu wangapi wamewaongoza! Ni athari nzuri iliyoje walionayo kwa watu na athari mbaya iliyoje walionayo watu dhidi yao.

Wanakilinda Kitabu cha Allaah kutokana na upotoshaji wa wapindukaji, dhana za watu wa batili na tafsiri za wajinga. Ni wenye kwenda kinyume na Kitabu na wamekusanyika katika kutofautiana nacho. Wanazungumza juu ya Allaah pasi na elimu. Wanaongea kwa maneno yasiyokuwa wazi na

wanawadanganya wajinga kwa yale wanayowatatiza kwayo. Tunamuomba Allaah atukinge na fitina za wapotevu."

Baada ya hapo waislamu wakarithi vitabu hivi na wakafupisha vitabu vya ´Aqiydah. Wakarithishana vitabu hivi vilivyotungwa na maimamu hawa. Ndipo kukapatikana vitabu vya ´Aqiydah ambavyo ndani yake mlikuwa mambo yote yanayohusiana na ´Aqiydah waliokuwa wakifuata Salaf wa Ummah huu.

Baadhi ya wanachuoni wakatilia umuhimu kuviweka vitabu hivi kwa mtindo wa mashairi. Kwa sababu vitabu vilivyo kwa mtindo wa mashairi ni vyepesi na vinahifadhika haraka na vinabaki kwenye kumbukumbu. Ndipo wakatunga vitabu hivi vinavyozungumzia ´Aqiydah ili iwe sahali kuvihifadhi. Miongoni mwavyo ni shairi hili liliyoko mbele yetu kwa jina "Haa-iyyah" ya Ibn Abiy Daawuud.

## 02. Wasifu wa mtunzi wa kitabu Ibn Abiy Daawuud

Anaitwa Abu Bakr ´Abdullaah bin Abiy Daawuud Sulaymaan bin Ash´ath as-Sijistaaniy.

Baba yake ni Abu Daawuud Sulaymaan bin Ash´ath ambaye ni mmoja katika wale watunzi wa vitabu vya Sunan vine ambavyo ni muhimu.

Abu Daawuud ni katika maswahiba na wanafunzi wa Imaam Ahmad. Ana mambo aliyopokea kutoka kwa Imaam Ahmad yaliyochapishwa kwa jina "Masaa-il Abiy Daawuud."

Mtoto wake huyu mwandishi anaitwa ´Abdullaah. Kun-ya yake ni Abu Bakr. Ni imamu mtukufu. Alisoma kwa baba yake na kwa wanachuoni wengine waliokuwa wakati wake. Alikuwa amebobea katika elimu na mapokezi. Ni mtu ambaye ana nafasi kubwa katika elimu. Haitofautiani na nafasi aliokuwa nayo baba yake (Rahimahumaa Allaah) au inakaribia. Yeye ndiye ametunga mashairi haya yaliyo na ´Aqiydah ya Salaf.

## 03. Shikamana na Qur-aan na Sunnah

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

01- *Shikamana na Kamba ya Allaah na ufuate uongofu*

*usiwe mzushi huenda ukafaulu*

**MAELEZO**

Mwandishi (Rahimahu Allaah) ameanza kwa kusema:

***Shikamana na Kamba ya Allaah na ufuate uongofu***

Anamzungumzisha muislamu. Kamba ya Allaah ni Qur-aan na Sunnah. Amechukua haya kutoka katika maneno Yake (Ta´ala):

وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا

**"Shikamaneni kwa kamba ya Allaah nyote pamoja wala msifarikiane." (03:103)**

Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Hakika yeyote atakayeishi katika nyinyi basi atakuja kuona tofauti nyingi. Hivyo basi, jilazimieni na Sunnah zangu na Sunnah za makhaliyfah wangu waongofu baada yangu. Shikamaneni nazo barabara na ziumeni kwa magego yenu. Tahadharini na mambo ya kuzua. Hakika kila kilichozushwa ni Bid´ah na kila Bid´ah ni upotevu."[1]**

Shairi hili limechukuliwa kutoka katika Qur-aan na Sunnah. Ndani yake mna maamrisho ya kushikamana barabara na Kamba ya Allaah ambayo ni Qur-aan na Sunnah. Kwa msemo mwingine unaweza vilevile kusema kuwa kamba ya

[1] Abu Daawuud (4607), at-Tirmidhiy (2676) na wengine

Allaah ni Uteremsho Wake aliomteremshia Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ni mamoja ikawa ni Qur-aan au Sunanh.

***Shikamana na Kamba ya Allaah...*** - Bi maana shikamana nayo barabara. Amesema (Ta´ala):

وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ

**"Shikamaneni kwa kamba ya Allaah."**

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Hakika Allaah anaridhia kwenu mambo matatu; mumuabudu na wala msimshirikishe na chochote, mshikamane nyote na kamba ya Allaah na wala msifarikiane na mumnasihi yule ambaye Allaah amemfanya kuyatawalia mambo yenu."[2]**

Ameusia mambo haya matatu ambapo moja wapo ni kushikamana na kamba ya Allaah. Kufanya hivo kunamuepusha mtu na mfarakano na tofauti. Hakutokei tofauti na mfarakano isipokuwa ni kwa sababu ya kutokushikamana na Qur-aan na Sunnah. Hivyo ndivyo ilivyokuwa mfarakano na tofauti ya Ahl-ul-Kitaab pamoja na kuwa Allaah aliwateremshia Tawrat na Injiyl. Lakini ilipokuwa hawakushikamana na kamba ya Allaah ndio wakafarikiana na kutofautiana. Kwa ajili hii amesema:

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ تَفَرَّقُوا وَاخْتَلَفُوا مِن بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْبَيِّنَاتُ ۚ وَأُولَٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ

**"Msiwe kama wale waliofarikiana na wakatofautiana baada ya kuwajia hoja bayana. Hakika hao watapata adhabu kuu." (03:105)**

Huu ndio mwenendo wa Ahl-ul-Kitaab. Waliacha Kitabu cha Mola wao na matokeo yake wakafarikiana.

[2] Muslim (10) na (1715)

## 04. Umoja unapatikana kupitia Qur-aan na Sunnah

Hii ndio inakuwa natija ya mwisho. Kila ambaye hachukui dini na ´Aqiydah yake kutoka katika Qur-aan na Sunnah, basi natija ya mwisho inakuwa ni mfarakano na tofauti. Allaah (Ta´ala) amesema:

وَإِنَّ هَٰذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاتَّقُونِ فَتَقَطَّعُوا أَمْرَهُم بَيْنَهُمْ زُبُرًا ۖ كُلُّ حِزْبٍ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ

**"Hakika huu ummah wenu ni ummah mmoja Nami ni Mola wenu, basi Nicheni. Lakini wakalivunja jambo lao baina yao makundi mbalimbali, kila kundi kwa waliyokuwa nayo linafurahia." (23:52-53)**

Kila mmoja akazua madhehebu na mfumo wenye kutofautiana na mwengine. Matokeo yake kukatokea fitina na shari kubwa. Hakuna njia nyingine ya kuyaepuka isipokuwa kwa kushikamana na Qur-aan na Sunnah na khaswa inapokuja katika jambo la msingi ambalo ni ´Aqiydah. Allaah huwafanya watu wakawa na umoja kupitia ´Aqiydah. Amesema (Ta´ala):

وَإِن يُرِيدُوا أَن يَخْدَعُوكَ فَإِنَّ حَسْبَكَ اللَّهُ ۚ هُوَ الَّذِي أَيَّدَكَ بِنَصْرِهِ وَبِالْمُؤْمِنِينَ وَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ ۚ لَوْ أَنفَقْتَ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مَّا أَلَّفْتَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ أَلَّفَ بَيْنَهُمْ ۚ إِنَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

**"Wakitaka kukuhadaa, basi Allaah anakutosheleza. Hakika Yeye ndiye ambaye amekusaidia kwa nusra Yake na kwa waumini na Akaunganisha nyoyo zao. Lau ungelitoa vyote vilivyomo ardhini, basi usingeliweza kuunganisha nyoyo zao lakini Allaah amewaunganisha. Hakika Yeye ni Mwenye nguvu kabisa, Mwenye hikmah." (08:62-63)**

Vijizawadi na mali nyingi hazifanyi nyoyo zikawa na umoja. Kinyume chake mambo haya yanazidisha chuki. Vovyote utavyotoa mali zako huwezi kuzifanya nyoyo zikawa na umoja. Kinachofanya nyoyo zikawa na umoja ni Qur-aan na Sunnah.

## 05. Allaah ametahadharisha mfarakano na tofauti

Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) ametahadharisha yale waliyotumbukiaemo nyumati zilizotangulia pindi zilipofarikiana. Amesema (Ta´ala):

وَمَا تَفَرَّقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ إِلَّا مِن بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمُ الْبَيِّنَةُ

**"Hawakufarikiana wale waliopewa kitabu isipokuwa baada ya kuwajia hoja bayana." (98:04)**

Hawana udhuru wowote kwa kuwa Allaah amewabainishia. Lakini hata hivyo wakaacha ubainifu huu na hatimaye wakafarikiana. Amesema (Ta´ala):

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ تَفَرَّقُوا وَاخْتَلَفُوا مِن بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْبَيِّنَاتُ ۚ وَأُولَٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ

**"Msiwe kama wale waliofarikiana na wakatofautiana baada ya kuwajia hoja bayana. Hakika hao watapata adhabu kuu." (03:105)**

فَبَعَثَ اللَّهُ النَّبِيِّينَ مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ وَأَنزَلَ مَعَهُمُ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ لِيَحْكُمَ بَيْنَ النَّاسِ فِيمَا اخْتَلَفُوا فِيهِ ۚ وَمَا اخْتَلَفَ فِيهِ إِلَّا الَّذِينَ أُوتُوهُ مِن بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمُ الْبَيِّنَاتُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ ۖ فَهَدَى اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا لِمَا اخْتَلَفُوا فِيهِ مِنَ الْحَقِّ بِإِذْنِهِ ۗ وَاللَّهُ يَهْدِي مَن يَشَاءُ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ

**"Allaah akatuma Manabii wabashiriaji na waonyaji na akateremsha pamoja nao Kitabu kwa haki ili kihukumu baina ya watu katika waliyokhitilafiana kwayo. Hawakukhitilafiana katika hayo isipokuwa wale waliopewa hicho Kitabu baada ya kuwajia hoja bayana kwa uhusuda baina yao. Allaah akawaongoza wale walioamini kuendea haki katika yale waliyokhitilafiana kwa idhini Yake. Hakika Allaah humwongoza amtakaye kuelekea njia iliyonyooka. (02:213)**

Kwa ajili hii Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) pindi alikuwa anasimama kuswali usiku alikuwa akisema:

**"Ee Allaah! Mola wa Jibraaiyl, Mikaa-il na Israafiyl! Mwenye kuendesha mbingu na ardhi, mjuzi wa vilivyodhahiri na viliyojificha. Hakika wewe utahukumu kati ya waja Wako katika yale waliyokuwa wakitofautiana**

**kwayo. Niongoze katika haki kwa yale kumetokea tofauti kwayo - kwani hakika Wewe unamwongoza umtakaye katika njia iliyonyooka."[3]**

Hii ni du´aa kubwa ambayo Allaah anamkinga kwayo muislamu kutokamana na matamanio, fitina na shari.

[3] Muslim (200) na (770)

## 06. Aina mbili za uongofu

Amesema mwandishi (Rahimahu Allaah):

... *na ufuate uongofu*

Uongofu ni dini aliyotumwa kwayo Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Amesema (Ta´ala):

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ

**"Yeye ndiye ambaye Kamtume Mtume Wake kwa mwongozo na dini ya haki ili ishinde juu ya dini zote japo watachukia washirikina." (09:33)**

Uongofu kwa maana nyingine ni elimu yenye manufaa. Dini ya haki ni yale matendo mema. Tunasoma mwisho wa "al-Faatihah":

اهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ

**"Tuongoze njia iliyonyooka. Njia ya wale Uliowaneemesha, sio ya walioghadhibikiwa wala waliopotea." (01:06-07)**

Ambao Allaah amewaneemesha ni wale waliokusanya baina ya elimu yenye manufaa na matendo mema.

Walioghadhibikiwa ni wale waliojifunza elimu na wakaacha kutenda.

Waliopotea ni wale walioenda kutenda pasi na kuwa na elimu. Mfano wa watu hawa ni kama wale Suufiyyah wajinga.

Kuna sampuli mbili za uongofu:

Ya kwanza: Uongofu wenye maana ya kuelekeza na kuibainisha haki. Huu ni ule uongofu ulioenea. Allaah amewaongoza watu wote kwa maana ya kwamba amewabainishia haki. Amesema (Ta´ala):

وَأَمَّا ثَمُودُ فَهَدَيْنَاهُمْ فَاسْتَحَبُّوا الْعَمَىٰ عَلَى الْهُدَىٰ

**"Ama kina Thamuud Tuliwaongoza, lakini hata hivyo walifadhilisha upofu juu ya uongofu." (41:17)**

Huu ni uongofu wa maelekezo.

Ya pili: Uongofu wa kuongozwa kuitendea kazi haki na kushikamana nayo. Uongofu huu ni maalum na hauwi isipokuwa kwa watu walio na imani. Hakuna mwenye kuumiliki isipokuwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Hakuna anayemiliki suala la kuiongoza mioyo isipokuwa Allaah (Jalla wa ´Alaa). Amesema (Ta´ala):

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَن يَشَاءُ ۚ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ

**"Hakika wewe humwongozi umpendaye, lakini Allaah ndiye anamwongoza amtakaye - Naye Anawajua zaidi waongokao." (28:56)**

Aina ya uongofu wa kwanza unamilikiwa na Mitume, Manabii na wanachuoni. Wote wanaelekeza, kubainisha na kuifahamisha haki. Kwa ajili hii amesema (Ta´ala) kumwambia Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

وَإِنَّكَ لَتَهْدِي إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ

**"Bila shaka unaongoza kuelekea njia iliyonyooka." (42:52)**

Huenda mtu akauliza ni kwa nini Allaah (Jalla wa ´Alaa) amemwamba Mtume Wake katika Aayah:

وَإِنَّكَ لَتَهْدِي

**"Bila shaka unaongoza... "**

Ilihali katika Aayah nyingine amesema:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ

**"Hakika wewe huwezi humwongozi umpendaye."**

Kuna mgongano? Jibu ni hapana. Aayah inayosema:

وَإِنَّكَ لَتَهْدِي إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ

**"Bila shaka unaongoza kuelekea njia iliyonyooka." (42:52)**

bi manaa unaelekeza. Ama kuhusu Aayah inayosema:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ

**"Hakika wewe huwezi humwongozi umpendaye." (28:56)**

bi manaa huwezi kumuwafikisha mtu akaikubali haki. Hakuna mwenye uwezo wa jambo hilo isipokuwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Hakuna mgongano kati ya Aayah mbili hizo. Ambaye anaweza kuonelea hivyo ni yule ambaye hana elimu. Kuhusu yule ambaye yuko na ujuzi wa Qur-aan na elimu hakuna mgongano uliyopo katika Qur-aan na Sunnah. Qur-aan kamwe haiwezi kujigonga. Kadhalika Sunnah. Kwa sababu ni Uteremsho wenye kutoka kwa Mwingi wa hekima, mhimidiwa. Lakini hili linahitajia kwa yule mwenye uelewa na mwenye kuoanisha baina ya dalili.

## 07. Usiwe ni jitu la Bid´ah lenye kuzua

Amesema mwandishi (Rahimahu Allaah):

*usiwe mzushi huenda ukafaulu*

**MAELEZO**

Haya ni makatazo. Huu ni unasibisho wa Bid´ah. Bid´ah ni kile kilichozuliwa katika dini ambacho hakina asli si katika Qur-aan wala Sunnah.

Allaah ametukataza kuzua katika dini. Vivyo hivyo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ametutahadharisha kuzua katika dini. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا

**"Leo nimekukamilishieni dini yenu, nimekutimizieni neema Yangu na nimekuridhieni kwenu Uislamu uwe ndio dini yenu." (05:03)**

Dini imekamilika na haina haja ya kuiongezea mambo ambayo wewe unaonelea kuwa ni mazuri au ukawafuata kichwa mchunga wengine ilihali mambo hayo hayana dalili katika Qur-aan wala Sunnah ukajikurubisha kwayo kwa Allaah. Kwa mfano Adhkaar za Bid´ah, swalah za Bid´ah na aina nyenginezo zote za kujikurubisha kwa Allaah endapo yatakuwa hayana dalili. Katika hali hiyo itakuwa ni Bid´ah. Haijalishi kitu hata kama nia ya mwenye kufanya hivo ni nzuri anachokusudia ni kupata ujira na thawabu na hakusudii kwenda kinyume. Yeye ameonelea kuwa jambo hilo lina kheri na hivyo akalifanya kuwa zuri. Uhakika wa mambo jambo hilo halina kheri yoyote. Kama lingekuwa na kheri basi lingekuja katika Qur-aan na Sunnah:

وَمَا كَانَ رَبُّكَ نَسِيًّا

**"Mola wako si Mwenye kusahau kabisa." (19:64)**

مَّا فَرَّطْنَا فِي الْكِتَابِ مِن شَيْءٍ

**"Hatukupuuza katika Kitabu kitu chochote." (06:38)**

Kheri zote na uongofu unapatikana katika Qur-aan na Sunnah. Ambaye ataleta nyongeza isiyokuwepo katika Qur-aan na Sunnah, basi hiyo ni Bid´ah yenye kurudishwa. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Mwenye kufanya kitendo kisichoafikiana na dini yetu, atarudishiwa mwenyewe."[4]**

**"Mwenye kuzua katika dini yetu hii yale yasiyokuwemo, atarudishiwa mwenyewe."[5]**

Haijuzu kuzua katika dini au kufanya kitu ambacho hakuja nacho Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na mtu akawa ni mwenye kujikurubisha kwacho mbele ya Allaah. Hii ni Bid´ah. Kila Bid´ah ni upotevu.

[4] Muslim (18) na (1718)

[5] al-Bukhaariy (2697) na Muslim (18) na (1718)

## 08. Maana ya Bid´ah kilugha na Kishari´ah

Bid´ah kilugha maana yake ni kitu kilichozuliwa ambacho hakikutanguliwapo kuwa na mfano. Kwa mfano mtu anaweza kusema:

"Kitu hiki kimezuliwa."

Bi maana kipya. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

بَدِيعُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ

**"Mwanzilishi wa mbingu na ardhi." (02:117)**

Bi maana Aliyevianzilisha bila ya kutanguliwapo kuwa na mfano wake. Kadhalika anasema kumwambia Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

قُلْ مَا كُنتُ بِدْعًا مِّنَ الرُّسُلِ

**"Sema: "Mimi sikuwa jambo jipya lilozuka miongoni mwa Mitume."" (46:09)**

Bi maana mimi sio Mtume wa kwanza. Bali kabla yangu walikuwepo Mitume wengi. Mimi sio Bid´ah, yaani mpya ambaye hakukutangulia kuwepo mfano wangu katika nyumati zilizotangulia. Ni vipi mtanikemea mimi kuwa Mtume wa Allaah ilihali kabla yangu kulikuwepo Mitume tu wengi?

Bid´ah Kishari´ah maana yake ni mambo yaliyozushwa katika dini yasiyokuwemo na wakati huo huo yakawa hayana dalili si katika Qur-aan wala Sunnah.

Bid´ah haina kheri yoyote. Inamtenga mtu mbali na Allaah na inamkasirisha Allaah (´Azza wa Jall). Kuhusu Sunnah yote ni kheri na Allaah anairidhia, anaipenda na kulipa thawabu kwayo. Kadhalika Allaah (Ta´ala) anaichukia Bid´ah, anawachukia Ahl-ul-Bid´ah na anaadhibu kwayo. Hakuna nafasi yoyote ya kuongeza, kuweka mambo yenye kuonelewa kuwa ni mazuri na

kuwafuata watu kwa yale waliyomo. Ni lazima kwanza kujua dalili zao. Endapo watakuwa katika haki, tutawafuata. Amesema (Ta´ala):

وَاتَّبَعْتُ مِلَّةَ آبَائِي إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ

**“Nimefuata dini ya baba zangu; Ibraahiym, Ishaaq na Ya’quub." (12:38)**

Huku ni kufuata kwa haki. Lakini endapo watakuwa katika isiyokuwa haki hatuwafuati hata kama watakuwa ni watu bora kabisa.

Manaswara pindi walipozua utawa ambao Allaah hakuwaandikia walipotea kwao. Isitoshe hawakuweza kusimama nao. Uliwashinda kusimamisha. Kwa sababu wao wenyewe ndio walijibebesha wasiyoyaweza. Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) haikalifishi nafsi yoyote isipokuwa yale inayoyaweza. Lakini wao walijibebesha mambo wasiyoyaweza. Hatimaye utawa ukawashinda na wakauacha:

فَمَا رَعَوْهَا حَقَّ رِعَايَتِهَا

**"Hawakuuchunga ipasavyo kuchungwa." (57:27)**

إِلَّا ابْتِغَاءَ رِضْوَانِ اللَّهِ

**"... isipokuwa ni kutafuta radhi za Allaah." (57:27)**

Ni jambo walizua wakitaka kupata radhi za Allaah. Hii ni dalili inayofahamisha kuwa kinachozingatiwa ni dalili. Lengo na nia peke yake havitoshelezi.

## 09. Radd kwa wenye kusema kuna Bid´ah nzuri

Kwa ufupi ni kwamba Bid´ah ni shari hata kama watu wake watadai kuwa ni kheri. Hata kama watasema kuwa Bid´ah imegawanyika sehemu mbili:

Ya kwanza: Bid´ah nzuri.

Ya pili: Bid´ah mbaya.

Tunawaambia kuwa hakuna kitu kizuri katika Bid´ah kwenye dini. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Kila Bid´ah ni upotevu."**

Mwenye kusema kuwa kuna Bid´ah nzuri basi huku ni kukadhibisha maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Kila Bid´ah ni upotevu."**

Kadhalika:

**"Mwenye kufanya kitendo kisichoafikiana na dini yetu, atarudishiwa mwenyewe."**

Katika dini hakuna Bid´ah nzuri hata siku moja.

Kuhusu yale waliyodai kwamba ni Bid´ah nzuri ikiwa ni pamoja vilevile na ujenzi wa masomo, kutunga vitabu n.k. tunawaambia kuwa sio Bid´ah. Uhakika wa mambo ni kuwa dini imesisitiza katika mambo haya. Ni njia zinazopelekea katika mambo yaliyowekwa katika Shari´ah. Dini imesisitiza kutenda wema, matendo mema na kufanya mambo ya kheri. Zote hizi ni njia za kheri. Ni mambo yanasaidia katika kutenda kheri. Kwa hivyo sio Bid´ah. Mambo haya yameletwa na dini na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akakokoteza kwayo. Amesema (Ta´ala):

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ ۖ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ

**"Saidianeni katika wema na uchaji Allaah, na wala msishirikiane katika dhambi na uadui." (05:02)**

Kuhusu maneno yake (´alayhis-Salaam):

**"Ambaye ataweka katika Uislamu msingi mzuri basi atapata ujira wake na ujira wa yule atakayeufanya."[6]**

Kikusudiwacho ni mtu amehuisha Sunnah iliyofishwa na watu wakamfuata katika hilo. Mtu huyu atapata ujira wake na ujira wa atakayemuiga na kumfuata. Haina maana kwamba ni Bid´ah nzuri. Kinyume chake ni Sunnah.

Kufunza elimu yenye manufaa na kutendea kazi mambo yenye kumsaidia mtu na kujifunza elimu kama mfano wa kufungua masomo, kuanzisha vyuo vikuu na kufungua vitu vyenye kuwaunganisha wanafunzi. Yote haya ni katika mambo yenye kusaidia katika kujifunza elimu. Ni mambo yameamrishwa Kishari´ah na sio Bid´ah.

Kuhusu kuzua katika mambo yasiyohusiana na dini. Kwa mfano kuvumbua mambo ya viwanda, ndege, gari na vyombo vya bahari. Hayahusiani na dini. Ni mambo yameruhusiwa. Sio kuzua katika dini. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

وَسَخَّرَ لَكُم مَّا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مِّنْهُ

**"Amekutiishieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini vyote humo." (45:13)**

Ni kwa ajili ya manufaa yenu nyinyi. Mambo haya hayaingii katika ´ibaadah. Hata hivyo vinaweza kumsaidia mtu kufanya ´ibaadah. Kwa mfano tunapanda gari kwa ajili ya kwenda hajj, kuwaunga ndugu, kufikia jambo la halali, kwa ajili ya kwenda kufanya biashara na sherehe. Yote haya ni katika mambo yenye manufaa ya mbinguni na ardhini ambayo Allaah ametujuzishia. Hayana lolote kuhusiana na dini. Ni mambo ya kidesturi na yaliyoruhusiwa.

[6] Muslim (69) na (1017)

Hatuyaiti kuwa ni Bid´ah. Isipokuwa ikiwa kama mtu anakusudia kwa upande wa lugha kwa kuwa ni mambo mepya ingawa yamejitokeza katika wakati fulani na hayakujitokeza hapo kabla. Watu wameyaweza ilihali hapo kabla watu walikuwa hawayawezi.

Ni wajibu kuyajua mambo haya. Kwa kuwa wapotevu wanataka kuwapaka watu mchanga wa machoni. Wanauliza: "Sasa mambo yote imekuwa ni Bid´ah?" Tunawaambia: sio kila kitu ni Bid´ah. Bid´ah ni yale yaliyozushwa katika dini ilihali hayapo na wakati huo huo yakawa hayana dalili si katika Qur-aan wala Sunnah. Mbali na hayo sio Bid´ah. Ni miongoni mwa mambo ambayo Allaah amewaruhusu waja Wake. Kuna tofauti kati ya hayo mawili.

## 10. Unataka kufaulu? - basi shikamana na mambo haya matatu

Amesema mwandishi (Rahimahu Allaah):

... *huenda ukafaulu*

Bi maana ikiwa unataka kufaulu ambako ni furaha duniani na Aakhirah basi shikamana na kamba ya Allaah na ufuate uongofu. Hii ndio njia ya furaha. Kufaulu maana yake ni kheri nyingi na kupata furaha. Amesema (Ta´ala):

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَاشِعُونَ

**"Hakika wamefaulu waumini ambao katika swalah zao wananyenyekea." (23:01-02)**

Mpaka alipofikia kusema (Ta´ala):

وَالَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَوَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ أُولَٰئِكَ هُمُ الْوَارِثُونَ الَّذِينَ يَرِثُونَ الْفِرْدَوْسَ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

**"Na ambao wanazihifadhi swalah zao - hao ndio warithi ambao watarithi [mabustani ya] *al-Firdaws* wao humo ni wenye kudumu." (23:09-11)**

Hizi ndio sababu za kufaulu. Ikiwa unataka kufaulu basi ni lazima kwako ushikamane na mambo haya matatu:

La kwanza: Shikamana na kamba ya Allaah.

La pili: Ufuate uongofu.

La tatu: Jiepushe na Bid´ah.

Ukikosa moja katika mambo haya matatu basi utakhasirika na hutofaulu kamwe. Amesema (Ta´ala):

فَمَن ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ وَمَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَٰئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ فِي جَهَنَّمَ خَالِدُونَ

**"Basi yule ambaye mizani yake itakuwa nzito, hao ndio wenye kufaulu; na yule ambaye mizani yake itakuwa khafifu, basi hao ni wale ambao wamekhasirika nafsi zao Motoni watakuwa ni wenye kudumu." (23:102-103)**

Hiki ndiko kinyume cha kufaulu: ni khasara. Si kwamba wamekhasirika mali zao. Bali wamekhasirika nafsi zao. Mtu kukhasirika nafsi yake ndio khasara kubwa kabisa na tunaomba Allaah atukinge. Amesema (Ta´ala):

قُلْ إِنَّ الْخَاسِرِينَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ وَأَهْلِيهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ أَلَا ذَٰلِكَ هُوَ الْخُسْرَانُ الْمُبِينُ

**"Sema: "Hakika waliokhasirika ni wale waliokhasiri nafsi zao na familia zao Siku ya Qiyaamah." Tanabahi! Huko ndiko kukhasirika kwa wazi." (39:15)**

***huenda... -*** Haya ni matarajio. Kwa sababu ´Aqiydah sahihi ni kwamba hatumkatii yeyote kufaulu isipokuwa yule aliyekatiwa na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) au ikawa imekuja katika Qur-aan ya kwamba mtu huyo amefaulu. Yule ambaye hakutajwa si katika Qur-aan wala Sunnah kwa dhati yake ya kwamba ni katika waliofaulu sisi hatumkatii kufaulu. Lakini hata hivyo tunatarajia wema kwa walio wema na tunachelea kwa wenye kutenda mabaya. Sababu nyingine ni kuwa muislamu asidanganyike na matendo yake. Maana ya maneno yake:

***huenda ukafaulu -*** Bi maana usighurike na matendo yako. Lakini hata hivyo jibidishe na matendo mema na utaraji kuwa Allaah atakujaalia kuwa miongoni mwa wenye kufaulu. Usitegemee kufaulu pake yake pasi na matendo. Huu ni mwenendo wa wapotevu. Haya ndio matarajio mabaya. Matarajio mazuri ni yale yenye kuambatana na matendo mema. Kwanza fanya sababu kisha mtegemee Allaah (´Azza wa Jall).

## 11. Sunnah ni Wahy wa pili

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

02- *Amini kwa Kitabu cha Allaah na Sunan ambazo*

*iliyokujia kutoka kwa Mtume wa Allaah utaokoka na kufaidi*

**MAELEZO**

Bi manaa fuata Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ifanye dini yako ni yenye kuchukuliwa kutoka katika Qur-aan na Sunnah na isiwe yenye kutoka katika matamanio na mambo yaliyozuliwa.

***Sunan... -*** Ni wingi wa Sunnah. Ni njia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliyesema:

**"Jilazimieni na Sunnah zangu... "**

Bi maana njia yangu.

Muhaddithuun na elimu ya istilahi ya Hadiyth Sunnah maana yake ni yale yaliyothibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) sawa iwe ni maneno, matendo, kulikubali jambo au sifa. Maana maalum ni ule ufafanuzi wa Muhaddithuun.

Hapa tunajifunza ya kwamba ni lazima kutumia Sunnah kama dalili baada ya Qur-aan. Sunnah ni chanzo cha pili miongoni mwa vyanzo vya Uislamu baada ya Qur-aan tukufu.

Misingi ya dalili kwa watu wa Usuwl kuna ambayo kuna maafikiano juu yake na kuna mingine kuna tofauti juu yake. Misingi ambayo kuna maafikiano juu yake ni ifuatayo:

Msingi wa kwanza: Qur-aan tukufu.

Msingi wa pili: Sunnah ya Mtume. Kwa kuwa ni Wahy wa pili baada ya Qur-aan. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا

**"Yale anayokupeni Mtume yachukueni, na yale anayokukatazeni, yaacheni." (59:07)**

فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

**"Watahadhari wale wanaokhalifu amri yake, isije kuwasibu *fitnah* au ikawasibu adhabu iumizayo." (24:63)**

Huu ndio msingi wa pili ambao ni Sunnah za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kwani yeye (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni kama Mola alivyomsifu:

وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ

**"Wala hatamki kwa matamanio. Hayo ayasemayo si chochote isipokuwa ni *Wahy* unaofunuliwa kwake." (53:03-04)**

Kwa ajili hii wanachuoni wanaita - yaani Sunnah - kuwa ni Wahy wa pili baada ya Qur-aan tukufu.

## 12. Radd kwa Qur-aaniyyuun

Kila kilichosihi kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) basi ni wajibu kukichukua, kukifuata na kukitendea kazi. Ni mamoja ikawa kimepokelewa kwa njia nyingi au moja tofauti na wanavyofanya watu wa Bid´ah ambao wanaikataa Sunnah. Wanasema kuwa Qur-aan inawatosheleza. Ni jambo linalojulikana kwamba ambaye ataitendea kazi Sunnah basi kaitendea kazi vilevile Qur-aan. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا

**"Yale anayokupeni Mtume yachukueni, na yale anayokukatazeni, yaacheni." (59:07)**

Halafu hawa wanasema kuwa Qur-aan inatutosheleza.

Amesema (Jalla wa ´Alaa):

مَّن يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ

**"Atakayemtii Mtume basi amemtii Allaah." (04:80)**

وَاتَّبِعُوهُ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ

**"Mfuateni ili mpate kuongoka." (07:158)**

وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ

**"Mtiini Allaah na Mtume mpate kurehemewa." (03:132)**

Watu hawa wanasema uongo pale wanaposema kuwa wanaitendea kazi Qur-aan pekee midhali wameiacha Sunnah.

Jengine ni kwamba Qur-aan imekuja kwa jumla. Sunnah ndio inayoibainishia na kuifafanua. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema kumwambia Mtume Wake:

وَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ

**"Tumekuteremshia Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwao." (16:44)**

Sunnah ndio yenye kuifasiri Qur-aan, kuiweka wazi na kuifahamisha. Qur-aan ina mafungamano yenye nguvu kabisa na Qur-aan. Kwa sababu Sunnah ndio yenye kuibainisha, kuiweka wazi, kufafanua yaliyo ya jumla na kuyafunga ambayo hayakufungwa. Sivyo tu, bali Qur-aan inaweza kufuta Sunnah na kinyume chake, Qur-aan ikaifuta Qur-aan na Sunnah ikaifuta Sunnah. Ni lazima yapatikane mambo haya makuu. Watu hawa wenye kuipuuza Qur-aan walielezewa na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na akatahadharisha nao aliposema:

**"Kunakaribia kuwepo mtu aliyeshiba aegemee kitandani mwake. Akaelezwa Hadiyth miongoni mwa Hadiyth ambapo atasema: "Baina yetu sisi na nyinyi kuna Kitabu cha Allaah (´Azza wa Jall). Tutayoyatapa humo ya halali na sisi pia tutayahalalisha na tutayoyapata humo ya haramu na sisi pia tutayaharamisha. Tanabahini! Hakika aliyoharamisha Mtume wa Allaah ndio yale yale aliyoharamisha Allaah."[7]**

Vilevile amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Nimepewa Qur-aan na kitu mfano wake."**

Bi maana Sunnah.

Amesema (Ta´ala):

وَأَنزَلَ اللَّهُ عَلَيْكَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ

**"Allaah amekuteremshia Kitabu na hikmah." (04:113)**

وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ

[7] Abu Daawuud (4604), at-Tirmidhiy (2664), Ibn Maajah (12), Ahmad (04/131) na wengine

**"Awafunze Kitabu na hikmah." (03:164)**

Kitabu ni Qur-aan na hikmah ni Sunnah. Sunnah ni kitu cha lazima na ndio msingi wa pili miongoni mwa misingi ya dalili ambayo kuna maafikiano juu yake.

Kuhusu tofauti ya watu hawa haizingatiwi. Kwa sababu watu hawa ima ni Khawaarij, wajinga au wanaojifanya kuwa ni wasomi. Kuna uwezekano vilevile wana malengo mengine wanachotaka ni kuiharibu dini hatua kwa hatua. Tofauti yao haizingatiwi na maneno yao hayaangaliwi. Sunnah sahihi ndio inatakiwa kutendewa kazi sawa iwe katika mambo ya matawi au ya msingi.

Kadhalika wapuuze wale wenye kusema kuwa mapokezi yaliyopokelewa kwa njia moja yasitendewe kazi katika mambo ya ´Aqiydah. Yanatakiwa kutendewa kazi katika mambo ya matawi peke yake. Wanaonelea kuwa ni dalili zenye kutia mashaka. Tunawaambia: ni zenye kuwatia mashaka nyinyi. Kwa walio na imani sio dalili zenye kutia mashaka. Ni dalili zinazofidisha yakini. Maadamu zimesihi kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) basi zinafidisha elimu. Hazitii mashaka. Zinatendewa kazi katika mambo ya ´Aqiydah, mu´amala na mengineyo.

Msingi wa tatu: Maafikiano. Dalili yake ni maneno Yake (Ta´ala):

وَمَن يُشَاقِقِ الرَّسُولَ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَىٰ وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ الْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِ مَا تَوَلَّىٰ وَنُصْلِهِ جَهَنَّمَ ۖ وَسَاءَتْ مَصِيرًا

**"Atakayempinga Mtume baada ya kuwa imeshambainikia uongofu na akaifuata njia isiyokuwa ya waumini, Tutamgeuza alikogeukia mwenyewe na tutamuingiza Motoni - ni uovu ulioje mahali pa kuishia." (04:115)**

Vilevile amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Ummah wangu hauafikiani juu ya upotevu."[8]**

[8] Abu Daawuud (4253), at-Twabaraaniy katika "al-Kabiyr" (3440) na wengineo

Maafikiano ya kimaneno ni hoja yenye kukata mashauri. Kuhusu maafikiano ya kunyamazia ni hoja yenye kutia mashaka. Kwa sababu kuna uwezekano kukawepo aliyeonelea kinyume ingawa haikubainika. Lakini wanachuoni wote wakisema neno na wakaafikiana juu yake na pasiwepo ambaye alionelea kinyume, basi hiyo ni hoja yenye kukata mashauri kabisa.

Ya nne: Kipimo (Qiyaas). Ni kunyofoa hukumu kutoka katika msingi kutokana na kasoro iliyopo. Hivi ndivyo wanavyoonelea wanachuoni wengi na Dhwaahiriyyah na baadhi ya Hanaabilah wameonelea kinyume. Lakini wengi katika Ummah wanaonelea kutumia kipimo. Ni dalili sahihi endapo itatimiza masharti yaliyotajwa katika vitabu vya Usuwl.

Mbali na hizo kumebaki misingi mingine kadhaa kama mfano wa maneno ya Swahabah n.k. Mambo haya wanachuoni wametofautiana kwayo na ni tofauti iliyo na nguvu.

Kuhusu tofauti iliyopo juu ya kipimo haina nguvu. Wengi wanaonele kutumia kipimo. Imaam Ahmad amesema:

"Kipimo kinatumiwa wakati wa dharurah."[9]

Ni kama mfano wa nyamafu inaliwa wakati wa dharurah. Kunapokuwepo dalili katika Qur-aan na Sunnah kunakuwa hakuna haja ya kipimo. Isipopatikana ndio kipimo kinaendewa kwa sababu ya dharurah.

[9] adh-Dhahabiy katika "as-Sayr" (10/77)

## 13. Msimamo wa maimamu wa nne pale maoni yao yatatofautiana na dalili

Mwandishi (Rahimahu Allaah) amesema:

02- *Amini kwa Kitabu cha Allaah na Sunan ambazo*

*iliyokujia kutoka kwa Mtume wa Allaah utaokoka na kufaidi*

**MAELEZO**

Ifanye dini yako ni yenye kuchukuliwa kutoka katika Qur-aan na Sunnah ambazo ni zile Hadiyth Swahiyh. Kuhusu yenye kuja kutoka kwa wengine yanatakiwa kuangaliwa. Endapo yatakuwa ni yenye kuafikiana na Qur-aan na Sunnah yatatendewa kazi. Ikiwa yanatofautiana na Qur-aan na Sunnah yatarudishwa kwa mwenye nayo. Maimamu wanausia kufanya hivi. Imaam ash-Shaafi´iy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Maoni yangu yakitofautiana na maneno ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), yachukueni maneno ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na yatupeni maoni yangu kando."[10]

Imaam Maalik (Rahimahu Allaah) amesema:

"Kila mmoja wetu anarudiwa isipokuwa mtu mwenye kaburi hili."

Bi maana Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kwa kuwa alikuwa akifunza katika msikiti wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) harudiwi kabisa. Maneno yake (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) yanakubaliwa. Kuhusu wengine yakiafikiana na Qur-aan na Sunnah yatatendewa kazi na yakitofautiana nayo yanarudishwa.

[10] Tazama "Qawaa´iyd at-Tahdiyth", uk. 273 ya al-Qaasimiy, "Siyaar A´laam-in-Nubalaa" (10/35) na wengineo

Imaam Abu Haniyfah (Rahimahu Allaah) - naye ndiye wa kwanza katika maimamu wanne - amesema:

"Ikija Hadiyth kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) tutaikubali, ikija Hadiyth kutoka kwa Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) tutaikubali na ikija Hadiyth kutoka kwa waliokuja baada ya Maswahabah (Taabi´uun), wao ni wanaume na sisi pia ni wanaume."

Bi maana chenye kutoka kwa asiyekuwa Allaah, Mtume Wake na Maswahabah zake kitatakiwa kuangaliwa kwanza hata kama kitakuwa kimetoka kwa mtu aliye bora kabisa. Haijalishi kitu hata kama ni Taabi´uun. Kitahitaji kuangaliwa. Kikiafikiana na Qur-aan na Sunnah kitachukuliwa. Kikienda kinyume navyo kitaachwa.

Imaam Ahmad (Rahimahu Allaah) amesema:

"Ninastaajabishwa na watu wanaojua elimu ya mlolongo wa wapokezi na usahihi wake halafu wanaenda katika maoni ya Sufyaan."

Sufyaan ath-Thawriy alikuwa ni mwanachuoni na imamu mtukufu.

Akaendelea kusema (Rahimahu Allaah):

"Allaah (Ta´ala) amesema:

فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

**"Na watahadhari wale wanaokhalifu amri yake, isije ikawapata *fitnah* au ikawapata adhabu iumizayo." (24:63)**

Haijuzu kuchukua maoni ya mwanachuoni pasi na kujali ni elimu kiasi gani atakuwa amefikia isipokuwa mpaka yawe yamejengwa juu ya dalili sahihi. Ikiwa yanaenda kinyume na dalili, basi haijuzu kuyatendea kazi. Kwa kuwa hakuna maoni ya yeyote ambayo yanaweza kusimama pamoja na maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Amesema (Ta´ala):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ ۖ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

**"Enyi mlioamini! Msitangulie mbele ya Allaah na Mtume Wake. Mcheni Allaah, kwani hakika Allaah ni Mwenye kusikia na ni Mjuzi." (49:01)**

## 14. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya Qur-aan

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

03- *Sema "Hayakuumbwa maneno ya Mfalme Wetu"*

*hivyo ndivyo walivyoamini wachaji Allaah na wakaweka wazi"*

**MAELEZO**

Katika ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wakiwemo Maswahabah na Taabi´uun na waliowafuata ni kwamba hawana shaka yoyote juu ya kwamba Qur-aan ni maneno ya Allaah ya kihakika. Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) amezungumza kwayo na Akamletea nayo Jibriyl (´alayhis-Salaam). Jibriyl ameyasikia kutoka kwa Allaah na yeye akamteremshia nayo Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambapo na yeye pia (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akawafikishia nayo Ummah Wake.

## 15. Mtiririko wa mlolongo wa Qur-aan

Amesema (Ta´ala):

وَإِنَّهُ لَتَنزِيلُ رَبِّ الْعَالَمِينَ نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ عَلَىٰ قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ بِلِسَانٍ عَرَبِيٍّ مُّبِينٍ

**"Hakika ni uteremsho wa Mola wa walimwengu. Ameiteremsha roho mwaminifu juu ya moyo wako ili uwe miongoni mwa waonyaji kwa lugha ya kiarabu ilio wazi." (26:192-195)**

Maneno Yake:

وَإِنَّهُ لَتَنزِيلُ رَبِّ الْعَالَمِينَ

**"Hakika ni uteremsho wa Mola wa walimwengu."**

Amezungumza kwayo na yameteremka kutoka Kwake (Subhaanahu wa Ta´ala).

نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ

**"Ameiteremsha roho mwaminifu... "**

Naye ni Jibriyl ambaye kazi yake ni kuteremsha Wahy.

عَلَىٰ قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ

**"... juu ya moyo wako ili uwe miongoni mwa waonyaji... "**

Anazungumzishwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ameyapokea kutoka kwa Jibriyl.

بِلِسَانٍ عَرَبِيٍّ مُّبِينٍ

**"... kwa lugha ya kiarabu ilio wazi."**

Lugha ya Qur-aan ni kiarabu. Ndio lugha faswaha zaidi.

Amesema vilevile (Subhaanahu wa Ta´ala):

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ

**"Hakika hii bila shaka ni kauli ya mjumbe mtukufu." (81:19)**

Bi maana Jibriyl (´alayhis-Salaam).

ذِي قُوَّةٍ عِندَ ذِي الْعَرْشِ

**"Mwenye nguvu kwa huyo Mwenye ´Arshi... "**

Bi maana Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).

مَكِينٍ

**"... na mwenye cheo."**

Bi maana Jibriyl (´alayhis-Salaam). Allaah amempa nguvu na cheo na ukuruba Kwake (Jalla wa ´Alaa).

مُطَاعٍ

**"Anayetiiwa... "**

Malaika wanamtii.

ثَمَّ أَمِينٍ

**"... tena muaminifu."**

Ni mwaminifu juu ya Wahy wa Allaah (´Azza wa Jall). Hizi ndio sifa za Jibriyl (´alayhis-Salaam). Ni mwaminifu ambaye hazidishi wala hapunguzi. Anafikisha kama alivyopokea kutoka kwa Allaah (´Azza wa Jall).

Halafu akasema:

وَمَا صَاحِبُكُم

**"Na wala huyu mwenzenu... "**

Bi maana Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

بِمَجْنُونٍ

**"... hana wazimu."**

Kama wanavyosema washirikina. Amemkanushia wendawazimu.

وَلَقَدْ رَآهُ

**"Bila shaka alimuona... "**

Bi maana alimuona Jibriyl (´alayhis-Salaam) katika umbile lake la kimalaika. Alimuona kwa juu katika upeo Makkah.

بِالْأُفُقِ

**"... upeo." (81:19-23)**

Kwa juu. Alimuona kwa macho yake.

Amesema tena (Jalla wa ´Alaa):

وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَىٰ

**"Hakika alimuona katika uteremko mwingine." (43:13)**

Bi maana Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimuona Jibriyl katika umbile lake kwa mara nyingine kwenye mkunazi wa mwisho usiku wa Mi´raaj. Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimuona Jibriyl katika umbile lake ambalo Allaah amemuumba kwalo mara mbili; mara ya kwanza ilikuwa Makkah na mara nyingine ilikuwa katika ulimwengu wa juu kwenye mkunazi wa mwisho. Mbali na hizi Jibriyl alikuwa akimjia Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika umbile la mwanaume ambapo amekaa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na watu

wake. Tahamaki walikuwa wakiona mtu. Kwa sababu hawawezi kumuona katika umbile lake la kimalaika.

Huu ndio mtiririko wa mlolongo wa Qur-aan. Ummah wa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wameipokea kutoka kwa Muhammad, Muhammad ameipokea kutoka kwa Jibriyl, Jibriyl ameipokea kutoka kwa Allaah (´Azza wa Jall). Kwa hivyo ni maneno ya Allaah. Kuhusu kuinasibisha kwa Malaika:

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ

**"Hakika hii bila shaka ni kauli ya mjumbe mtukufu." (81:19)**

Vilevile kuinasibisha kwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ

**"Hakika hii bila shaka ni kauli ya Mtume mtukufu na sio kauli ya mshairi." (60:40-41)**

Ni unasibisho wa kufikisha. Jibriyl na Muhammad (´alayhimaas-Salaam) wote wawili kazi yao ni kufikisha kutoka kwa Allaah. Maneno yananasibishwa kwa yule aliyeanza kuyasema na hayanasibishwi kwa yule mwenye kuyafikisha. Ni jambo lisilowezekana maneno yakawa ya watu watatu. Allaah amekhabarisha kwamba ni maneno Yake. Ameyanasibisha kwa mjumbe wa kimalaika na mjumbe wa kianaadamu kwa njia ya kufikisha. Kwa hivyo ni maneno ya Allaah ndiye kaanza kuyazungumza na vilevile ni maneno ya Jibriyl na Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhimaa wa sallam) kwa njia kuwa wamefikisha kutoka kwa Allaah (Jalla wa ´Alaa).

Waislamu hawana shaka juu ya hili ya kwamba ni maneno ya Allaah. Yameteremshwa na wala hayakuumbwa. Amesema (Ta´ala):

إِنَّا أَنزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ

**"Hakika Sisi tumekuteremshia Kitabu." (39:02)**

تَنزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ

**"Ni uteremsho wa Kitabu kutoka kwa Allaah." (39:01)**

مُنَزَّلٌ مِّن رَّبِّكَ بِالْحَقِّ

**"Kimeteremshwa kutoka kwa Mola wako kwa haki." (06:114)**

Allaah (Jalla wa ´Alaa) ameeleza kuwa ni maneno Yake. Amesema (Ta´ala):

وَإِنْ أَحَدٌ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ اسْتَجَارَكَ فَأَجِرْهُ حَتَّىٰ يَسْمَعَ كَلَامَ اللَّهِ ث

**"Ikiwa mmoja wa washirikina akikuomba umlinde, basi mlinde mpaka asikie Maneno ya Allaah." (09:06)**

يُرِيدُونَ أَن يُبَدِّلُوا كَلَامَ اللَّهِ

**"Wanataka kubadilisha Maneno ya Allaah." (48:15)**

Ameyasifu kuwa ni maneno Yake na kwamba Yeye ndiye Mwenye kuyateremsha.

## 16. Radd kwa Ashaa´irah kwamba Qur-aan imechukuliwa kutoka Ubao uliohifadhiwa

Ashaa´irah wanasema kuwa imeandikwa kwenye Ubao uliohifadhiwa na kwamba Jibriyl ameichukua kutoka kwenye Ubao uliohifadhiwa na akateremka nayo kwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Haya ni maneno batili. Jibriyl hakuyachukua kutoka kwenye Ubao uliohifadhiwa. Bali ameyachukua kutoka kwa Allaah (´Azza wa Jall). Ni kweli kwamba yameandikwa kwenye Ubao uliohifadhiwa. Amesema (Ta´ala):

بَلْ هُوَ قُرْآنٌ مَّجِيدٌ فِي لَوْحٍ مَّحْفُوظٍ

**"Bali hii ni Qur-aan tukufu [ilio] kwenye Ubao uliohifadhiwa." (85:21-22)**

وَإِنَّهُ فِي أُمِّ الْكِتَابِ لَدَيْنَا لَعَلِيٌّ حَكِيمٌ

**"Hakika hii iko katika mama wa Kitabu Kwetu, bila shaka imetukuka, yenye hikmah." (43:04)**

Bi maana Qur-aan. Imeandikwa katika Ubao uliohifadhiwa. Hili halina shaka. Lakini hata hivyo Jibriyl hakuyachukua kutoka kwenye Ubao, kama wanavyosema Ashaa´irah, bali aliyachukua kutoka kwa Allaah (Jalla wa ´Alaa). Mambo haya yanatakiwa kutambulika kwa kuwa yametajwa katika ´Aqiydah ya Ashaa´irah.

Shaykh Muhammad bin Ibraahiym (Rahimahu Allaah) ameraddi maneno haya katika kitabu kilichochapishwa kilicho pamoja na fataawaa zake kwa jina "Jawaab-ul-Waadhwih al-Mustaqiym fiy Kayfiyyat-in-Nuzuul al-Qur-aan al-Kariym". Ameraddi na kuyaponda maneno haya. Kwa sababu kusema kwamba yamechukuliwa kutoka katika Ubao uliohifadhiwa ni njia inayopelekea kusema kuwa Allaah ameyaumba kwenye Ubao uliohifadhiwa, kama wanavyosema Jahmiyyah. Haya yamechukuliwa kutoka katika maneno ya Jahmiyyah. Ni maneno batili ambayo ni wajibu kuzinduka nayo.

## 17. Vitabu vyote vya mbinguni ni maneno ya Allaah na hayakuumbwa

Allaah (Jalla wa ´Alaa) katika sifa Zake za kimatendo ni kwamba anazungumza. Kama ambavyo anaumba, anaruzuku, anahuisha na kufisha, anaendesha mambo, anapenda na kutaka (Subhaanahu wa Ta´ala) vilevile anazungumza maneno yanayolingana na utukufu Wake (Subhaanahu wa Ta´ala) kama zilivyo sifa Zake zingine. Anazungumza pindi anapotaka, anachokitaka na namna anayotaka.

Maneno Yake anazungumza anapotaka. Alizungumza kwa Qur-aan wakati wa kuteremka Kwake, anamzungumzisha Jibriyl, alimzungumzisha Muusa na Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) usiku alipandishwa mbingu. Kabla ya hapo alimzungumzisha Aadam (´alayhis-Salaam) na atazungumza siku ya Qiyaamah akiwafanyia watu hesabu. Atawazungumzisha waumini Peponi nao watamzungumzisha. Kwa hivyo anazumgumza kwa maneno aina yake ni ya tagu hapo kale na yanatokea kwa wakati mbalimbali kutegemea na tukio.

Vitabu vyote walivyoteremshiwa Mitume vyote ni maneno ya Allaah (Jalla wa ´Alaa). Miongoni mwayo ni Qur-aan tukufu ambayo ndio kubwa yavyo na Allaah amejaalia kuwa ndio yenye kuvihukumu. Kwa hivyo Qur-aan ni maneno Yake (Jalla wa ´Alaa) ya kihakika na sio *Majaaz.* Qur-aan imeteremka kutoka Kwake na haikuumbwa. Haya ndio madhehebu ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Wanayasema haya kwa mdomo mpana.

## 18. Ambaye hazungumzi hastahiki uola na uungu

Waislamu katika zama za Maswahabah hawakuwa na shaka yoyote kwa hili. Pindi walipojitokeza Jahmiyyah na wakasema kuwa Qur-aan imeumbwa na vilevile Mutazilah, Ashaa´irah na vijukuu vyao ndipo Ahl-us-Sunnah wakawaraddi ya kuwa Qur-aan ni maneno ya Allaah na hayakuumbwa na wakabatilisha maneno yao. Kukisemwa kuwa Qur-aan imeumbwa ina maana kwamba Allaah hazungumzi. Ambaye hazungumzi hastahiki kuwa mungu. Ibraahiym (´alayhis-Salaam) alisema kumwambia baba yake:

إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ يَا أَبَتِ لِمَ تَعْبُدُ مَا لَا يَسْمَعُ وَلَا يُبْصِرُ وَلَا يُغْنِي عَنكَ شَيْئًا

**"Pindi alipomwambia baba yake: "Ee baba yangu! Kwa nini unaabudu vile visivyosikia na visivyoona na visivyokufaa kitu chochote?"" (19:42)**

Kitu kisichosikia na kisichoona. Kitu kisichokuwa na uhai wowote. Katika Aayah nyingine:

وَاتَّخَذَ قَوْمُ مُوسَىٰ مِن بَعْدِهِ مِنْ حُلِيِّهِمْ عِجْلًا جَسَدًا لَّهُ خُوَارٌ ۚ أَلَمْ يَرَوْا أَنَّهُ لَا يُكَلِّمُهُمْ وَلَا يَهْدِيهِمْ سَبِيلًا

**"Watu wa Muusa walijichukulia baada yake katika mapambo yao ndama - kiwiliwili kilichokuwa na sauti kama ya ng'ombe [wakikiabudu]. Je, hawakuona kwamba yeye [ndama huyo] hawazungumzishi na wala hawaongozi njia?" (07:148)**

Hawazungumzishi kwa kuwa ni kitu kisichokuwa na uhai. Ni dalili yenye kuonesha kuwa ambaye hazungumzi hawezi kuwa mungu. Kadhalika imekuja katika Aayah nyingine:

فَأَخْرَجَ لَهُمْ عِجْلًا جَسَدًا لَّهُ خُوَارٌ فَقَالُوا هَٰذَا إِلَٰهُكُمْ وَإِلَٰهُ مُوسَىٰ فَنَسِيَ أَفَلَا يَرَوْنَ أَلَّا يَرْجِعُ إِلَيْهِمْ قَوْلًا

**"Akawatolea umbo la ndama aliye na sauti. Wakasema: "Huyu ndiye mungu wenu na mungu wa Muusaa, lakini [Muusa] amesahau." Je, hawaoni kwamba [ndama huyo] hawarudishii kauli..."**

Bi maana hawazungumzishi.

وَلَا يَمْلِكُ لَهُمْ ضَرًّا وَلَا نَفْعًا

**"... wala hawamiliki kuwadhuru na wala kuwanufaisha?" (20:88-89)**

Kwa ufupi ni kwamba ambaye hazungumzi hastahiki uola na uungu. Kuwa kuwa ni mpungufu. Vipi ataweza kuamrisha, kukataza na kuyaendesha mambo ilihali hazungumzi? Huku ni kumfanya Allaah (Jalla wa ´Alaa) kutokuwa muweza. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

قُل لَّوْ كَانَ الْبَحْرُ مِدَادًا لِّكَلِمَاتِ رَبِّي لَنَفِدَ الْبَحْرُ قَبْلَ أَن تَنفَدَ كَلِمَاتُ رَبِّي

**"Sema: "Kama bahari ingelikuwa ni wino wa [kuandika] maneno ya Mola wangu, basi ingelikauka bahari kabla ya kumalizika maneno ya Mola wangu." (18:109)**

وَلَوْ أَنَّمَا فِي الْأَرْضِ مِن شَجَرَةٍ أَقْلَامٌ وَالْبَحْرُ يَمُدُّهُ مِن بَعْدِهِ سَبْعَةُ أَبْحُرٍ مَّا نَفِدَتْ كَلِمَاتُ اللَّهِ

**"Lau kama miti yote iliyomo katika ardhi ingalikuwa kalamu na bahari [ikafanywa wino], ikaongezewa juu yake bahari saba [zengine]. yasingelimalizika Maneno ya Allaah." (31:27)**

Maneno ya Allaah ambayo anaamrisha na anakataza kwayo daima na siku zote. Maneno ya Allaah hayadhibitikiwi na hayawezi kuandikwa na bahari na kalamu zote za ulimwenguni. Halafu Jahmiyyah wanasema kuwa maneno ya Allaah yameumbwa? Kusema Allaah kuwa hazungumzi na haamrishi na kukataza ni kumsifu Allaah kutokuwa na uwezo. Isitoshe inapelekea vilevile kusema kuwa Qur-aan sio maneno ya Allaah. Pamoja na kuwa Qur-aan ndio msingi wa kwanza katika misingi ya dalili. Ikiwa kweli sio maneno ya Allaah ni vipi yatatumiwa kama dalili?

## 19. Qur-aan sio maneno ya Allaah - njama za kiyahudi

Ni njama za kiyahudi. Kwa kuwa asli ya madhehebu ya Jahmiyyah yamechukuliwa kutoka kwa mayahudi. Hivyo ndivyo alivyosema Shaykh-ul-Islaam (Rahimahu Allaah) katika kitabu chake "al-Hamawiyyah"[11]. Amesema kuwa yamechukuliwa kutoka kwa mayahudi. Hili sio jambo la ajabu kwa mayahudi Allaah awalaani. Wameyapotosha maneno ya Allaah na wakayabadili na kuyageuza. Hizi ni kampeni za mayahudi ili waibatilishe Qur-aan ilio kwenye mikono ya waislamu. Haya ni madhehebu machafu. Kwa ajili hii ndio maana maimamu wakasimama kidete kuiraddi na kuibatilisha na kubainisha kuwa ni kampeni zilizopenyezwa.

[11] Tazama "al-Hamawiyyah al-Kubraa", uk. 232-235

## 20. Haya ndio malengo ya wenye kuwatetea Ahl-ul-Bid´ah

Kuhusu wale wanaosema kuwa masuala ya kusema kuwa Qur-aan imeumbwa hayahitajii kutiliwa umuhimu mkubwa hivo na kwamba ni katika mambo madogo. Haya yanasemwa na baadhi ya waandishi wa leo wapotevu na wenye kujifanya kuwa ni wanachuoni. Haya ni maneno batili na kuchukulia wepesi suala la khatari mno. Haifai kulichukulia usahali. Haya si mambo yasiyokuwa na maana. Huku ni kuwadharau wanachuoni waliosimama na kazi ya kuiraddi na wakaadhibiwa walioadhibiwa, kama Imaam Ahmad, na wakauawa waliouawa katika wao kwa sababu ya kuiraddi. Halafu baada ya haya yote anakuja mtu na kusema kuwa ni mambo madogo tu na hayahitaji yote haya. Mtu huyu ima ni mjinga asiyetambua kitu au anajifanya kuwa ni mjinga na ni mpotevu. Lengo lake anataka wasiraddiwe Jahmiyyah, Mu´tazilah na Ashaa´irah.

Kuna wengine wanaosema kuwa watu wako huru na kwamba watu wasikatane kwa sababu kila mmoja ana uhuru wa kuzungumza. Hii ina maana kwamba batili isiraddiwe na haki isibainishwe. Kila mmoja azungumze anachokitaka. Kwa kufanya hivi dunia nzima itajaa vurugu.

Ni wajibu kuzinduka na propaganda kama hizi na shari hizi zinazoenezwa dhidi ya waislamu.

## 21. Ufalme wa kihakika ni wa Allaah

Amesema mwandishi (Rahimahu Allaah):

*Sema "Hayakuumbwa*

Hii ni Radd kwa Jahmiyyah na wenye kusema maneno yao.

***... maneno ya Mfalme Wetu -*** Mfalme ni Allaah (Jalla wa ´Alaa). Yeye ndiye mfalme. Amesema (Ta´ala):

تَبَارَكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمُلْكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**"Amebarikika ambaye mkononi Mwake umo ufalme Naye juu ya kila kitu ni muweza." (67:01)**

قُلِ اللَّهُمَّ مَالِكَ الْمُلْكِ تُؤْتِي الْمُلْكَ مَن تَشَاءُ وَتَنزِعُ الْمُلْكَ مِمَّن تَشَاءُ وَتُعِزُّ مَن تَشَاءُ وَتُذِلُّ مَن تَشَاءُ ۖ بِيَدِكَ الْخَيْرُ ۖ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

**"Sema: "Ee Allaah Mfalme uliyemiliki ufalme wote! Unampa ufalme umtakaye na unamuondoshea ufalme umtakaye na unamtukuza umtakaye na unamdhalilisha umtakaye - kheri yote imo mkononi mwako. Hakika Wewe juu ya kila kitu ni muweza."" (03:26)**

Allaah (Jalla wa ´Alaa) Yeye ndiye mfalme wa wafalme. Kuhusu ufalme wa wanaadamu ufalme wao ni wa muda. Allaah anampa ufalme yule anayemtaka kisha baadae anamnyakua nao na kumpa mwingine tena.

Kuhusu ufalme wenye kuthibiti na wa daima usioondoka ni ufalme wa Allaah (Jalla wa ´Alaa). Pindi kitaposimama Qiyaamah Allaah (Jalla wa ´Alaa) atauliza:

لِّمَنِ الْمُلْكُ الْيَوْمَ

**"Ufalme ni wa nani hii leo?"**

Hakuna yeyote atayejibu wala kuzungumza. Angelikuweko yeyote aliye na madai angesema kuwa ni yeye. Baada ya hapo Ajijibu Mwenyewe kwa kusema:

لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ

**“Ni wa Allaah pekee Mmoja, Aliye juu." (40:16)**

Hakuna hata mmoja anayepingana na hili. Ufalme ni wa Allaah (Jalla wa ´Alaa). Anampa ufalme yule Amtakaye kwa muda maalum kisha baada ya hapo ima anakufa au anapokonywa kwa mabavu.

Maneno ya mwandishi (Rahimahu Allaah):

***hivyo ndivyo... -*** Bi maana ya kwamba Qur-aan haikuumbwa.

***walivyoamini wachaji Allaah... -*** Bi maana ndivyo maimamu wachaji Allaah walivyoitakidi msemo huu.

***wakaweka wazi -*** Wakawadhihirishia watu na wakasema kuwa Qur-aan imeteremshwa na haikuumbwa. Hawakusema kuwa hii ni mitazamo ya wengine na watu waachwe kwa sababu wana uhuru wa kuzungumza na uhuru wa kuwa na maoni mbalimbali. Kinyume chake waliyaweka mambo wazi kwa hali ya juu na wakabisha na kujadili. Vilevile wakatunga na kuandika [vitabu] kwa ajili ya kuraddi maneno haya. Hilo ni kutokana na khatari na aibu yake. Maneno haya ndani yake kuna kumtukana Allaah (´Azza wa Jall). Wanachuoni hawawezi kunyamazia maneno haya au wakayachukulia usahali.

## 22. Msimamo wa kusimama katika masuala ya kuumbwa kwa Qur-aan

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

04- *Usichukue msimamo wa kusimama katika Qur-aan*

*kama walivyosema wafuasi wa Jahmiy na wakatasahuli*

**MAELEZO**

***Usichukue msimamo***… **-** Katika Jahmiyyah kuna ambao wanasema waziwazi kwamba Qur-aan imeumbwa. Hawa ni wale viongozi wa Jahmiyyah.

Katika wao kuna wengine wanasema kuwa hawasemi kuwa imeumbwa wala haikuumbwa. Wanasema kuwa wanachukua msimamo wa kusimama. Huyu ni shaytwaan bubu. Akisimama watu watafikiria kuwa Qur-aan imeumbwa. Ni lazima kubainisha. Wakisema kuwa imeumbwa basi usinyamaze. Maana yake ni kwamba unawasapoti lakini hata hivyo huweki wazi. Kwa hivyo haijuzu kusimama katika hili.

Haya ni madhehebu ya wasimamaji ambao hawasemi kuwa Qur-aan imeumbwa wala haikuumbwa. Hili maana yake ni kuficha kubainisha haki na ni jambo linatoa ishara kwamba maoni ya Jahmiyyah ni sahihi kwa sababu mtu huyu hakuwaraddi, hakuwafedhehesha na kuwafichua.

Ambaye ana shaka kama Qur-aan imeumbwa au haikuumbwa na badala yake akaamua kusimama, huyu ni Jahmiy. Vinginevyo kama asingalikuwa mtu Jahmiy angesema kwa kinywa kipana. Lakini anajificha kwa kunyamaza.

Uhakika wa mambo ni kuwa huyu ni mbaya zaidi kuliko Jahmiyyah. Kwa sababu wao wameweka wazi na madhehebu yao yakajulikana. Kuhusu mtu huyu anataka kuwapaka watu mchanga wa machoni na kuonesha kuwa ni mnyenyekevu sana na kwamba eti hawezi kuzungumzia mambo haya. Haifai kusimama. Ni lazima kusema kwa kinywa kipana na kubatilisha msemo huu.

***kama walivyosema... -*** Amewafanya kuwa na wao ni katika wafuasi wa Jahmiyyah. Kwa kuwa lau wasingelikuwa ni katika wafuasi wa Jahmiyyah wasingesimama. Kinyume chake wangeliwaraddi na wakasema waziwazi jambo hilo.

Jahmiyyah walipoona kuwa watu hawakubaliani na maneno yao ndio wakakimbia katika hila hii. Lengo ilikuwa wafiche batili yao nyuma yake. Kwa ajili hii pindi Imaam Ahmad alipoulizwa juu ya msimamo wa kusimama akasema yafuatayo:

"Lau hili lingelikuwa kabla ya Jahmiyyah kusema waliyoyasema tungekuwa tunasimama. Ama baada ya wao kusema maneno yao ya aibu, ni lazima kusema wazi kwa kinywa kipana juu ya ubatilifu wake na kuyaraddi."

Haya ni maana ya aliyoyasema Imaam Ahmad kuhusu masuala ya kusimama kwamba Qur-aan imeumbwa.

***wakatasahuli... -*** Bi maana kufanya wepesi na kulainisha. Kutasahuli.

Katika baadhi ya vitabu imekuja:

***wakasamehe***

Bi maana wakasamehe hili. Sawa walitasahuli au walisamehe maana yake ni kwamba hawakukemea. Badala yake ni kwamba walilainisha pamoja na Jahmiyyah na hawakuwakemea. Walichukua msimamo wa kusimama katika masuala haya.

## 23. Msimamo kuhusu matamshi ya Qur-aan

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

05- *Usisemi kuwa kisomo cha Qur-aan kimeumbwa*

*maneno ya Allaah yanawekwa wazi kwa matamshi*

**MAELEZO**

Haya ni madhehebu ya tatu katika masuala haya.

Madhehebu ya kwanza: Wanasema wazi kuwa Qur-aan imeumbwa.

Madhehebu ya pili: Wanasimama. Bi maana hawasemi kuwa imeumbwa wala haikuumbwa.

Madhehebu ya tatu: Matamshi ya Qur-aan yameumbwa. Mtu anasema kuwa matamshi yake ya Qur-aan yameumbwa. Hii ni hila ya kusema kuwa Qur-aan imeumbwa. Haijuzu kwako kusema kuwa matamshi yako ya Qur-aan yameumbwa na wala haijuzu vilevile kusema kuwa matamshi yako ya Qur-aan hayakuumbwa. Ni lazima upambanue. Kwa sababu ukisema kwamba matamshi yako ya Qur-aan yameumbwa na usipambanue, haya ni madhehebu ya Jahmiyyah. Vilevile ukisema kuwa matamshi yako ya Qur-aan hayakuumbwa, huku ni kuwasapoti Jahmiyyah. Kwa kuwa ukisema kwamba matamshi yako ya Qur-aan hayakuumbwa, utakuwa umeingiza matendo yako pamoja na matendo ya Allaah na umefanya kitendo chako hakikuumbwa. Haya ni madhehebu ya Qadariyyah ambao wanapinga Qadar na wanaona kuwa viumbe ndio wanaovumbua na kuumba matendo yao wenyewe.

## 24. Matamshi ya Qur-aan yameumbwa au hayakuumbwa?

Ni lazima kuweka wazi na kuuliza: nini unachokusudia kwa kusema kuwa matamshi yako ya Qur-aan; unakusudia ule utamkaji na sauti au kile kinachotamkwa? Ikiwa unakusudia kile kinachotamkwa hakikuumbwa. Kile kinachotamkwa ni maneno ya Allaah (Jalla wa ´Alaa). Ama matamshi ikiwa unakusudia matamshi unayotamka kwa ulimi wako yameumbwa. Ulimi wako umeumbwa. Kadhalika suati yako imeumbwa. Matamshi yako yameumbwa. Lakini kile chenye kutamkwa hakikuumbwa. Ni lazima kupambanua. Wao wanataka useme kwa jumla ya kwamba matamshi ya Qur-aan yameumbwa au useme hayakuumbwa. Wanaingia kwa hila kama hii. Ni lazima upambanue na uwakatie njie.

Kwa ajili hii ndio maana Ahl-us-Sunnah wanasema kuwa sauti ni ya yule msomaji na maneno ni ya Allaah. Kile chenye kutamkwa ni maneno ya Allaah. Kuhusu matamshi ni maneno yaliyoumbwa. Bi maana sauti yake imeumbwa. Ule utamkaji wake umeumbwa. Kwa ajili hii ndio maana visomo na sauti zinatofautiana. Kuna sauti ambazo ni nzuri na zingine sio nzuri. Kuna sauti za sawa na zingine si za sawa. Hii ni dalili juu ya kwamba sauti imeumbwa. Wasomaji wanatafautiana. Kuna ambao wamepewa sauti nzuri na wengine ni chini ya hapo. Kuhusu maneno ya Allaah (´Azza wa Jall) ni lazima yawe katika upeo wa ukamilifu wa hali ya juu kabisa.

Haikutakikana kuingia katika hili. Lakini wao - yaani Jahmiyyah - ndio ambao wamewafanya waislamu kuingia katika jambo hili. Hivyo ni lazima kulifichua na kulibainisha. Kwa hakika ni msiba. Lau Allaah asingelitenga maimamu wakalibainisha basi jambo hili lingewatatiza watu wengi. Kwa hivyo kuna madhehebu matatu:

Ya kwanza: Jahmiyyah wanaosema kuwa Qur-aan imeumbwa.

Ya pili: Wenye kusimama.

Ya tatu: Watamkaji wanaosema kuwa matamshi ya Qur-aan yameumbwa au hayakuumbwa. Tunawaambia: ni lazima kupambanua. Ikiwa unakusudia ule utamkaji wa sauti umeumbwa. Ama ikiwa unakusudia kile kinachotamkwa na kinachosomwa ni maneno ya Allaah hayakuumbwa. Kwa ajili hii ndio maana imekuja katika Hadiyth:

**"Ipambeni Qur-aan kwa sauti zenu."**[12]

Inatakikana kwa msomaji aipambe sauti yake kwa Qur-aan. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa anapendezeshwa na sauti nzuri ya Qur-aan. Alikuwa akimsikiza Abu Muusa al-Ash´ariy (Radhiya Allaahu ´anh) pindi alipokuwa akiswali usiku. Allaah alikuwa amemtunuku sauti nzuri. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akawa anamsikiliza[13]. Kadhalika alimuamrisha ´Abdullaah bin Mas´uud (Radhiya Allaahu ´anh) amsomee na huku anasikiliza. Akasema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Mimi napenda kuisikia kutoka kwa mwengine asiyekuwa mimi."**[14]

Akamsomea mwanzoni mwa Suurah "an-Nisaa´". Alikuwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akipenda sauti nzuri ya Qur-aan. Kuwa na sauti nzuri ni neema kutoka kwa Allaah (´Azza wa Jall).

---

[12] Abu Daawuud (1468), an-Nasaa´iy (02/179), Ibn Maajah (1342), Ahmad (04/283) na wengineo

[13] al-Bukhaariy (5048) na Muslim (793) na (236).

[14] al-Bukhaariy (4582) na Muslim (800) na (248)

## 25. Kutofautiana kwa watu juu ya Kuonekana kwa Allaah

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

06- *Sema "Allaah atajionyesha kwa viumbe waziwazi*

*kama ambavyo mwezi haufichikani - basi na Mola wako yu waziwazi"*

**MAELEZO**

Haya ni masuala ya Kuonekana kwa Allaah (´Azza wa Jall). Je, viumbe watamuona Allaah au hawatomuona? Jahmiyyah na Mu´tazilah wote wanapinga Kuonekana. Wanasema kuwa Allaah hatoonekana. Hoja yao ni kwamba viwiliwili ndivyo huonekana na wanasema kuwa Allaah hana kiwiliwili. Hivyo hatoonekana. Wanapinga Kuonekana kabisa si duniani wala Aakhirah. Tunamuomba Allaah afya.

Kuna wengine wanaosema kuwa Allaah anaonekana duniani na Aakhirah. Haya ni maneno ya baadhi ya Suufiyyah.

Maoni ya tatu - na haya ndio maoni ya watu wa haki - ni kwamba Allaah (´Azza wa Jall) ataonekana Aakhirah. Watu wa Peponi watamuona. Kumethibiti Hadiyth tele juu ya hilo zilizopokelewa kwa mapokezi mengi kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kuhusu duniani Hatoonekana. Watu hawawezi kumuona Allaah duniani. Pindi Muusa (´alayhis-Salaam) alipomuomba kumuona Allaah (Subhaanah) hapa duniani kwa kusema:

قَالَ رَبِّ أَرِنِي أَنظُرْ إِلَيْكَ ۚ قَالَ لَن تَرَانِي وَلَـٰكِنِ انظُرْ إِلَى الْجَبَلِ فَإِنِ اسْتَقَرَّ مَكَانَهُ فَسَوْفَ تَرَانِي ۚ فَلَمَّا تَجَلَّىٰ رَبُّهُ لِلْجَبَلِ جَعَلَهُ دَكًّا وَخَرَّ مُوسَىٰ صَعِقًا ۚ فَلَمَّا أَفَاقَ قَالَ سُبْحَانَكَ تُبْتُ إِلَيْكَ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُؤْمِنِينَ

**"Akasema: "Mola wangu! Nionyeshe ili nikutazame." Akasema: "(Lan) Hutoniona! Lakini tazama jabali. Likitulia mahali pake, basi utaniona." Basi Mola wako alipojidhihirisha katika jabali akalifanya livurugike kuwa vumbi na Muusa akaanguka hali ya kuzimia. Alipozindukana akasema:**

**"Utakasifu ni Wako! Nimetubu Kwako nami ni wa kwanza wa wanaoamini."" (07:143)**

Mlima ulipasuka na ukageuka udongo kutokana na ukubwa wa Allaah (´Azza wa Jall). Ni vipi binaadamu ataweza kumuona Allaah? Hili ni kuhusiana na duniani.

Kuhusu Aakhirah Allaah atawapa nguvu watu wa Peponi ambazo kwazo wataweza kumuona Allaah (´Azza wa Jall). Huku ni kuwakirimu. Pindi walipomuamini duniani pasi na kumuona ndipo Allaah akawarimu na akajionyesha kwao Peponi ili waburudike na kule kumuona. Qur-aan na Sunnah iliyopokelewa kwa mapokezi mengi imefahamisha hivyo.

Ama makafiri ilipokuwa hawakumuamini duniani ndipo Allaah akawazuia kumuona siku ya Qiyaamah. Amesema (Ta´ala):

كَلَّا إِنَّهُمْ عَن رَّبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّمَحْجُوبُونَ

**"Hapana! Hakika wao siku hiyo watawekewa kizuizi [wasimuone] Mola wao." (83:15)**

Ikiwa makafiri wao watazuiawa na kumuona Mola wao basi mtu anapata kufahamu kupitia hili ya kwamba waumini hawatozuiwa na kumuona Mola wao. Vinginevyo makafiri na waumini wangalikuwa sawa Aakhirah. Allaah ametafautisha kati yao. Amewakirimu waumini kwa kujionyesha kwao (Subhaanahu wa Ta´ala) kama inavyolingana na utukufu Wake. Watamuona waziwazi kwa macho yao na hawatosongamana katika kumuona. Bi maana hawatokuwa na msongamano katika kumuona. Watamuona waziwazi kwa macho yao kama wanavyoliona jua waziwazi pasi na mawingu na kama wanavyouona mwezi mg´aro. Haya ni mashabihisho ya maono na sio ya kitachoonwa. Hivyo ndivyo zimesihi Hadiyth kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Haya ndio madhehebu ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah kuhusu Kuonekana kwa Allaah (´Azza wa Jall).

Jambo muhimu analotakiwa mwanafunzi kushikamana nalo ni kumdhukuru Allaah (´Azza wa Jall) katika kila hali na kila wakati.

## 26. Baadhi ya Aayah zinazothibitisha Kuonekana kwa Allaah Aakhirah

Allaah (´Azza wa Jall) amesema:

لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ

**"Kwa wale waliofanya mazuri watapata Pepo na zaidi." (10:26)**

*al-Husnaa* maana yake ni Pepo. Zaidi maana yake ni kuona uso wa Allaah. Hivyo ndivyo ilivyokuja katika "as-Swahiyh" ya Muslim[15].

Amesema (Ta´ala):

لَهُم مَّا يَشَاءُونَ فِيهَا وَلَدَيْنَا مَزِيدٌ

**"Watapata humo wayatakayo na Kwetu kuna yaliyo zaidi" (50:35)**

Watapata humo wayatakayo bi maana Peponi. Kwetu kuna yaliyo zaidi bi maana kumuona Allaah (Jalla wa ´Alaa).

Amesema vilevile (Ta´ala):

وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ

**"Kuna nyuso siku hiyo zitanawiri. Zikimtazama Mola wake." (75:22-23)**

Bi maana kwa macho yao. Kwa sababu "*an-Nadhwra*" ikifuatiwa na "*ilaa*" maana yake ni kuona kwa macho.

Ama "*an-Nadhwra*" ikiwa peke yake maana yake ni kusimama na kusubiri.

Lakini "*an-Nadhwra*" ikifuatiwa na "*fiy*", kama ilivyo katika maneno Yake (Ta´ala):

أَوَلَمْ يَنظُرُوا فِي مَلَكُوتِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ

[15] Muslim (181) na (297)

**"Je, hawazingatii (*fiy)* ufalme wa mbingu na ardhi." (07:185)**

maana yake inakuwa kufikiria na kuzingatia.

Kwa ufupi ni kwamba "*an-Nadhwra*" iko ifuatavyo:

Mosi: Ikija peke yake maana yake ni kusubiri.

Pili: Ikifuatiwa na "*fiy*" maana yake ni kufikiria na kuzingatia.

Tatu: Ikifuatiwa na "*ilaa*" maana yake ni kutazama kwa macho.

Hizi ndio kanuni.

Aayah tulionayo imefuatiwa na "*ilaa*"*:*

إِلَىٰ رَبِّهَا نَاظِرَةٌ

**"(*ilaa*) Zikimtazama Mola wake." (75:22-23)**

Maana yake ni kuona kwa macho.

Kuhusu maneno Yake (Ta´ala):

لَّا تُدْرِكُهُ الْأَبْصَارُ وَهُوَ يُدْرِكُ الْأَبْصَارَ

**"Macho hayamzunguki bali Yeye anayazunguka macho yote." (06:103)**

Kuzunguka haina maana ya kuona. Wewe unaweza kukiona na kukitazama kitu lakini usikidiriki bi maana usikizunguki. Huwezi kukizunguka chenye kuonwa kwa kila pande ingawa unakiona. Waumini watamuona Mola Wao siku ya Qiyaamah lakini pamoja na hivyo hawatomzunguka. Kwa msemo mwingine hawatomzunguka ukubwa Wake (Jalla wa ´Alaa) na hawamzingiri kielimu. Wewe unaliona jua lakini huwezi kulizunguka kutokana na ukali wake. Hili ni kuhusu kiumbe. Vipi kuhusu Muumbaji (Subhaanahu wa Ta´ala)? Kukanushwa uzingirwaji sio kukanushwa kuonekana. Uhakika wa mambo ni kwamba wamesema kukanushwa uzingirwaji kunatolea dalili ya

kwamba Ataonekana lakini hata hivyo hatodirikiwa. Bi maana hatozungukwa (Subhaanahu wa Ta´ala).

Kuhusu maneno ya Allaah kumwambia Muusa:

لَن تَرَانِي

**"(Lan) Hutoniona!" (07:143)**

Haina maana ya makanusho ya milele. Maneno Yake:

لَن تَرَانِي

**"(Lan) Hutoniona!"**

Bi maana duniani. Hilo ni kwa dalili ya kwamba Kuonekana kumethibiti Aakhirah.

Wasomi wa lugha wanasema kuwa neno "lan" sio la makanusho ya milele. Bali ni la makanusho ya muda fulani.

***atajionesha... -*** Bi maana atajidhihirisha (Subhaanahu wa Ta´ala). Atajiondoshea pazia (Jalla wa ´Alaa).

***kama ambavyo mwezi haufichikani... -*** Haya yamechukuliwa kutoka katika maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Hakika nyinyi mtamuona Mola wenu kama mnavyouona mwezi huu katika usiku wa m´garo."[16]**

Usiku wa mng´aro ni usiku wa tarehe kumi na tano au kumi na nne. Ni usiku ambao mwezi unakuwa mkubwa kwelikweli. Kwa kuwa mwezi mwanzoni mwa mwezi unakuwa dhaifu. Halafu baada ya hapo unaenda unakuwa mkubwa zaidi na zaidi mpaka unatimia katika zile nyusiku za mng´aro. Kisha unapungua tena na kuwa mwembamba. Amesema (Ta´ala):

[16] al-Bukhaariy (7439) na Muslim (183) na (302)

وَالْقَمَرَ قَدَّرْنَاهُ مَنَازِلَ حَتَّىٰ عَادَ كَالْعُرْجُونِ الْقَدِيمِ

**"Mwezi Tumeukadiria vituo mpaka ukarudi [mwembamba] kama kwamba karara la shina la mtende lililopinda la zamani." (36:39)**

## 27. Kumtakasa Allaah kutokana na mtoto na baba

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

07- *Hana mtoto wala Hana baba*

*na wala hana mwenza - Ametakasika msabihiwaji*

**MAELEZO**

Haya yamechukuliwa kutoka katika maneno ya Allaah (Ta´ala) katika Suurah "al-Ikhaasw":

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ اللَّهُ الصَّمَدُ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Kwa jina la Allaah, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Sema: "Yeye ni Allaah Mmoja Pekee. Allaah ndiye mkusudiwa. Hakuzaa na wala hakuzaliwa na wala hakuna yeyote anayefanana na kulingana Naye." (112:01-04)**

Imeitwa kuwa ni Suurah "al-Ikhaasw" kwa kuwa imeitakasa Tawhiyd. Qur-aan imegawanyika sehemu tatu:

Ya kwanza: Tawhiyd. Maelezo kuhusu Allaah, kumuabudu na makatazo ya kumshirikisha.

Ya pili: Maamrisho na makatazo Yake. Ni yale ya halali na haramu na hukumu za Kishari´ah.

Ya tatu: Maelezo juu ya Mitume, nyumati, yaliyotangulia na yaliyoko mbele, Pepo na Moto.

Suurah hii imetakasa aina ya kwanza ambapo ni maelezo juu ya Allaah (Jalla wa ´Alaa). Ni kuhusu Tawhiyd. Ndio maana ikawa ni sawa na theluthi ya Qur-aan inapokuja katika fadhila[17]. Kwa sababu imetakasa kumpwekesha

[17] al-Bukhaariy (5013).

Allaah (´Azza wa Jall). Hii ndio sababu ikaitwa Suurah "al-Ikhaasw". Ndani yake mna makanusho na mathibitisho. Inamkanushia Allaah kuwa na mapungufu na wakati huo huo inamthibitishia Allaah (Jalla wa ´Alaa) ukamilifu:

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ

**"Sema: “Yeye ni Allaah Mmoja Pekee."**

Haya ni mathibitisho.

اللَّهُ الصَّمَدُ

**"Allaah ndiye mkusudiwa."**

Haya ni mathibitisho.

لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Hakuzaa na wala hakuzaliwa na wala hakuna yeyote anayefanana na kulingana Naye."**

Haya ni makanusho. Amejikanushia mapungufu na wakati huo huo akajithibitishia ukamilifu. Maneno Yake:

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ

**"Sema: “Yeye ni Allaah Mmoja Pekee."**

Bi maana ni mmoja asiyekuwa na mshirika si katika uola, uungu wala katika majina na sifa Zake. Ni Mmoja Pekee katika vigawanyo vitatu vya Tawhiyd. Maneno Yake:

اللَّهُ الصَّمَدُ

**"Allaah ndiye mkusudiwa."**

Bi maana anayekusudiwa na viumbe na wanaomba kutoka Kwake haja mbalimbali. Kisha akakanusha na kusema:

لَمْ يَلِدْ

**"Hakuzaa... "**

Bi maana hana mtoto. Hakika Yeye (Subhaanah) ametakasika kutokamana na kuwa na mtoto.

## 28. Radd kwa wenye kumfanyia Allaah kuwa na watoto

Hii Radd kwa wale waliomthibitishia Allaah kuwa na mtoto ambao ni wafuatao:

Wa kwanza: Manaswara ambao wamesema kuwa al-Masiyh ni mwana wa Allaah.

Wa pili: Mayahudi ambao wamesema kuwa ´Uzayr ni mwana wa Allaah.

Wa tatu: Washirikina ambao wamesema kuwa Malaika ni wasichana wa Allaah. Wamemfanya Allaah kuwa na wasichana ilihali wao wenyewe wanawachukia. Amesema (ta´ala):

وَيَجْعَلُونَ لِلَّهِ مَا يَكْرَهُونَ

**"Wanamfanyia Allaah yale wanayoyachukia... "**

Wao wenyewe wanawachukia wasichana. Ni vipi basi watamjalia nao Allaah (Jalla wa ´Alaa)? Amesema (Ta´ala):

وَتَصِفُ أَلْسِنَتُهُمُ الْكَذِبَ أَنَّ لَهُمُ الْحُسْنَىٰ

**"... na ndimi zao zinaeleza uongo kwamba watapata mema." (16:62)**

Amesema vilevile:

أَمْ لَهُ الْبَنَاتُ

**"Au Yeye ana wasichana... "**

Mnamfanya Yeye kuwa na wasichana ilihali nyinyi wenyewe mnawachukia.

وَلَكُمُ الْبَنُونَ

**"... nanyi mna watoto wa kiume?" (52:39)**

Nyinyi wenyewe ndio mnafanya kuwa na wavulana mnaowapenda. Amesema (Ta´ala):

وَيَجْعَلُونَ لِلَّهِ مَا يَكْرَهُونَ وَتَصِفُ أَلْسِنَتُهُمُ الْكَذِبَ أَنَّ لَهُمُ الْحُسْنَىٰ

**"Wanamfanyia Allaah yale wanayoyachukia na ndimi zao zinaeleza uongo kwamba watapata mema." (16:62)**

Amesema (Subhaanahu wa Ta´ala):

وَجَعَلُوا لَهُ مِنْ عِبَادِهِ جُزْءًا

**"Wakamfanyia kati ya waja Wake sehemu." (43:15)**

Kwa kuwa mtoto ni sehemu ya baba. Wao wamemshabihisha Allaah (Jalla wa ´Alaa) na viumbe na wakamfanya kuwa na watoto ilihali Yeye ametakasika kutokana na hayo. Kisha akasema (Jalla wa ´Alaa):

أَوَمَن يُنَشَّأُ فِي الْحِلْيَةِ وَهُوَ فِي الْخِصَامِ غَيْرُ مُبِينٍ

**"Hivi kweli yule aliyelelewa katika mapambo naye katika mabishano si mbainifu." (43:18)**

Mwanamke analelewa katika mapambo. Ni mpungufu anahitaji mapambo. Mwanamke ni mpungufu.

وَهُوَ فِي الْخِصَامِ غَيْرُ مُبِينٍ

**"... katika mapambo naye katika mabishano si mbainifu."**

Wakati wa mabishano na magomvi mwanamke anadhoofika na wala hayawezi mabishano. Kwa ajili hii mara nyingi mwanamke huwakilisha mtu wa kumbishia. Amesema (Ta´ala):

وَجَعَلُوا الْمَلَائِكَةَ الَّذِينَ هُمْ عِبَادُ الرَّحْمَٰنِ إِنَاثًا

**"Wakawafanya Malaika ambao ni waja wa Mwingi wa Rahmah kuwa ni wa kike."**

Wakasema kuwa ni wasichana wa Allaah.

أَشَهِدُوا خَلْقَهُمْ ۚ سَتُكْتَبُ شَهَادَتُهُمْ وَيُسْأَلُونَ

**"Je, kwani wao wameshuhudia uumbaji wao? Utaandikwa ushahidi wao na wataulizwa." (43:19)**

Washirikina wamemsifu Allaah kuwa ana watoto wa kike. Manaswara wamemsifu Allaah kuwa ana mtoto wa kiume ambaye ni al-Masiyh mwana wa Maryam (´alayhis-Swalaatu was-Salaam). Uhakika wa mambo Yeye ni Mtume na mja wa Allaah.

قَالَ إِنِّي عَبْدُ اللَّهِ آتَانِيَ الْكِتَابَ وَجَعَلَنِي نَبِيًّا

**"Akasema: "Hakika mimi ni mja wa Allaah. Amenipa Kitabu na amenijaalia kuwa Nabii."" (19:30)**

إِنْ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ وَجَعَلْنَاهُ مَثَلًا لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ

**"Yeye si jengine isipokuwa ni mja Tuliyemneemesha na Tukamfanya ni mfano kwa wana wa Israaiyl." (43:59)**

´Iysaa ni mja na Mtume wa Allaah ambaye ni neno Lake alilompelekea Maryam na ni roho. Kwa hiyo yeye sio mtoto wa Allaah (´Azza wa Jall). Allaah (Subhaanah):

لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ

**"Hakuzaa na wala hakuzaliwa." (112:04)**

Hakika Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) Hana mwanzo kama ambavyo vilevile Hana mwisho. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akiomba du´aa na kusema:

**"Wewe ndiye wa kwanza na hakuna kabla Yako kitu na Wewe ndiye wa mwisho na hakuna kitu baada yako na Wewe ndiye Uliye juu na hakuna juu Yako kitu na Wewe ndiye Uliye karibu zaidi hakuna kilicho karibu zaidi Yako."**[18]

Hizi ndio sifa za Allaah (Jalla wa ´Alaa). Yeye ni wa kwanza pasi na kuwa na mwanzo na ni mwenye kudumu pasi na kuwa na mwisho (Subhaanahu wa Ta´ala). Maneno Yake (Ta´ala):

وَلَمْ يُولَدْ

**"... na wala hakuzaliwa."**

Haya ni makanusho ya kuwa na washirika na wenye kushabihiana Naye. Mtoto hushabihiana na baba yake na ni mshirika wake. Jengine ni kwamba mtoto anakuwa kwa sababu ya haja ilihali Allaah (Subhaanah) ni mkwasi wa hayo:

هُوَ الْغَنِيُّ ۖ لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

**"Yeye ni mkwasi - ni Vyake vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini." (10:68)**

Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) ni mkwasi kutokana na mtoto. Kuhusu nyinyi ni wenye kuhitajia watoto. Mtu asiyeweza kupata mtoto anakuwa si muweza na ana udhaifu. Ni mwenye kuhitajia mtoto wa kumsaidia. Maneno Yake (Ta´ala):

وَلَمْ يُولَدْ

**"... na wala hakuzaliwa."**

Haya ni makanusho.

[18] Muslim (61) na (2713)

Maneno Yake (Ta´ala):

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"... na wala hakuna yeyote anayefanana na kulingana Naye."**

Maana yake yaani hana mwenza na mshirika. Allaah (Jalla wa ´Alaa) hana anayeshabihiana Naye wala anayefanana Naye. Kwa msemo mwingine ni kwamba hakuna yeyote anayefanana Naye, kuwa sawa Naye na kushabihiana Naye. Amesema (Ta´ala):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye." (42:11)**

Huku ni kukanusha washirika na wenza. Amesema (Ta´ala):

هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا

**"Je, unamjua mwengine anaye jina kama Lake?" (19:65)**

Bi maana mnamjua mwengine aliye sawa au ambaye ana jina kama Lake (Subhaanah) kihakika? Haina maana kwamba hakuna yeyote anayeitwa jina Lake kwa mfano mfalme na mtukufu. Maneno ya mwandishi (Rahimahu Allaah):

*Hana mtoto wala Hana baba*

Yamechukuliwa kutoka katika Suurah "al-Ikhlaasw" ambamo ndani yake kuna uthibitisho wa umoja na ukusudiwaji kwa Allaah na kumkanushia mwana na baba na vilevile kumkanushia kushabihiana Naye (Subhaanahu wa Ta´ala). Hashabihiani na yeyote katika viumbe Wake.

## 29. Sema kama alivyosema Mtume (´alayhis-Salaam)

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

08- *Jahmiy anaweza kuyapinga haya*

*sisi kwa ukweli wa tuliyoyasema tuna Hadiyth zilizoweka wazi*

09- *Jariyr amepokea kutoka katika maneno ya Muhammad*

*juu ya hayo utafaulu*

**MAELEZO**

Jahmiy anaweza kupinga Kuonekana kwa Allaah (´Azza wa Jall) Aakhirah. Hawana mashiko yoyote kwa hayo. Kuhusu sisi katika kuthibitisha Kuonekana tuna Hadiyth nyingi zilizopokelewa kwa njia nyingi kutoka kwa kundi la Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum). Ibn-ul-Qayyim (Rahimahu Allaah) amezipokea katika "Haadi al-Arwaah ilaa Bilaad-il-Afraah". Ni kitabu kinachozungumzia Pepo, kimeisifu na kuelezea yaliyomo ndani yake. Ndani yake ametaja Kuonekana kwa Allaah na amesimulia vilevile Hadiyth zilizothibiti kwa mapokezi mengi kwa mtiririko wake, mlolongo wa wapokezi wake na mapokezi yake.

***Jariyr... -*** Anaitwa Jariyr bin ´Abdillaah al-Bajaliy (Radhiya Allaahu ´anh). Ni mmoja miongoni mwa wapokezi katika Maswahabah. Vinginevyo kuna Maswahabah wengine waliopokea. Amechotaka mwandishi (Rahimahu Allaah) ni kupigia mfano peke yake.

***... kutoka katika maneno ya Muhammad -*** Bi maana Jariyr alipokea kutoka katika maneno ya Mtume wa Allaah Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

***sema kama alivyosema... -*** Bi maana sema kama alivyosema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) utafaulu. Usiende kinyume na maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ukaja kula khasara. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hatamki kwa matamanio yake:

وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ

**"Wala hatamki kwa matamanio. Hayo ayasemayo si chochote isipokuwa ni *Wahy* unaofunuliwa kwake." (53:03-04)**

Maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni haki na hayaingiliwi na shaka yoyote.

## 30. Allaah ana sifa za kidhati na za kimatendo

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

10- *Jahmiy anaweza vilevile kupinga mkono Wake wa kuume*

*mikono Yake yote miwili kwa fadhila ni mikunjufu*

**MAELEZO**

Jahmiy ni ambaye yuko katika madhehebu ya Jahmiy bin Swafwaan. Mtu huyu alichukua madhehebu yake kutoka kwa Ja´d bin Dirham.

***Jahmiy anaweza... -*** Bi maana wafuasi wa Jahmiy wanapinga majina na sifa. Haya ni moja katika madhehebu yake machafu. Vinginevyo ana madhehebu machafu katika mambo mengi. Miongoni mwa mambo hayo ni kupinga majina na sifa.

***... anaweza... -*** Bi maana hakika. Ni kama mfano wa kusema "hakika wakati wa swalah umewadia". Ni kama mfano wa maneno Yake (Ta´ala):

لَّقَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ فَقِيرٌ وَنَحْنُ أَغْنِيَاءُ ۘ سَنَكْتُبُ مَا قَالُوا

**"Hakika Allaah ameyasikia maneno ya wale waliosema: "Hakika Allaah ni fakiri na sisi ni matajiri." Tutayaandika waliyoyasema."" (03:181)**

"Inaweza" (*Qad*) wakati mwingine inakuja ikiwa na maana ya hakika. Hayo ndio makusudio hapa. Wakati mwingine inaweza kuja kwa maana ya pengine. Kama kusema "bakhili anaweza kuwa mkarimu". Hapa imekuja kwa maana ya pengine. Lakini iliyokuja hapa sio kwa njia ya pengine. Bali ni kwa njia ya hakika. Ni kama mfano wa maneno Yake (Ta´ala):

قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الْمُعَوِّقِينَ

**"Hakika Allaah ameshajua wenye kuweka kizuizi." (33:18)**

Hii imekuja kwa njia ya kuyakinisha.

***... vilevile... -*** Bi maana kama ambavyo wamekanusha Kuonekana kwa Allaah (´Azza wa Jall), kadhalika wanapinga kumthibitishia Allaah kuwa na mikono miwili.

Allaah (´Azza wa Jall) ana sifa za kidhati. Kama mfano wa mikono miwili, uso, miguu na vidole. Kadhalika Ana sifa za kimatendo. Kama mfano wa kushuka, kulingana, maneno na kuumba.

Kila dalili iliyokuja kumthibitishia Allaah sifa ya kidhati, basi na sisi vilevile tunamthibitishia Allaah (´Azza wa Jall). Tofauti na wanavyofanya wakanushaji (*Mu´attwilah*) ambao wanakanusha majina na sifa za Allaah. Katika kilele chao kuna Jahmiyyah. Tofauti vilevile na wafananishaji (*Mumaththilah*) ambao wakapetuka katika kuthibitisha mpaka wanazithibitisha sifa za Allaah na sifa za viumbe Wake. Wamoja wamepetuka mpaka katika kutakasa mpaka wakafikia kukanusha majina na sifa za Allaah. Wengine wamepetuka mpaka katika kuthibitisha mpaka wakamshabihisha Allaah na viumbe Wake.

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ndio wako kati na kati baina ya makundi hayo mawili. Wanamthibitishia Allaah zile sifa za kidhati na za kimatendo Alizojithibitishia Mwenyewe. Tofauti na wanavyofanya wakanushaji. Wanathibitisha pasi na kufananisha. Tofauti na wanavyofanya wafananishaji. Amesema (Ta´ala):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye Ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)**

Katika maneno Yake:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye."**

Hii ni Radd kwa wafananishaji.

وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**"Naye Ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona."**

Hii ni Radd kwa wakanushaji.

Haya ndio madhehebu ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.

## 31. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya mikono ya Allaah

Allaah (Jalla wa ´Alaa) ana sifa za kidhati na za kimatendo. Sifa za kimatendo ni kama Ujuu, kushuka, kuumba, kuruzuku, maneno na sifa nyenginezo za matendo Yake (Subhaanahu wa Ta´ala).

Miongoni mwa sifa Zake za kimatendo ni mikono miwili. Imethibiti katika maneno ya Allaah (´Azza wa Jall) na katika Sunnah za Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Amesema (Ta´ala):

وَالسَّمَاوَاتُ مَطْوِيَّاتٌ بِيَمِينِهِ

**"Mbingu zitakunjwa mkononi Mwake wa kulia." (39:67)**

قَالَ يَا إِبْلِيسُ مَا مَنَعَكَ أَن تَسْجُدَ لِمَا خَلَقْتُ بِيَدَيَّ

**"Akasema: "Ee Ibliys! Nini kilichokuzuia usimsujudie Niliyemuumba kwa mikono Yangu?"" (38:75)**

Bi maana Aadam (´alayhis-Swalaatu was-Salaam).

Katika Hadiyth imekuja:

**"Mikono ya Allaah imejaa inatoa usiku na mchana."[19]**

Kuna Hadiyth zingine Swahiyh ambazo zimemthibitishia Allaah (´Azza wa Jall) kuwa na mikono miwili na mmoja. Maana yake inajulikana katika lugha. Ni mikono miwili ya kihakika. Lakini hata hivyo sio kama mikono ya viumbe. Ni mikono miwili inayolingana na utukufu na ukubwa wa Allaah. Hakuna anayejua namna ilivyo isipokuwa Allaah (Jalla wa ´Alaa). Sisi tunaithibitisha kutokana na maana yake ya kihakika na wakati huo huo tunakanusha ufananishaji na ushabihishaji. Haifanani na mikono ya viumbe. Haya ndio

[19] al-Bukhaariy (7419) na Muslim (36) na (993)

madhebeu ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Ni madhehebu yanaenda kwa mujibu wa Qur-aan na Sunnah. Mwenendo wao katika hayo ni mwenendo ule ule inapokuja katika majina na sifa za Allaah (´Azza wa Jall) zingine.

## 32. Radd kwa wanaokanusha Allaah kuwa na mikono

Kuhusu wakanushaji ambao wanakanusha mikono miwili ya Allaah (Jalla wa ´Alaa) - kama ambavyo vilevile wanakanusha sifa zingine zote - wanaipindisha maana mikono ya kwamba maana yake ni nguvu au kwamba maana yake ni neema. Wanasema kuwa mikono ya Allaah maana yake ni nguvu. Wanafasiri maneno Yake (Ta´ala):

لِمَا خَلَقْتُ بِيَدَيَّ

**"Niliyemuumba kwa mikono Yangu." (38:75)**

kwamba maana yake ni nguvu Zangu. Tunawaraddi kwa kuwaambia: Allaah (´Azza wa Jall) ameitaja mikono kwa njia ya uwili. Je, Allaah (Jalla wa ´Alaa) ana nguvu mbili au ana nguvu moja? Jibu ni kuwa Allaah ana nguvu moja. Si sawa kusema kwamba Allaah ana nguvu mbili. Maneno Yake:

لِمَا خَلَقْتُ بِيَدَيَّ

**"Niliyemuumba kwa mikono Yangu."**

Je, mtu anawea kusema:

"Niliyemuumba kwa nguvu zangu mbili."?

Hakuna hata mmoja aliyesema hivi.

Kuhusu kuipindisha kwao kwamba maana yake ni neema. Wanasema ni kama mfano wa mtu kusema "wewe una mkono kwangu" akikusudia "wewe una zawadi kwangu". Hivyo wanafasiri:

لِمَا خَلَقْتُ بِيَدَيَّ

**"Niliyemuumba kwa mikono Yangu."**

kwamba maana yake ni neema zangu mbili. Tunawaraddi kwa kusema: Je, Allaah (Jalla wa ´Alaa) hana isipokuwa neema mbili peke yake au uhakika wa mambo ni kuwa neema zote zinarejea Kwake (Subhaanahu wa Ta´ala)?

Jengine ni kuwa mikono miwili ya Allaah ikifasiriwa kuwa ni nguvu kutakuwa hakuna tofauti kati ya Aadam na viumbe wengine. Itakuwa Allaah ameumba viumbe wote kwa nguvu Zake (Subhaanahu wa Ta´ala). Hivyo Aadam (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) atakuwa hana tofauti na wengine. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amempambanua aliposema:

لِمَا خَلَقْتُ بِيَدَيَّ

**"Niliyemuumba kwa mikono Yangu."**

Hivi ndivyo wanavyoraddiwa watu hawa.

## 33. Radd kwa wanaoifananisha mikono ya Allaah na ya viumbe

Kuhusu wafananishaji Qur-aan imewaraddi. Allaah (Ta´ala) amesema:

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye." (42:11)**

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

**"Na wala hakuna yeyote anayefanana na kulingana Naye." (112:04)**

هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا

**"Je, unamjua mwengine anaye jina kama Lake?" (19:65)**

فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ

**"Basi msimfanyie Allaah wenza na hali ya kuwa nyinyi mnajua." (02:22)**

Mwenza ni anayeshabihiana na kufanana Naye. Amekataza kumfanyia Allaah anaoshabihiana na kufanana Naye kutoka katika viumbe Wake (Subhaanahu wa Ta´ala). Hakuna kitu kinachofanana Naye.

Haya ndio madhehebu ya Jahmiyyah katika masuala ya mikono miwili ya Allaah (´Azza wa Jall). Wanaraddiwa namna hii vile walivyopindisha. Ndio madhehebu vilevile ya wafananishaji na wakanushaji na wanaraddiwa kupitia maneno ya Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).

## 34. Mikono miwili ya Allaah yote ni ya kuume

Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

وَالسَّمَاوَاتُ مَطْوِيَّاتٌ بِيَمِينِهِ

**"Mbingu zitakunjwa mkononi Mwake wa kulia." (39:67)**

Katika Hadiyth kumetajwa mkono wa kulia na wa kushoto yote miwili. Lakini hata hivo akasema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Mikono Yake yote ni ya kuume."[20]**

Ni mkono wa kushoto ukiwa na maana ya wa kuume. Hilo ni kutokana na kumtakasa Allaah (´Azza wa Jall) kutokamana na mapungufu. Kwa kuwa huenda akisikia mwenye kusikia kuhusu Allaah kuthibitishiwa mkono wa kushoto, huenda akaingiwa akilini mwake kwamba ni kama mfano wa mkono wa kushoto wa kiumbe. Kwa sababu mkono wa kushoto wa kiumbe sio kama mkono wa kulia. Mkono wake wa kushoto una kasoro. Jengine kama mnavojua ni kuwa mkono wa kushoto ni wenye kuondosha taka na kujisafisha. Kuhusu mkono wa kuume ni bora zaidi na ndio mkono wenye kupokea na kupeana kitu, kula, kunywa na mengineyo. Hivyo akisikia mwenye kusikia kuwa Allaah anathibitishiwa mkono wa kushoto, huenda akaingiwa akilini mwake kwamba na wenyewe ni mpungufu kuliko mkono wa kuume, kama ilivyo kwa viumbe. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akakanusha fikira hizi na akasema:

**"Mikono Yake yote ni ya kuume."**

***... mikonoYake yote miwili... -*** Bi maana mikono ya Allaah (Jalla wa ´Alaa).

***... kwa fadhila... -*** Bi maana kwa kutoa na neema.

[20] Muslim (18) na (1827)

***... ni mikunjufu... -*** Bi maana inatoa kuwapa na kuwatunuku viumbe. Imekuja katika Hadiyth:

**"Mikono Yake imejaa inatoa usiku na mchana. Hivi huoni Alivyotoa tangu kuumbwe mbingu na ardhi. Hakika havijapungua vilivyomo kwenye mkono Wake wa kuume."**

Hakika Yeye (Jalla wa ´Alaa) anatoa vya kutoa pasi na mpaka wala kikomo. Anatoa kwa mkono Wake mtukufu kuwapa waja Wake.

***mikonoYake yote miwili kwa fadhila... -*** Bi maana kwa kutoa na kwa fadhila za Allaah.

***... mikunjufu -*** Bi maana ni yenye kuendelea kutoa pasi na Allaah (Subhnaanahu wa Ta´ala) kukatikiza.

Mayahudi - Allaah awakebehi - pindi walipomsifu Allaah (Jalla wa ´Alaa) kwa ubakhili wakasema:

يَدُ اللَّهِ مَغْلُولَةٌ

**“Mkono wa Allaah umefumbwa."**

Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) akasema:

غُلَّتْ أَيْدِيهِمْ وَلُعِنُوا بِمَا قَالُوا ۘ بَلْ يَدَاهُ مَبْسُوطَتَانِ يُنفِقُ كَيْفَ يَشَاءُ

**"Bali mikono Yake imefumbuliwa hutoa Atakavyo." (05:64)**

Bi maana imefumbuliwa kwa ukarimu na kwa kutoa.

## 35. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya kushuka kwa Allaah

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

11- *Sema "Jabbar hushuka katika kila usiku*

*bila ya namna ametukuka Mmoja mwenye kuhimidiwa"*

**MAELEZO**

***Sema... -*** Bi maana sema ee Sunniy ambaye umeshikamana na Qur-aan na Sunnah. Sema na wala usiteteleki.

***Jabbar hushuka... -*** Allaah (Jalla wa ´Alaa) hushuka katika mbingu ya dunia kila usiku.

***... katika kila usiku -*** Kwa kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndiye kasema hivo. Yeye ndiye mjuzi zaidi kumtambua Mola Wake na yanayolingana Naye. Sema aliyosema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na mthibitishie Allaah kushuka.

Kushuka ni katika sifa Zake za kimatendo ambazo anazifanya (Jalla wa ´Alaa) kwa utashi na matakwa Yake pale anapotaka. Kushuka huku kumepokelewa mapokezi tele ya Hadiyth kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wamezipokea kundi la Maswahabah na ziko katika vitabu "as-Swahiyh". Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) ameandika kitabu cha kipekee akifafanua Hadiyth ya kushuka. Kitabu hicho kimechapishwa kipekee na kadhalika kimechapishwa pamoja na "Majmuu´-ul-Fataawaa". Anwani yake ni "Sharh Hadiyth-in-Nuzuul".

Ni wajibu kuthibitisha kushuka kama alivyothibitisha Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hushuka kila usiku pale kunapobaki theluthi ya mwisho ya usiku. Haya yanawaponda wakanushaji. Kwa kuwa yamepokelewa kwa mapokezi mengi. Wamezowea kusema kuwa Hadiyth

imepokelewa kwa njia moja (*Aahaad*) na kwamba haifidishi elimu. Lakini hapa hawana hila kwa kuwa zimepokelewa Hadiyth tele kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Kushuka huku ni kama sifa Zake zingine (Jalla wa ´Alaa). Sio kama kushuka kwa viumbe. Ni kushuka kwa Jabbar (Jalla wa ´Alaa) ambako kunalingana na utukufu Wake. Hatujui namna yake. Sisi tunathibitisha kama ilivyokuja na hali ya kuwa tunaamini hilo. Hatuipindishi maana, hatuikanushi na wala hatuifananishi na kushuka kwa viumbe. Ni kushuka kunakolingana na ukubwa wa Allaah (Jalla wa ´Alaa).

## 36. Radd kwa wanaokanusha Allaah kushuka kwenye mbingu ya dunia

Kwa vile Hadiyth hii imepokelewa kwa mapokezi mengi (*Mutawaatir*) na wakaona hawana namna ya kuikwepa, sasa wakataka kujibebetua ili wajikwamue nayo. Wakasema:

"Hushuka"

maana yake ni amri Yake ndio hushuka. Tunawaraddi kwa kuwaambia: katika Hadiyth imekuja ya kwamba Husema: **"Ni nani anayeniomba msamaha nimsamehe? Ni nani anayeniomba nimpe? Kuna mwenye kutubia nimsamehe? Kuna mwenye kuniomba msamaha nimghufurie? Kuna kwenye kuniomba nimpe?"**[21]

Je, amri inaweza kusema:

**"Ni nani anayeniomba nimpe? Ni nani anayeniomba msamaha nimsamehe?"**

Hili ni batili. Mwenye kusema haya ni Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).

Wakasema:

**"Hushuka Mola wetu."**

maana yake ni Malaika miongoni mwa Malaika ndiye mwenye kushuka. Tunawaraddi kwa kuwaambia: Je, Malaika ndiye mwenye kusema:

**"Ni nani mwenye kuniomba msamaha? Ni nani mwenye kuniomba? Ni nani mwenye kutubia nimsamehe?"**

Hivi kweli Malaika anaweza kusema haya au yanasemwa na Mola (Subhaanahu wa Ta´ala)? Bila shaka ni Mola (Jalla wa ´Alaa).

[21] al-Bukhaariy (1145) na Muslim (168) na (758)

Kwa hivyo makusudio sio kwamba amri wala Malaika ndiye mwenye kushuka. Kwa kuwa si amri wala Malaika vyote viwili hakuna mwenye kuweza kutamka maneno haya yaliyokuja katika Hadiyth.

## 37. Radd kwa baadhi ya shubuha zinazotumika juu ya kushuka kwa Allaah

Wakatazama namna ambavyo jua linaizunguka ardhi, wakasema Atashuka vipi ilihali usiku unatofautiana kwa kutofautiana kwa miji? Jua ndio lenye kuizuguka ardhi. Hivyo sehemu ya ulimwengu kunakuwa ni mchana na sehemu nyingine inakuwa ni usiku. Hivi kwetu inakuwa ni mchana na kwa wengine inakuwa ni usiku na kinyume chake. Tunawaraddi kwa kuwaambia:

Sisi hatuingilii hili kwa kuwa hili ni jambo la Allaah. Yule ambaye ameweka usiku na mchana na akafanya kuwa vinapishana ndiye huyo huyo Aliyetukhabarisha kuwa hushuka (Subhaanahu wa Ta´ala). Sisi tunathibitisha kushuka na wala hatuingilii namna. Hatuulizi ni vipi anashuka theluthi ya usiku ilihali usiku unatofautiana kwa kutofautiana kwa miji. Mtu anaweza kuuliza hivi ikiwa inahusiana na kushuka kwa viumbe. Kuhusu kushuka kwa Muumba Yeye hushuka namna anavyotaka (Subhaanahu wa Ta´ala).

Wakasema tena kwamba kuteremka kunapelekea kufanya harakati na kutoka sehemu kwenda nyingine. Wakauliza kama Allaah hutoka kwenye ´Arshi Yake na kuteremka kwenye mbingu ya dunia na kama anafanya harakati. Tunawaraddi kwa kuwaambia: huku ni kutafiti namna. Sisi tunasema kuwa Anashuka namna anavyotaka. Hatujui namna. Allaah hushuka namna anavyotaka. Hakika Yeye juu ya kila jambo ni muweza. Yeye ndiye ambaye ameumba mbingu na ardhi. Hivyo hatuingii ndani ya hili.

Sisi tunathibitisha kushuka, kama ilivyokuja, pindi kunapobaki theluthi ya mwisho ya usiku. Tunathibitisha hilo na wakati huo huo tunaliamini. Hatujali ubabaishaji wa watu hawa ambao wanataka kumkosoa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Ni kama kwamba wanamwambia: "Ee Mola wetu! Hakika kushuka hakulingani na Wewe kutokana an sababu hii na ile." Wanamkosoa Allaah (Jalla wa ´Alaa) na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ni kama kwamba wao ni wajuzi zaidi kuliko Allaah na ni wajuzi zaidi kumtambua Allaah (Jalla wa ´Alaa) kuliko Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa

sallam). Huku ni kuwa na utovu wa adabu kwa Allaah (Jalla wa ´Alaa). Allaah anathibitisha kuwa anashuka na wao wanakanusha na wanasema ikiwa anafanya hivo, basi itamlazimu hili na lile. Haya ni malazimisho batili.

## 38. Maana tatu ya Jabbar

***Jabbar* -** Bi maana Allaah (Jalla wa ´Alaa). Moja katika majina Yake ni Jabbaar. Jabbar lina maana nyingi:

Ya kwanza: Ambaye anawapa moyo waja Wake waliovunjika moyo.

Ya pili: Ambaye hukumu Zake za kimakadirio zinapita kwa waja Wake bila ya wao kuzizuia. Hukumu Zake (Jalla wa ´Alaa) za kimakadirio hazirudishwi.

Ya tatu: Maana yake nyingine ya kilugha ni Aliye juu. Allaah (Jalla wa ´Alaa) yuko juu ya viumbe Wake:

وَهُوَ الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ ۚ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْخَبِيرُ

**"Naye ni mshindi Aliye juu ya waja Wake, Naye ni Mwenye hikmah, Mjuzi." (06:18)**

وَهُوَ الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ ۖ وَيُرْسِلُ عَلَيْكُمْ حَفَظَةً

**"Naye ni mshindi Aliye juu ya waja Wake na anakutumieni walinzi." (06:61)**

***hushuka katika kila usiku* -** Kama ilivyokuja katika Hadiyth.

***bila ya namna...* -** Bi maana hatujui namna ya kushuka huko. Hakuna anayejua hili isipokuwa Allaah peke yake. Haimlazimu haya malazimisho yaliyowekwa na wakanushaji, wafananishaji na washabihishaji kwa sababu sisi hatutafiti namna hii. Hakika Allaah juu ya kila kitu ni muweza. Viumbe hawawezi kumzunguka Yeye wote kwa kumtambua. Hakuna anayejua namna ilivyo dhati Yake wala namna yalivyo majina na sifa Zake isipokuwa Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala).

Kadhalika Jabbar hushuka jioni ya ´Arafah na hujifakhari kwa waja Wake Malaika na kusema:

**"Watazameni waja Wangu wamenijia wakiwa timtimu wamejaa vumbi kutoka katika kila kona ya dunia. Ninakushuhudisheni kwamba hakika Mimi nimewasamehe."**[22]

Hii ni aina nyingine ya kushuka. Mola wetu hushuka jioni ya ´Arafah katika mbingu ya dunia kama ambavyo Anashuka kila usiku katika nyusiku za mwaka pindi kunapobaki theluthi ya mwisho ya usiku. Haya ni kutokana na upole na huruma Wake (Subhaanahu wa Ta´ala) kwa waja Wake.

***... ametukuka... -*** Bi maana ametukuka uwezo Wake kuwekewa namna au kwa sisi kutambua namna yalivyo majina na sifa Zake. Miongoni mwazo ni kushuka. Sisi tunathibitisha kushuka na wala hatutafiti namna. Ni kama sifa zingine zote: kushuka kunajulikana. Kuhusu namna haijulikani. Hivyo ndivyo alivyosema Maalik (Rahimahu Allaah) juu ya kulingana ya kwamba:

"Kulingana (*Istiwaa´*) inajulikana. Namna haijulikani."[23]

***... Mmoja... -*** Mmoja ni katika majina ya Allaah (Jalla wa ´Alaa). Hakika Yeye (Subhaanah) ni Mmoja Peke ambaye hana mshirika katika dhati, majina na sifa Zake, matendo na ´ibaadah Zake.

***... mwenye kuhimidiwa... -*** Mwenye kusifiwa kwa sifa za kusifiwa kamilifu.

[22] Ahmad (02/305), Ibn Hibbaan (3852) na wengineo

[23] Tazama "ar-Radd ´alaa al-Jahmiyyah", uk. 33 ya ad-Daarimiy na "I´tiqaad Ahl-is-Sunnah" (03/527) (928) ya al-Laalakaa´iy

## 39. Allaah hushuka mbingu ya chini ya dunia kila usiku

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

12- *Hutunuku fadhila Zake katika tabaka ya dunia*

*milango ya mbingu hufunguliwa*

13- *Husema "Tanabahini! Kuna mwombaji msamaha amuombae mghufiriaji*

*na mwenye kuomba kheri na riziki apewe"*

**MAELEZO**

***... katika tabaka ya dunia -*** Hushuka katika tabaka ya chini kabisa ya dunia. Kwa sababu mbingu ina tabaka saba. Amesema (Ta´ala):

أَلَمْ تَرَوْا كَيْفَ خَلَقَ اللَّهُ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ طِبَاقًا

**"Je, hamuoni jinsi Allaah alivyoziumba mbingu saba kwa matabaka?" (71:15)**

Baadhi ya tabaka ziko juu ya zingine. Hushuka (Jalla wa ´Alaa) namna anavyotaka katika mbingu ya dunia inayofuatiwa na ardhi.

***Hutunuku fadhila Zake... -*** Husema (Subhaanah):

**"Kuna anayeniomba nimpe?"**

Hizi ni fadhila kutoka kwa Allaah. Husema:

**"Kuna anayeomba msamaha nimsamehe? Kuna mwenye kutubia nimsamehe?"**

Yote haya ni kutokana na fadhila Zake (Subhaanahu wa Ta´ala). Anawatunuku waja Wake ukarimu Wake.

## 40. Muislamu isikupite fursa hii kubwa

Kwa ajili hii imependekezwa kwa muislamu aamke mwishoni mwa usiku pale kunapobaki theluthi ya mwisho ya usiku. Anatakiwa awe macho huku akiswali, akiomba du´aa na akiomba msamaha. Hakika huu ni wakati ambapo du´aa inakubaliwa. Asilale katika wakati huu akajinyima nafsi yake. Hivi ndivyo wanavyofanya wengi walionyima ambapo wanakesha usiku mzima na inapofika mwishoni mwa usiku wanalala na kupitwa hata na swalah ya Fajr ambayo ni faradhi. Huku ni kunyimwa. Inatakikana kwa muislamu alale mapema na ajizoweze nafsi yake. Kila kitu ni kwa mazoezi. Lengo ni ili aweze kuamka mwishoni mwa usiku. Akijizoweza nafsi yake kufanya hivi atazowea. Lakini iwapo atajizoweza uzembe na kulala, basi itamkuwia uzito kuamka hata wakati wa swalah ya Fajr.

Haitakikani kwa muislamu akapitwa na fursa kama hii. Huu ni wito wa kiungu. Anatakiwa awepo. Allaah (Jalla wa ´Alaa) anasema kuhusu wanaomcha:

كَانُوا قَلِيلًا مِّنَ اللَّيْلِ مَا يَهْجَعُونَ وَبِالْأَسْحَارِ هُمْ يَسْتَغْفِرُونَ

**"Walikuwa wakilala kidogo tu usiku na kabla ya alfajiri wakiomba maghfirah." (51:17-18)**

وَالْمُسْتَغْفِرِينَ بِالْأَسْحَارِ

**"Na waombao maghfirah kabla ya alfajiri." (03:17)**

Kuomba msamaha kabla ya alfajiri ni kitendo kilicho na sifa ya kipekee kuliko nyakati zingine.

***milango ya mbingu hufunguliwa -*** Bi maana hufunguliwa milango ya kujibiwa. Inatakikana kwa muislamu awepo wakati kama huu na aombe msamaha, atubie na kuomba. Kwani amefunguliwa milango ya kujibiwa. Hii ni fursa kubwa. Amesema (Rahimahu Allaah):

*Husema "Tanabahini! Kuna mwombaji msamaha amuombae mghufiriaji*

Bi maana zindukeni kwa kitachosemwa.

***... aombae msamaha* -** Imechukuliwa katika maneno Yake:

**"Je, kuna anayeomba msamaha nimsamehe?"**

***na mwenye kuomba kheri...* -** Bi maana kuna anayemuomba Allaah (´Azza wa Jall) anachokitaka katika kheri sawa katika riziki na haja yoyote ile. Haja za watu zinatofautiana. Amuombe Allaah haja yoyote ile ilio na kheri kwake. Allaah hutoa zaidi katika wakati huu kuliko wakati mwingine wowote ule.

Hakika Allaah (Jalla wa ´Alaa) yu karibu na ni Mwenye kujibu. Anaikubali tawbah na anasamehe madhambi katika nyakati zote. Lakini zipo nyakati ambazo ni maalum ambapo kuna matarajio zaidi ya kujibiwa. Moja wapo ni wakati huu. Mfano mwingine ni saa iliopo siku ya Ijumaa. Kuna nyakati ambazo kujibiwa kunakuwa karibu zaidi. Kwa mfano katika Sujuud. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Mja anakuwa karibu zaidi na Mola wake katika hali ya kusujudu."[24]**

Kadhalika katika hali ya safari:

**"... anarefusha safari yake nywele timtim. Ananyoosha mikono yake... "[25]**

Vilevile katika hali ya kudhikika:

أَمَّن يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ

**"Ni nani anayemuitika aliyedhikika anapomwomba." (27:62)**

Kuna nyakati na hali ambazo kuna matarajio makubwa ya kujibiwa kuliko nyakati na hali zingine. Vinginevyo Allaah (Jalla wa ´Alaa) anasikia,

[24] Muslim (215) na (482)

[25] Muslim (65) na (1015)

anasamehe, anatunuku, anasikia du´aa na anajibu katika kila wakati usiku na mchana.

***... na riziki apewe -*** Ni vipi mtu atajikosesha haya na akalala? Atafaidika nini na kulala? Ni vipi ataghafilika na kuendekeza upuuzi wa TV na Intaneti. Utamuona mtu ametulizana hali ya kuyakodoa macho hatikisiki na sanamu hili chafu na wala hachoshwi kabisa na anampuuza Mola Wake (Subhaanahu wa Ta´ala) anajikosesha kheri hii nyingi ambayo yeye ni mwenye kuihitaji sana. Hakuna mwenye kuweza kujitosheleza na Allaah (Jalla wa ´Alaa) kwa muda wa kukapua macho. Ni vipi mtu anaweza kupuuza haya na asiyatilie umuhimu?

Pengine vilevile akafuata madhehebu ya Jahmiyyah, Mu´tazilah na Ashaa´irah akakadhibisha, akapinga na kupuuza kushuka huku. Huyu anayepinga ni mbaya zaidi kuliko ambaye hapuuzi na wala hapingi. Lau kama kuna wakati fulani ambapo kunagawiwa pesa au kumefunguliwa mchango katika shirika na huku wanatarajia katika wakati huo kupata faida, mnaonaje watu watafanya nini? Hawatosongamana? Bali tumefikiwa na khabari kwamba watu hupigana kwa sababu ya msongamano kwa ajili ya kutafuta dunia itayoisha ambayo huenda mtu akaipata na huenda asiipate. Na kama mtu ataipata huenda ikawa ni shari na balaa kwa mwenye nayo. Huenda vilevile mchango huu ukawa ni haramu na ndani yake mna ribaa na kamari. Pamoja na haya yote watashindana na kupigana kwa ajili yake. Wataenda mapema kabla ya mambo kuanza ili kila mmoja awe karibu na nafasi hiyo na asiwe mbali. Ikiwa mambo ni namna hii katika jambo la kidunia ni vipi mtu atapuuza jambo la Aakhirah ambalo halihitaji msongamano na limejaa kheri tupu na hakuna msongamano, mashindano, fujo na vurugu? Ni vipi mtu atapuuza haya na kwenda katika jambo ambalo hajui kuwa ni kheri au shari? Bila shaka katika zama hizi liko karibu zaidi na shari. Wakati huu watu wengi wamekuwa hawaangalii halali na haramu. Hakika shari na fitina ya mali leo ni kubwa. Pamoja na hivyo watu wanapigana kwayo. Ni vipi basi watu wanaghafilika na fursa kama hii kubwa pamoja na Allaah (´Azza wa Jall) - ambaye ni mkarimu sana na mwenye huruma sana na ambaye hakuna yeyote awezae kujitosheleza Naye kwa muda wa kukapua macho - ambayo

amewafungulia? Allaah hahitajii kwao wakeshe usiku mzima wakifanya ´ibaadah. Bali Yeye (Subhaanah) hushuka sehemu ya mwisho ya usiku kabla ya Fajr. Unaweza kuamka muda kidogo tu kabla ya Fajr ili uweze kushuhudia wakati huu mkubwa. Iwapo utaamka mapema ndio bora zaidi. Isikupite fursa kama hii kubwa na ukaghafilika nayo. Huenda huu ukawa ndio uhai wako wa mwisho na usiudiriki huko mbeleni. Maadamu uko katika wakati ambapo uko na uwezo na uko na faragha si mwenye kushughulishwa, usiipoteze fursa hii kubwa.

***Kuna mwombaji msamaha... -*** Ni kuomba maghfirah.

***... amuombae mghufiriaji -*** Naye ni Allaah (Jalla wa ´Alaa). Miongoni mwa majina Yake ni msamehevu (*Ghaffaar/Ghafuur/Dhul-Maghfirah*). Haya ni majina ya Allaah (Jalla wa ´Alaa). Ni yule ambaye anasitiri madhambi. Maana ya jina hili ni kusitiri. Anayasitiri madhambi kwa kuyasamehe na kutoyachukulia.

***na mwenye kuomba kheri -*** Ni kuomba neema. Imechukuliwa katika maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akielezea juu ya Mola wake aliposema:

**"Je, kuna mwenye kuomba nimpe?"**

## 41. Jahmiyyah, Mu´tazilah na vifaranga vyao wameangamia

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

14- *Wameyapokea hayo watu zisizorudishwa Hadiyth zao*

*wameangamia watu waliowakadhibisha na wakebehewe*

**MAELEZO**

***Wameyapokea hayo watu... -*** Wamepokea Hadiyth kuhusu Kushuka kundi la Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

***... zisizorudishwa Hadiyth zao -*** Kwa sababu ni Hadiyth zilizopokewa kwa mapokezi mengi kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Jahmiyyah na wakanushaji hawana njia yoyote inapokuja katika mlolongo wa wapokezi.

***wameangamia watu... -*** Kwa kuwa wamekadhibisha Hadiyth hizi na wakapinga kuwa Allaah anashuka na wakapindisha maana ya Hadiyth za Mtume kinyume na alivyokusudia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wamemzulia na kumsemea Allaah uongo.

***... waliowakadhibisha na wakebehewe -*** Nao ni Jahmiyyah na wale wenye kufuata mfumo wao. Asli ya balaa ni Jahmiyyah na Mu´tazilah. Wote waliokuja baada yao wakafuata mfumo wao. Wao ndio ambao wamefungua mlango wa upotevu. Wapotevu wote waliokuja baada yao ni wenye kuwafuata. Wanaguswa na maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Mwenye kuita katika upotevu atakuwa na madhambi mfano wa madhambi ya ambaye atamfuata, hakutopungua kitu katika madhambi yao, na**

**mwenye kulingania katika uongofu atakuwa na ujira mfano wa ujira wa ambaye atamfuata, hakutopungua kitu katika ujira wao."[26]**

[26] al-Bukhaariy (7321) na Muslim (16) na (2674)

## 42. Kuwa mlinganizi wa haki - usiwe mlinganizi wa upotevu

Muislamu atahadhari asiwe katika walinganizi wa upotevu. Si kwamba atapata madhambi yeye peke yake. Bali atabeba madhambi pia ya wale watakaomfuata. Kwa kuwa yeye ndiye kawaghuri, kawadanganya na akawafungulia mlango wa shari. Hivyo akawa ni kiigizo katika shari. Amesema (Ta´ala):

لِيَحْمِلُوا أَوْزَارَهُمْ كَامِلَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۙ وَمِنْ أَوْزَارِ الَّذِينَ يُضِلُّونَهُم بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ أَلَا سَاءَ مَا يَزِرُونَ

**"Ili wabebe madhambi yao kamili siku ya Qiyaamah na madhambi ya wale waliowapoteza bila ya elimu. Tanabahi! Uovu ulioje wanayoyabeba!" (16:25)**

Kuna khatari kubwa juu ya hili. Hili linazidi kuwa ni msisitizo kwa muislamu ya kwamba anatakiwa awe ni kiigizo katika kheri na alinganie katika kheri. Ajiepushe asiwe ni mlinganizi katika shari, kufuata matamanio au mikhalafa. Haijalishi kitu ni nani ambaye yuko katika hayo. Hakika haki ina haki zaidi ya kufuatwa.

## 43. Fadhila za Maswahabah na Radd kwa wale wenye kuwaponda

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

15- *Sema "Watu bora baada ya Muhammad*

*ni mawaziri wake, kisha ´Uthmaan [ndio maoni] yenye nguvu*

16- *Wanne wao ni kiumbe bora anayekuja baada yao*

*´Aliy kiongozi mwema kwa kheri"*

**MAELEZO**

Huu ni utafiti juu ya haki ya Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum). Nao si wengine ni Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambao ndio karne bora. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Wabora wenu ni karne yangu, kisha wataofuatia, kisha wataofuatia."**[27]

Mpokezi anasema:

"Sikumbuki baada ya karne yangu alitaja karne mbili au tatu."

Bi maana inakuwa karne nne. Zinaitwa kuwa ni karne bora kutokana na Hadiyth hii.

Bora katika karne hizi ni ya Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum). Allaah amewasifu katika Kitabu Chake (Radhiya Allaahu ´anhum). Amesema (Subhaanahu wa Ta´ala):

[27] al-Bukhaariy (6690), (6428), (365) na (2651) na Muslim (2525) na (214)

وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُم بِإِحْسَانٍ رَّضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتَهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

**"Na wale waliotangulia awali katika *Muhaajiruun* na *Answaar* na wale waliowafuata kwa wema, Allaah ameridhika nao nao wameridhika Naye na amewaandalia mabustani ipitayo chini yake mito - ni wenye kudumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa." (09:100)**

لِلْفُقَرَاءِ الْمُهَاجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِن دِيَارِهِمْ وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا وَيَنصُرُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۚ أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ

**"Mafuqara *Muhaajiruun* ambao wametolewa kutoka majumbani mwao na [zikataifishwa] mali zao wanatafuta fadhila na radhi kutoka kwa Allaah na wanamnusuru Allaah na Mtume Wake - hao ndio wakweli." (59:08)**

Allaah (Jalla wa ´Alaa) amewasifu na kuwatapa ya kwamba:

أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ

**"Hao ndio wakweli."**

Amefungamanisha ukweli kwao kwa vile waliuhakikisha. Hii ni dalili yenye kuonesha fadhila na nafasi walizo nazo kwa Allaah (Jalla wa ´Alaa).

Halafu anakuja zandiki na mkanamungu mmoja ambaye anadai Uislamu na kuwahujumu Maswahabah na kuwasema vibaya. Allaah (Jalla wa ´Alaa) anasema:

أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ

**"Hao ndio wakweli."**

Jitu hili linamkadhibisha Allaah (´Azza wa Jall).

Amesema (Jalla wa ´Alaa) kuhusu *Answaar:*

وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيمَانَ مِن قَبْلِهِمْ

**"Na wale waliokuwa na makazi na wakawa na imani kabla yao... "**

Bi maana mji wa kuhajiri. Nao ni *Answaar* al-Madiynah.

يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِّمَّا أُوتُوا وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ ۚ وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

**"... wanawapenda wale waliohajiri kwao na wala hawapati kuhisi uzito wowote vifuani mwao kwa yale waliyopewa [*Muhaajiruun*] na wanawapendelea kuliko nafsi zao japokuwa wao wenyewe wako na njaa. Na yeyote anayeepushwa na ubakhili na tamaa ya uchu wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufaulu." (59:09)**

Haya ni matapo na sifa kwa *Answaar* na kutajwa sifa zao nzuri. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amethibitisha juu yao kufaulu. Amesema:

وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

**"Na yeyote anayeepushwa na ubakhili na tamaa ya uchu wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufaulu."**

Ni dalili kwamba Allaah amewaepusha na ubakhili na tamaa ya uchu wa na nafsi zao mpaka wakawa:

وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ

**"... na wanawapendelea kuliko nafsi zao japokuwa wao wenyewe wako na njaa."**

Wanazitanguliza haja za ndugu zao japokuwa wao wenyewe wako na njaa. Pindi ndugu zao walihama kwenda kwao basi wakawafungulia vifua na nyoyo zao. Sivyo tu bali wakawashirikisha katika mali zao na majumba yao - Allaah awawie radhi wote. Halafu akasema kuhusu wale waliokuja baada yao:

وَالَّذِينَ جَاءُوا مِن بَعْدِهِمْ

**"Na wale waliokuja baada yao... "**

Baada ya Maswahabah mpaka siku ya Qiyaamah:

يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِّلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

**"... wanasema: “Mola wetu! Tusamehe sisi na ndugu zetu ambao wametutangulia kwa imani na wala Usijaalie katika nyoyo zetu mafundo ya chuki kwa wale walioamini. Mola wetu! Hakika Wewe ni Mwenye huruma, Mwenye kurehemu." (59:10)**

Hapa kumebainisha kwamba lililo la wajibu kwa Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) ni kuwaombea du´aa, kuwaombea msamaha, kutambua kutangulia kwao katika imani na kumuomba Allaah azitakase nyoyo zetu kutokamana na kuwa na chuki, vifundo na kuwachukia. Hapa kuna dalili ya kusifiwa kwa Maswahabah na kubainisha yaliyo ya wajibu kwa wale waliokuja baada yao mpaka siku ya Qiyaamah. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) anasema:

**"Msiwatukane Maswahabah zangu. Ninaapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mkononi Mwake! Lau mmoja wenu atatoa dhahabu mfano wa mlima wa Uhud hatofikia robo ya mmoja wao wala nusu yake."[28]**

Iwapo mmoja wenu atatoa swadaqah ya dhahabu mfano wa mlima wa Uhud kwa nia safi kabisa, akatoa yote, hatofikia mfano wa ujira na thawabu za Swahabah mmoja kwa kutoa robo au nusu ya chakula. Mlima wa dhahabu wa ambaye si Swahabah haufikii robo ya chakula cha mmoja wao. Hilo ni kutokana na fadhila na nafasi yao. Kwa sababu miongoni mwa sababu za ujira kuzidishwa ni ule utukufu ambao mtendaji yuko nao mbele ya Allaah.

[28] al-Bukhaariy (3673) na Muslim (222) na (2541)

## 44. Mpangilio wa fadhila za Maswahabah

Ni jambo lisilokuwa na shaka ya kwamba Muhaajiruun ni bora kuliko Answaar kwa kuwa Allaah ametangulia kuwataja wao. Jengine ni kwa sababu wameziacha mali zao, watoto wao na miji yao na wakahajiri katika njia ya Allaah (´Azza wa Jall). Amesema (Ta´ala):

وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا وَيَنصُرُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ

**"Wanatafuta fadhila na radhi kutoka kwa Allaah na wanamnusuru Allaah na Mtume Wake - hao ndio wakweli." (59:08)**

Kisha wabora katika Muhaajiruun ni wale makhaliyfah wanne; Abu Bakr asw-Swiddiyq, kisha ´Umar al-Faaruuq, halafu ´Uthmaan Dhun-Nurayn, kisha ´Aliy bin Abiy Twaalib (Radhiya Allaahu ´anhum).

Halafu wanafuata wale kumi waliobashiriwa Pepo.

Kisha wanafuata walioshuhudia vita vya Badr.

Kisha wanafuata waliompa kiapo cha usikivu na utiifu Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) chini ya mti:

لَّقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ

**"Hakika Allaah amewawia radhi waumini walipokupa kiapo cha usikivu na utiifu chini ya mti." (48:19)**

Allaah (´Azza wa Jall) ameeleza kuwa amewaridhia. Halafu anajitokeza mtenda dhambi mkubwa mmoja kisha anawasema vibaya Maswahabah. Allaah awakebehi waovu na wapotevu.

Halafu wale waliosilimu kabla ya Ushindi wa Makkah ni bora kuliko wale waliosilimu baada ya Ushindi. Amesema (Ta´ala):

لَا يَسْتَوِي مِنكُم مَّنْ أَنفَقَ مِن قَبْلِ الْفَتْحِ وَقَاتَلَ ۚ أُولَٰئِكَ أَعْظَمُ دَرَجَةً مِّنَ الَّذِينَ أَنفَقُوا مِن بَعْدُ وَقَاتَلُوا ۚ وَكُلًّا وَعَدَ اللَّهُ الْحُسْنَىٰ

**"Hawi sawa miongoni mwenu aliyetoa kabla ya Ushindi [wa Makkah] na akapigana. Hao watapata daraja kuu kabisa kuliko wale waliotoa baada [ya ushindi] na wakapigana - na wote Allaah amewaahidi Pepo." (59:10)**

Wote wawili, waliosilimu kabla ya Ushindi na waliosilimu baada ya Ushindi:

وَكُلًّا وَعَدَ اللَّهُ الْحُسْنَىٰ

**"Wote Allaah amewaahidi Pepo."**

Hakuna yeyote anayewafikia Maswahabah katika fadhila vovyote atavyotenda. Inatosheleza kwao kuwapenda, kufuata mwongozo wao, kuwasifu, asimtukane yeyote katika wao, asipekue kasoro zao na asiingilie yaliyopitika kati yao kwa sababu ya fitina iliyowaingilia. Waliingiliwa na janga pasi na wao kupenda. Asiwepo yeyote atayeingilia suala la Maswahabah isipokuwa kwa kuwasifu, kuwaombea msamaha na huruma, kuiga mwongozo wao na kuwapenda kwa kuwa Allaah na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wanawapenda. Sisi tunampenda yule anayependwa na Allaah na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

## 45. Haya ndio malengo ya wenye kuwatukana Maswahabah

Dini na Sunnah hii imetufikia kutoka wapi? Sio kupitia kwa Maswahabah? Wao ndio wakati na kati baina yetu sisi na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wao ndio walitufikishia dini kwa amana walipoipokea kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kila Hadiyth utakuta "kutoka kwa fulani, kutoka kwa fulani kutoka kwa Swahabah". Wao ndio wakati na kati baina yetu sisi na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika kufikisha dini. Wametuhifadhia Sunnah na Qur-aan na wakavifikisha kwetu.

Jengine ni wepi walioeneza Uislamu kwa kupigana kwao Jihaad na kulingania katika Uislamu mashariki na magharibi? Je, sio Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)? Ni wepi waliopambana na walioritadi baada ya kufa kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)? Je, si wao ndio ambao Allaah aliwafanya kuwa imara juu ya dini hii pindi watu wa shari walipotaka kutumia fursa ya kufa kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wakataka kuitikisa dini, kuwaritadisha watu na kuwaondosha kwayo? Allaah akaifanya dini hii kuwa imara kupitia Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa kumwongoza mbora wao ambaye ni Abu Bakr asw-Swiddiyq (Radhiya Allaahu ´anh).

Hizi ni baadhi ya fadhila na sifa zao tukufu (Radhiya Allaahu ´anhum).

Sababu zilizowafanya waandishi kuyataja masuala haya katika vitabu vya ´Aqiydah ni ili kuyaraddi mapote potevu yenye kufanya uadui juu ya Uislamu. Malengo yao ni kuutukana Uislamu. Hawakuona njia ilio karibu zaidi isipokuwa hii ya kuwatukana Maswahabah. Kwa kuwa wao ndio waliobeba dini hii na wakaifikisha kwa Ummah. Hivyo wakaona wakiwatukana Maswahabah - ambao ndio wakati na kati baina yetu sisi na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika kufikisha dini - basi watakuwa wameutukana Uislamu. Kwa sababu Uislamu utakuwa haukuthibiti kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa

sallam). Kwa kuwa wale walioinukuu hawatumiwi kama hoja. Haya ndio malengo yao.

## 46. Makundi yenye kuwatukana Maswahabah

Mapote matatu ndio yenye uadui kwa Maswahabah:

1- Raafidhwah.

2- Khawaarij.

3- Naaswibah.

Lakini hata hivyo wabaya zaidi ni Raafidhwah.

Kilichowapelekea Khawaarij kufanya hivi ni kuwa na ususuwavu na kupetuka mpaka katika dini. Hawa malengo yao haikuwa kuutukana Uislamu. Walifanya hivi kwa sababu ya kupetuka mpaka na ususuwavu katika dini. Lengo lao haikuwa kuitukana dini. Bali haya - kwa madai yao - ni kwa sababu ya kuipenda kwao dini na kuipupia.

Kuhusu Nawaaswib kilichowapelekea kuwatukana baadhi ya Maswahabah ni kwa sababu ya jambo la kisiasa. Wanachotaka kwa kufanya hivo ni kutukana uongozi wa ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh). Sababu ilikuwa jambo la kisiasa tu na kwamba hastahiki uongozi. Malengo yao pia haikuwa kuitukana dini.

Ama kuhusu Raafidhwah - Allaah awakebehi - malengo yao ilikuwa kuitukana dini. Endapo watawasema vibaya na kuwatukana Maswahabah, basi kutakuwa hakukubaki baina yetu sisi na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ukati na kati wowote ilihali dini imetufikia kupitia njia ya Maswahabah ambao - kwa mtazamo wa Raafidhwah - maneno yao hayatumiwi kama hoja. Kwa hivyo huku ni kuitukana dini. Haya ndio malengo yao.

## 47. Tofauti iliyopo kuhusu ni nani bora kati ya ´Uthmaan na ´Aliy

Tumetangulia kuzungumza juu ya fadhila za Maswahabah na kwamba wanatofautiana katika fadhila baina yao. Hata hivyo wanashirikiana katika fadhila za uswahabah. Hakuna yeyote anayeshirikiana nao katika fadhila hii. Hakuna yeyote anayewafikia katika hili. Kuhusu wao kati yao wanashindana. Baadhi ni wabora zaidi kuliko wengine. Tukisema kuwa baadhi ni wabora zaidi kuliko wengine haina maana kwamba tuwatukane wale wenye kushindwa ubora. Haijuzu kumtukana yule anayeshindwa ubora ilihali ni Swahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Kadhalika tumetangulia kubainisha kuwa Maswahabah bora ni wale makhaliyfah wane. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Jilazimieni na Sunnah zangu na Sunnah za makhaliyfah wangofu baada yangu. Shikamaneni nazo barabara na ziumeni kwa magego yenu."**

Ambaye amewaita kuwa ni makhaliyfah waongofu ni Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na pia akaamrisha kushikamana na Sunnah zao kwa kuwa wanapita juu ya Sunnah zake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wanazithibitisha na kuzitawanya kutokana na ile elimu, nguvu na uongozi aliyowapa Allaah.

Mbora zaidi katika makhaliyfah wanne ni Abu Bakr na kisha ´Umar. Haya ni kwa maafikiano ya waislamu. Walitafautiana kwa ´Aliy na ´Uthmaan ni nani ambaye ni bora zaidi. Kuna kundi lilimfadhilisha ´Uthmaan. Kundi lingine likamfadhilisha ´Aliy. Kundi lingine likasimama. Yote haya yanahusiana na ubora/fadhila. Kuhusu uongozi Ummah mzima umeafikiana juu ya kwamba uongozi baada ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni wa Abu Bakr, kisha wa ´Umar, halafu wa ´Uthmaan na kisha wa ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhum). Huu ndio mpangilio wa uongozi kwa maafikiano. Shaykh-ul-Islaam (Rahimahu Allaah) amesema katika "al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah":

"Mwenye kutukana uongozi wa mmoja katika hawa ni mpotevu kuliko punda wa kufugwa."[29]

Kuna tofauti kati ya masuala ya ubora na masuala ya uongozi. Kuhusu masuala ya ubora waislamu wameafikiana juu ya kwamba mbora ni Abu Bakr na kisha ´Umar. Wakatafautiana ni nani bora kati ya ´Aliy na ´Uthmaan. Maoni sahihi ni kwamba ´Uthmaan ndiye bora zaidi. Kwa mtazamo wa kuwepo tofauti inatajwa. Vinginevyo ni jambo lisilokuwa na shaka ya kwamba ´Uthmaan (Radhiya Allaahu ´anh) ndiye bora zaidi. Dalili ni kuwa watu wa mashauriano walimtanguliza ´Uthmaan juu ya ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhumaa) katika uongozi.

Masuala ya ubora kati ya ´Uthmaan na ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhumaa) ni kitu chepesi. Kutukana uongozi ndio upotevu. Kwa sababu Raafidhwah wanasema kuwa khaliyfah baada ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni ´Aliy na ndiye muusiwa. Wanasema kuwa Maswahabah walimdhulumu na wakampokonya uongozi. Isitoshe wanamlaani Abu Bakr na ´Umar na wanawaita kuwa ni masanamu mawili ya ki-Quraysh. Hili bila ya shaka yoyote ni upotevu, ukafiri na ni kwenda kinyume na maafikiano. Khaliyfah baada ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni Abu Bakr, halafu ´Umar, halafu ´Uthmaan na halafu ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anhum).

[29] Tazama "al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah", uk. 193 Sharh ya mwandishi (Hafidhwahu Allaah).

## 48. Baadhi ya fadhila za Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anh)

Abu Bakr asw-Swiddiyq (Radhiya Allaahu ´anh) ndiye mbora katika makhaliyfah. Allaah amemsifu pale aliposema:

وَلَا يَأْتَلِ أُولُو الْفَضْلِ مِنكُمْ وَالسَّعَةِ أَن يُؤْتُوا أُولِي الْقُرْبَىٰ

**"Wala wasiape wale wenye fadhila miongoni mwenu na nafasi kuwa hawatowapa [swadaqah] jamaa wa karibu." (24:22)**

Aayah hii imeshuka juu ya Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anh) pindi alipoapa kuwa hatompa Mistwha bin Uthaathah kitu katika mali. Mtu huyu alikuwa ni ndugu ambaye alikuwa akimhudumikia. Pindi alipodanganyika na wale waliozungumza machafu na akawasadikisha na yeye akawa ameongea, ndipo Abu Bakr akamghadhibikia na akaapa kuwa hatompa. Allaah akashusha Aayah ifuatayo:

وَلَا يَأْتَلِ

**"Wala wasiape... "**

أُولُو الْفَضْلِ

**"... wale wenye fadhila."**

Akamsifu Abu Bakr kuwa ni katika wenye fadhila.

Katika Aayah nyingine imekuja:

إِلَّا تَنصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ

**"Msipomnusuru basi Allaah Amekwishamnusuru, pale walipomtoa wale waliokufuru akiwa wa pili katika wawili."**

Wawili hawa ni watu gani? Ni Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Abu Bakr. Haya ni kwa maafikiano.

إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا

**"Wawili hao walipokuwa katika pango, alipomwambia swahiba yake: "Usihuzunike - hakika Allaah Yu Pamoja nasi." (09:40)**

Amemthibitishia usuhuba pamoja na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Abu Bakr ndiye Swahabah bora. Kadhalika ndivyo zinavyofahamisha Hadiyth Swahiyh zinazopatikana katika al-Bukhaariy na kwenginepo. Mbora katika Ummah huu ni Abu Bakr asw-Swiddiyq. Hilo ni kwa sababu ya kutangulia kwake katika Uislamu, kumnusuru kwake Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kulazimiana naye.

Pindi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipofariki Ummah mzima uliafikiana juu ya kumchagua Abu Bakr. Pindi waliporitadi walioritadi katika mabedui ambaye aliwasimamia kidete na akapambana nao ni Abu Bakr mpaka Allaah akaithibitisha dini hii na akawaangusha walioritadi kupitia yeye. Fadhila zake ni nyingi (Radhiya Allaahu ´anh). Anaitwa "as-Swiddiyq" (*mkweli sana*). Daraja ya wakweli inakuja baada ya daraja ya Mitume. Amesema (Ta´ala):

وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَٰئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِم مِّنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ ۚ وَحَسُنَ أُولَٰئِكَ رَفِيقًا

**"Atakayemtii Allaah na Mtume, basi hao watakuwa pamoja na wale Allaah aliowaneemesha miongoni mwa Manabii, na wakweli, na mashahidi na waja wema - na uzuri ulioje hao kuwa ni rafiki!" (04:69)**

*asw-Swiddiyq* ni ambaye anasema ukweli sana. Ni mtu amepindukia katika ukweli. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Hatoacha mtu kuendelea na ukweli na kuupa kipaumbele mpaka aandikwe mbele ya Allaah kuwa ni "mkweli"."[30]**

[30] al-Bukhaariy (6094) na Muslim (102) na (2606)

## 49. Baadhi ya fadhila za ´Umar (Radhiya Allaahu ´anh)

Baada yake anafuatia ´Umar al-Faaruuq. Ameitwa al-Faaruuq (*mfarikishi*) kwa sababu Allaah amefarikisha kupitia yeye baina ya haki na batili. Aliposilimu Uislamu ulitukuka kwa kuingia kwake katika Uislamu. Kabla ya Hamzah na ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhumaa) waislamu walikuwa wanyonge na wakijificha katika pango la Arqam. Pindi aliposilimu Hamzah na ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhumaa) wakatoka nao kuelekea katika Masjid-ul-Haraam. Hapakuwepo yeyote anayewajongelea ilihali wako pamoja na Hamzah na ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhumaa). Hapo ndipo Allaah aliutukuza Uislamu kupitia wawili hao. Ibn Mas´uud (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:

**"Hatukuacha kuwa na nguvu tangu aliposilimu ´Umar."[31]**

Allaah akaupa Uislamu nguvu kupitia yeye. Ndio maana akaitwa al-Faaruuq.

Yeye ndiye khaliyfah wa pili na kadhalika ndiye Swahabah bora baada ya Abu Bakr asw-Swiddiyq kama ilivyo katika al-Bukhaariy na kwenginepo[32]. Wawili hao ndio mawaziri wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Bi maana wenye kumshauri Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Waziri ni mtu anayemsapoti na kumsaidia mtawala. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

وَجَعَلْنَا مَعَهُ أَخَاهُ هَارُونَ وَزِيرًا

**"... na Tukamjaalia pamoja naye - yaani Muusa - kaka yake Haaruun kuwa waziri." (25:35)**

Kwa sababu Muusa alimuomba Mola Wake na kusema:

وَاجْعَل لِّي وَزِيرًا مِّنْ أَهْلِي هَارُونَ أَخِي اشْدُدْ بِهِ أَزْرِي وَأَشْرِكْهُ فِي أَمْرِي

[31] al-Bukhaariy (3863) na (3684), "al-Bidaayah wan-Nihaayah" (03/79)

[32] al-Bukhaariy (3662) na Muslim (08) na (2384).

**"Nifanyie waziri katika ahli zangu Haaruun ndugu yangu. Nitie nguvu kwaye, na umshirikishe katika jambo langu." (20:29-32)**

Hii ndio kazi ya waziri. Ni ambaye anashiriki katika maoni, anamsaidia mtawala na kumshauri na kumnasihi.

Kwa hiyo Abu Bakr na ´Umar ndio mawaziri wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kama ambavyo Haaruun ni waziri wa Muusa (´alayhis-Salaam).

## 50. Baadhi ya fadhila za ´Uthmaan (Radhiya Allaahu ´anh)

Amesema mwandishi:

15- *Sema "Watu bora baada ya Muhammad*

*ni mawaziri wake, kisha ´Uthmaan [ndio maoni] yenye nguvu*

**MAELEZO**

Watatu inapokuja katika ubora ni ´Uthmaan (Radhiya Allaahu ´anh). Yeye ni miongoni mwa wa awali waliotangulia katika Uislamu. Alihajiri mara mbili; alihajiri kwenda Habeshi na akahajiri kwenda al-Madiynah. Akajitolea mali tele katika njia ya Allaah (´Azza wa Jall) na akanunua kisima cha warumi kwa ajili ya waislamu. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Ni nani atayenunua kisima hichi na yuko na Pepo."[33]**

Akakinunua ´Uthmaan (Radhiya Allaahu ´anh) na akakifanya ni *Waqf* kwa waislamu. Akaandaa jeshi la ´Usrah kikamilifu kutokana na mali yake. Yeye ndiye ambaye alishika uongozi baada ya ´Umar kwa maafikiano ya watu wa mashauriano ambao aliwateulia ´Umar (Radhiya Allaahu ´anh). Wakampa kiapo cha usikivu na utiifu na waislamu kadhalika wakafanya hivo.

Isitoshe yeye ni mume wa wasichana wawili wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambao ni Ruqayyah na Umm Kulthuum. Ndio manaa akaitwa Dhun-Nurayn (*aliye na nuru mbili*) kwa kuwa alioa wasichana wawili wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Pindi Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipomtuma Makkah kuzungumza na washirikina na kukaenezwa uvumi kwamba ameuawa, Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akamtolea *bay´ah* kwa mkono wake kwa kusema:

**"Hii ni kwa ajili ya ´Uthmaan."[34]**

[33] al-Bukhaariy (2778)

*Bay´ah* ikatimia pasi na yeye kuwepo kwa kuwa wakati huo alikuwa Makkah.

Kadhalika yeye ndiye ambaye aliandika msahafu unaoitwa "msahafu wa ´Uthmaan" kwa hati ya ´Uthmaan. Hati yake ndio hii misahafu tulionayo hii leo. Fadhila zake ni nyingi (Radhiya Allaahu ´anh).

[34] al-Bukhaariy (3698) na (4066)

## 51. Baadhi ya fadhila za ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh)

Amesema mwandishi (Rahimahu Allaah):

16- *Wanne wao ni kiumbe bora anaye kuja baada yao*

*´Aliy kiongozi mwema kwa kheri*

**MAELEZO**

Anayefuata baada ya ´Uthmaan katika ubora ni kiongozi wa waumini ´Aliy bin Abiy Twaalib. Ni mtoto wa ami yake Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na mume wa msichana wake Faatwimah ambaye Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimwambia:

**"Je, huridhii kwangu uwe na manzilah kama Haaruun aliokuwa nayo kwa Muusa pamoja na kuwa hakuna Nabii mwingine baada yangu."**[35]

Hapa ilikuwa katika vita vya Tabuuk. Pindi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipomwacha al-Madiynah akahisi uzito wa kubakia. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akamkinaisha na kumwambia:

**"Wewe kwangu manzilah yako ni kama Haaruun aliokuwa nayo kwa Muusa."**

Kwa sababu Muusa alipoenda kwenye miadi ya Mola Wake alimwachia usimamizi Haaruun. Amesema:

اخْلُفْنِي فِي قَوْمِي

**“Shika mahali pangu." (07:142)**

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimwachia ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) ashike mahali pake nafasi. Haina maana kwamba yeye ndiye khaliyfah baada ya kufa kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kama

[35] al-Bukhaariy (3706) na (4416) na Muslim (2404) na (32)

wanavyosema Raafidhwah. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alifanya pamoja na ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) alipoenda katika Tabuuk kama jinsi alivyofanya Muusa pamoja na Haaruun (´alayhimaas-Salaam) alipoenda katika miadi ya Mola Wake. Amesema (Ta´ala):

وَقَالَ مُوسَىٰ لِأَخِيهِ هَارُونَ اخْلُفْنِي فِي قَوْمِي وَأَصْلِحْ وَلَا تَتَّبِعْ سَبِيلَ الْمُفْسِدِينَ

**"Muusa akasema [kumwambia] ndugu yake Haaruun: “Shika mahali pangu katika [kuwasimamia] watu wangu na tengeneza na wala usifuate njia ya mafisadi."" (07:142)**

Hii ni moja katika fadhila zake (Radhiya Allaahu ´anh).

Yeye ndiye ambaye vilevile aliwapiga vita Khawaarij na akazuia fitina yao na waislamu wakastarehe na shari yao. Hivyo ikawa imepatikana kwake bishara ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika kuwapiga vita.

´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) ndiye kijana aliye huru wa kwanza kusilimu. Abu Bakr asw-Swiddiyq (Radhiya Allaahu ´anh) ndiye mwanaume aliye huru wa kwanza kusilimu. Zayd bin Haarith (Radhiya Allaahu ´anh) ndiye mtu wa kwanza aliyeachwa huru aliyesilimu. Bilaal bin Rabaah (Radhiya Allaahu ´anh) ndiye mtumwa wa kwanza kusilimu. Khadiyjah bint Khuwaylid (Radhiya Allaahu ´anhaa) ndiye mwanamke wa kwanza kusilimu.

´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) ni katika wale wa awali waliotangulia kuingia katika Uislamu. Mke wake ni msichana wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambaye ni Faatwimah. Anaitwa Abul-Hasanayn; al-Hasan bin ´Aliy na al-Husayn bin ´Aliy (Radhiya Alolaahu ´anhumaa) ambao ndio viongozi wa vijana wa Peponi. Ana fadhila nyingi.

Yeye ndiye ambaye Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alisema juu yake siku ya Khaybar:

**"Nitampa bendera hii mwanaume anayempenda Allaah na Mtume Wake na Allaah na Mtume Wake nao wanampenda."[36]**

Maswahabah walikuwa wanavizia na kila mmoja akawa anataka yeye ndiye awe mtu huyu ambaye anampenda Allaah na Mtume Wake na Allaah na Mtume Wake nao pia wanampenda. Ikawa si mwingine ni ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh). Hii ni moja ya fadhila zake kubwa - Allaah awawie radhi wote.

[36] al-Bukhaariy (3009) na (3701) na (4210) na Muslim (2406) na (34)

## 52. Fadhila za Maswahabah kumi waliobashiriwa Pepo

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

17- *Hakika ni kikundi kisichokuwa na shaka yoyote juu yao*

*watakuwa juu ya farasi wa kwenye Firdaws kwa nuru wakitembea*

18- *Sa´iyd, Sa´d, Ibn ´Awf na Twalhah*

*´Aamir Fihr na az-Zubayd wenye kusifiwa*

**MAELEZO**

***Hakika ni kikundi... -*** Kikundi kinachokusudiwa hapa ni watu wasiopungua kumi. Wanaokusudiwa hapa ni wale kumi walioahidiwa Pepo[37].

***... juu ya farasi wa kwenye Firdaws... -*** Bi maana juu ya farasi wa Peponi.

***... kwa nuru wakitembea -*** Wakienda wapendapo.

Pindi alipowataja Maswahabah kumi (Radhiya Allaahu ´anhum) hapa ndipo akawataja wale kumi walioahidiwa Pepo. Wamebaki sita miongoni mwa wale kumi:

**Wa kwanza:** Sa´iyd. Anaitwa Sa´iyd bin Zayd bin ´Amr bin Nufayl. Ni mtoto wa ami yake ´Umar bin al-Khattwaab. Alikuwa ni mume wa dada yake na ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhum).

**Wa pili:** Sa´d. Anaitwa Sa´d bin Abiy Waqqaas az-Zuhriy (Radhiya Allaahu ´anh).

[37] Abu Daawuud (4650) na (4649), at-Tirmidhiy (3757) na (3748), an-Nasaa´iy (1630), Ibn Maajah (134), Ahmad (01/187-188) na wengineo.

**Wa tatu:** Ibn ´Awf. Anaitwa ´Abdur-Rahmaan bin ´Awf (Radhiya Allaahu ´anh). Alikuwa ni katika Maswahabah matajiri na miongoni mwa wale ambao wanajitolea sana katika njia ya Allaah (´Azza wa Jall).

**Wa nne:** Twalhah. Anaitwa Twalhah bin ´Ubaydillaah (Radhiya Allaahu ´anh).

**Wa tano:** ´Aamir. Anaitwa Abu ´Ubaydah ´Aamir bin Jarraah (Radhiya Allaahu ´anh). Yeye ndiye mwaminifu wa Ummah huu.

Fihr alikuwa ni katika babuze Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na katika mababa wa ma-Quraysh.

**Wa sita:** az-Zubayr. Anaitwa az-Zubayr bin ´Awwaam (Radhiya Allaahu ´anh). Alikuwa ni msaidizi wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Hawa sita, pamoja na wale makhaliyfah wanne, wanakuwa kumi waliobashiriwa Pepo. Wao ndio Maswahabah bora. Wote wanatokamana na kabila la Quraysh.

## 53. Kuzungumza maneno mazuri juu ya Maswahabah wote

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

19- *Zungumza maneno mazuri juu ya Maswahabah wote*

*usiwe ni mtusi kazi yako ni kutia aibu na kujeruhi*

20- *Wahy wenye kubainisha umezitamka fadhila zao*

*na katika "al-Fath" kuna Aayah inayowasifu*

**MAELEZO**

Alipowataja waliobakia baada ya kuwataja wale kumi waliobashiriwa Pepo ndio akasema:

*Zungumza maneno mazuri*

ili isije kudhaniwa kwamba akitajwa yule Swahabah ambaye ni mbora zaidi ina maana ni kumtukana yule ambaye anashindwa ubora. Wote ni Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wana fadhila za usuhubiano na kumnusuru Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Walipokea kutoka kwake, wamepokea kutoka kwa Mtume, wakamuamini, wakakusanyika naye, wakaswali nyuma yake na wakamsikia (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

***... kwa Maswahabah wote -*** Bi maana Maswahabah wote wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Wasifu na uwatape kwa kuwa wanastahiki sifa na matapo haya.

***usiwe ni mtusi kazi yako ni kutia aibu na kujeruhi -*** Haijuzu kumtukana yeyote katika wao au kuzitaja aibu zao. Hivi ndivyo wanavyofanya Raafidhwah Allaah akawakebehi. Wao ni maadui wa dini, ni maadui wa

Ummah na ni maadui wa Uislamu. Hivi vilevile ndivyo wanavyofanya Khawaarij ambao wamewakufurisha Maswahabah.

***Wahy wenye kubainisha umezitamka fadhila zao -*** Wahy kunaingia Qur-aan na Sunnah. Wahy, ambao ni Qur-aan na Sunnah, umezitaja fadhila za Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ambaye anawatukana ni mwenye kukadhibisha Kitabu cha Allaah na Sunanh za Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Amesema (Ta´ala):

وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُم بِإِحْسَانٍ رَّضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتَهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

**"Na wale waliotangulia awali katika *Muhaajiruun* na *Answaar* na wale waliowafuata kwa wema, Allaah ameridhika nao nao wameridhika Naye na amewaandalia mabustani ipitayo chini yake mito - ni wenye kudumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa." (09:100)**

Katika Suurah "al-Fath" ambayo inaanza kwa:

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا

**"Hakika tumekufungulia ushindi ambao ni wa wazi." (48:01)**

kumetajwa sifa zenye kukariri juu ya Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mwanzoni mwake amesema (Ta´ala):

لِّيُدْخِلَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَيُكَفِّرَ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ ۚ وَكَانَ ذَٰلِكَ عِندَ اللَّهِ فَوْزًا عَظِيمًا

**"Ili Awaingize waumini wa kiume na waumini wa kike [ndani ya] mabustani yapitayo chini yake mito - ni wenye kudumu humo milele - na Awafutie maovu yao na limekuwa hilo mbele ya Allaah, ni kufuzu kukubwa." (48:05)**

إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّهَ يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ ۚ فَمَن نَّكَثَ فَإِنَّمَا يَنكُثُ عَلَىٰ نَفْسِهِ ۖ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِمَا عَاهَدَ عَلَيْهُ اللَّهَ فَسَيُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا

**"Hakika wale waliofungamana ahadi ya utiifu nawe, hakika hapana vyengine ila wanafungamana ahadi ya utiifu na Allaah. Mkono wa Allaah uko juu ya mikono yao. Basi atakayevunja [fungamano hilo], hakika hapana ila anavunja dhidi ya nafsi yake na yeyote atimizaye yale aliyomuahidi Allaah, basi Atampa ujira mkubwa." (48:10)**

لَّقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنزَلَ السَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ

**"Hakika Allaah amewawia radhi waumini waliokupa kiapo cha usikivu na utiifu chini ya mti. Alijua yale yaliyomo nyoyoni mwao. Basi Akawateremshia utulivu na akawalipa ushindi wa karibu." (48:18)**

Mwishoni mwake akasema:

مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ اللَّهِ ۚ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ ۖ تَرَاهُمْ رُكَّعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا ۖ سِيمَاهُمْ فِي وُجُوهِهِم مِّنْ أَثَرِ السُّجُودِ ۚ ذَٰلِكَ مَثَلُهُمْ

**"Muhammad ni Mtume wa Allaah. Na wale walio pamoja naye ni wakali zaidi dhidi ya makafiri wanahurumiana baina yao. Utawaona wakirukuu na wakisujudu wakitafuta fadhila na radhi kutoka kwa Allaah. Alama zao dhahiri zi katika nyuso zao kutokana na athari za sujudu. Huo ni mfano wao...** "

Bi maana sifa zao:

فِي التَّوْرَاةِ

**"... katika Tawraat.... "**

Ambayo aliteremshiwa Muusa (´alayhis-Swalaatu was-Salaam).

وَمَثَلُهُمْ

**"... na ni mfano wao.... "**

Bi maana sifa zao:

فِي الْإِنجِيلِ

**"... katika Injiyl... "**

Ambayo aliteremshiwa ´Iysaa (´alayhis-Swalaatu was-Salaam).

كَزَرْعٍ أَخْرَجَ شَطْأَهُ فَآزَرَهُ فَاسْتَغْلَظَ فَاسْتَوَىٰ عَلَىٰ سُوقِهِ يُعْجِبُ الزُّرَّاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ ۗ وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنْهُم مَّغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا

**"... kama mmea umetoa chipukizi lake, likautia nguvu kisha likawa nene, kisha likasimama sawasawa juu ya shina lake liwapendezeshe wakulima ili liwaghadhibishe makafiri. Allaah amewaahidi wale walioamini na wakatenda mema miongoni mwao maghfirah na ujira mkubwa." (48:29)**

Hizi ndio sifa zao zilizomo katika Tawrat na Injiyl.

Amesema (Ta´ala):

لِيَغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ

**"... ili liwaghadhibishe makafiri." (48:29)**

Ni dalili inayofahamisha kuwa yule anayewachukia au kuwabughudhi Maswahabah ni kafiri. Kutokana na andiko la Aayah hii tukufu.

## 54. Baadhi ya fadhila za wajukuze, wana na wakeze Mtume na Mu´aawiyah

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

21- *Vilevile wajukuze Mtume wa Allaah na wana wa Khadiyjah*

*na Faatwimah ambaye alikuwa mtakasifu*

22- *Vilevile na ´Aaishah ambaye ni mama wa waumini na mjomba wetu*

*ambaye si mwengine ni Mu´aawiyah muheshimiwa*

**MAELEZO**

***Wajukuze Mtume wa Allaah -*** Bi maana al-Hasan na al-Husayn (Radhiya Allaahu ´anhumaa). al-Hasan na al-Husayn ni wajukuze wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Bi maana ni watoto wa msichana wake Faatwimah. Wao ndio:

**"Viongozi wa vijana wa Peponi."**[38]

kama alivyosema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

***... wana wa Khadiyjah -*** Watoto wote wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wanatokamana na Khadiyjah. Isipokuwa Ibraahiym peke yake. Yeye mama yake ni Maariyah Qibtwiyyah. Kuhusu watoto wengine wote wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wanatokamana na Khadiyjah (Radhiya Allaahu ´anhaa). Alizaa nae wavulana wawili waliokufa katika uhai wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika mji wa Makkah.

[38] Kuna idadi kubwa ya Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) ambao wamepokea Hadiyth hii mpaka as-Suyuutwiy akasema: "Hili ni jambo limepokelewa kwa njia nyingi." Faydhw al-Qadiyr (03/415)

***na Faatwimah -*** Faatwimah ambaye ni binti wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa anampenda. Faatwimah alipokuwa anafika anamsimamia na kumbusu na kumkalisha pembezoni nae.

***Vilevile na ´Aaishah ambaye ni mama wa waumini... -*** Yeye ndiye mwanamke aliyekuwa akipendwa zaidi na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mwanaume aliyekuwa akipendwa zaidi na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni baba yake ambaye ni Abu Bakr asw-Swiddiyq (Radhiya Allaahu ´anh)[39].

***... mjomba wetu ambaye si mwengine ni Mu´aawiyah -*** Mu´aawiyah bin Abiy Sufyaan (Radhiya Allaahu ´anh). Huyu alikuwa ni Swahabah mtukufu. Alikuwa ni mwandishi wa Wahy. Alikuwa akimwandikia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) Qur-aan. Alikuwa ni mjomba wa waumini kwa sababu dada yake ambaye ni Umm Habiybah ni mkewe Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hivyo yeye anakuwa ni mjomba wa waumini. Bi maana yeye ni kaka wa mama wa waumini. Hizi ni katika fadhila zake (Radhiya Allaahu ´anh).

[39] Ameyapokea haya al-Bukhaariy (4358) na (3662) na Muslim (08) na (2384)

## 55. Baadhi ya fadhila za Muhaajiruun na Answaar

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

23- *Vilevile na Wanusuraji wake na Wahajiri wa miji yao*

*kwa unusuraji wao wameokolewa na Moto*

**MAELEZO**

Muhaajiruun na Answaar vilevile wana fadhila kubwa. Amesema (Jalla wa ´Alaa):

وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنصَارِ

**"Na wale waliotangulia awali katika *Muhaajiruun* na *Answaar...* " (09:100)**

Muhaajiruun ni wale waliohama kutoka Makkah kwenda al-Madiynah. Walihama wakaiacha miji yao kwa ajili ya kuunusuru Uislamu.

Answaar ni wale waliomnusuru Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wakawasaidia ndugu zao katika mji wa kuhamia. Haya yametajwa katika Suurah "al-Hashr":

لِلْفُقَرَاءِ الْمُهَاجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِن دِيَارِهِمْ وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا وَيَنصُرُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۚ أُولَٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ

**"Mafuqara *Muhaajiruun* ambao wametolewa kutoka majumbani mwao na [zikataifishwa] mali zao wanatafuta fadhila na radhi kutoka kwa Allaah na wanamnusuru Allaah na Mtume Wake - hao ndio wakweli." (59:08)**

Halafu akasema kuhusu Answaar:

وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيمَانَ مِن قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِّمَّا أُوتُوا وَيُؤْثِرُونَ عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ
خَصَاصَةٌ ۚ وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ

**"Na wale waliokuwa na makazi na wakawa na imani kabla yao wanawapenda wale waliohajiri kwao na wala hawapati kuhisi uzito wowote vifuani mwao kwa yale waliyopewa [*Muhaajiruun*] na wanawapendelea kuliko nafsi zao japokuwa wao wenyewe wako na njaa. Na yeyote anayeepushwa na ubakhili na tamaa ya uchu wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufaulu." (59:09)**

***kwa unusuraji wao wameokolewa na Moto -*** Allaah amewaokoa na Moto kwa kusuhubiana kwao na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

## 56. Fadhila za baadhi ya maimamu wa Ahl-us-Sunnah

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

24- *Walioko baada yao ni Taabi´uun kwa uchukuliaji wao mzuri*

*sawa kwa matendo na maneno yao na wakawa ni wenye kufaulu*

25- *Pia na Maalik, ath-Thawriy na halafu ndugu zao*

*Abu ´Amr al-Awzaa´iy*

26- *Waliokuja baada yao ash-Shaafi´iy na Ahmad*

*ni imamu wa uongofu mwenye kufuata haki na kunasihi*

27- *Hao ni watu waliosamehewa na Allaah*

*hivyo wapende hakika utafurahi*

**MAELEZO**

***Walioko baada yao... -*** Wanaofuatia baada ya Maswahabah ni Taabi´uun. Allaah (Ta´ala) amesema:

وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُم بِإِحْسَانٍ

**"Na wale waliotangulia awali katika *Muhaajiruun* na *Answaar* na wale waliowafuata kwa wema." (09:100)**

Maneno Yake:

وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُم بِإِحْسَانٍ

**"... na wale waliowafuata kwa wema."**

yanajumuisha wale wote waliowafuata kwa wema hadi siku ya Qiyaamah. Lakini kunaposewa neno "Taabi´iy" kunakusudiwa yule ambaye alichukua elimu na akasoma kutoka kwa Swahabah. Vinginevyo neno "mfuataji" linajumuisha kila yule ambaye alichukua na akapita juu ya mfumo wa Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), kuanzia wale wa mwanzo, ambao walikuwa baada ya Maswahabah na wa mwisho. Kwa ajili hii amesema (Jalla wa ´Alaa) baada ya kuwataja Muhaajiruun na Answaar:

وَالَّذِينَ جَاءُوا مِن بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِّلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

**"Na wale waliokuja baada yao wanasema: "Mola wetu! Tusamehe sisi na ndugu zetu ambao wametutangulia kwa imani na wala Usijaalie katika nyoyo zetu mafundo ya chuki kwa wale walioamini. Mola wetu! Hakika Wewe ni Mwenye huruma, Mwenye kurehemu." (59:10)**

Katika Aayah hii kuna Radd kwa Raafidhwah ambao wanawachukia Maswahabah wa Mtume wa Allaah kwa mioyo yao na wanatamka kwa ndimi zao. Bali wanawalaani kabisa na kuwakufurisha Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kwa ajili hii ndio maana Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) amesema:

"Miongoni mwa misingi ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ni kuwa na mioyo na ndimi safi kwa Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)."[40]

Wana mioyo safi kutokana na maneno Yake:

وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا

**"... na wala Usijaalie katika nyoyo zetu mafundo ya chuki."**

[40] ´Aqiydah al-Waasitwiyyah katika "Majmuu´-ul-Fataawaa" (03/152).

Vilevile wana ndimi safi kutokana na maneno Yake:

يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ

**"Wanasema: "Mola wetu! Tusamehe sisi na ndugu zetu ambao wametutangulia kwa imani.""**

Katika Aayah hii kuna mafunzo ya kwamba inatakiwa kwa mtu awe na moyo na ulimi mzuri kwa Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Huu ndio mfumo wa wale wenye kuwafuata kwa wema.

Kuhusu wale ambao wanajeruhi, kupekua kasoro, kutatiza juu ya fadhila za Maswahabah, kuwakufurisha na kuwalaani, haya ni mambo yanayoenda kinyume na mfumo wa Kiislamu, anaujengea uadui Uislamu na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kwa sababu akiwatukana Maswahabah wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amemtukana Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Vilevile ameitukana Qur-aan inayowasifu na kuwatapa.

***Pia na Maalik, ath-Thawriy na halafu ndugu... -*** Mwandishi (Rahimahu Allaah) anataja fadhila za maimamu. Miongoni mwao ni maimamu hawa:

Maalik mkusudiwa ni Maalik bin Anas ambaye ni Imaam wa al-Madiynah.

ath-Thawriy mkusudiwa ni Sufyaan ath-Thawriy.

al-Awzaa´iy mkusudiwa ni Imaam wa watu wa Shaam.

***Waliokuja baada yao ash-Shaafi´iy na Ahmad -*** Ni Muhammad bin Idriys ash-Shaafi´iy na Ahmad bin Hanbal.

***hivyo wapende hakika utafurahi -*** Wapende as-Salaf as-Swaalih na maimamu wa Uislamu. Hakika kufanya hivo ni alama ya imani.

Hakumtaja Abu Haniyfah kwa kuwa imesemekana kuwa yeye ni katika Taabi´uun na kwamba alikutana na kundi la Maswahabah. Maoni sahihi ni kwamba yeye ni katika waliokuja baada ya Taabi´uun. Hakukutana na

Maswahabah. Alikutana na Taabi´uun. Yeye ni mtu wa karne ya tatu ambayo ni moja ya zile karne bora (Rahimahu Allaah). Yeye ndiye imamu wa kwanza miongoni mwa wale maimamu wane inapokuja katika zama.

## 57. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya Qadhwaa´ na Qadar

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

28- *Yakinisha makadirio yaliyopangwa*

*hakika ndio nguzo ya dini na dini imeenea*

**MAELEZO**

Kuamini Qadar ni nguzo ya sita miongoni mwa nguzo za imani. Jibriyl (´alayhis-Salaam) alikuja kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akamuuliza amkhabarishe juu ya imani ambapo (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema:

**"Imani kumuamini Allaah, Malaika Wake, vitabu Vyake, Mitume Wake, siku ya Mwisho na kuamini Qadar kheri na shari yake."**[41]

Akafanya (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuamini Qadar ni nguzo ya sita ya imani.

Kuamini Qadhwaa´ na Qadar ni kule kuamini elimu ya Allaah (Jalla wa ´Alaa), kuyakadiria Kwake mambo kabla ya kutokea Kwake, matendo ya Allaah (Jalla wa ´Alaa), utashi na matakwa Yake na kuumba Kwake. Ni jambo kubwa. Katika Qur-aan amesema (Ta´ala):

وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَّرَهُ تَقْدِيرًا

**"Ameumba kila kitu na Akakikadiria kipimo sawasawa." (25:02)**

إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ

**"Hakika sisi Tumekiumba kila kitu kwa makadirio." (54:49)**

[41] Muslim (01) na (08)

Bi maana amekadiria kutokea kwake, kupatikana kwake na akayaumba. Vilevile akakadiria sifa na wakati wake ambapo yatatokea. Hivyo kila kitu kimekadiriwa kwa njia zake zote:

Ya kwanza: Kwa njia ya kuyatambua.

Ya pili: Kwa njia ya kuyaandika katika Ubao uliohifadhiwa.

Ya tatu: Kwa njia ya Allaah kuyataka kwa muda wake.

Ya nne: Kwa njia ya kuyaumba.

Kila kitu kina sifa yake ambayo Allaah ameijaalia. Kitu hicho hakizidi na wala hakipungui. Hiki ni kitu pia kimekadiriwa. Kwa mfano amesema (Ta´ala) kuhusu mvua:

وَمَا نُنَزِّلُهُ إِلَّا بِقَدَرٍ مَّعْلُومٍ

**"Hatuiteremshi isipokuwa kwa kadiri maalumu." (15:21)**

Kile kima, pahali inapoteremka na wakati itapoteremka yote Allaah anayajua kwa njia zake zote. Hakuna kitu isipokuwa Allaah (Jalla wa ´Alaa) alikijua , akakiumba na akakikadiria. Hakikupatikana pasi na kuumbwa, bila ya kutangulia kukadiriwa, bila ya kuandikwa kwenye Ubao uliohifadhiwa na wala pasi na Allaah (Jalla wa ´Ala) kukitaka kwanza. Mambo yanayopitika ulimwenguni hayapitiki hivi hivi. Bali mambo hayo yamedhibitiwa kwa Allaah kuyakadiria, kuyaumba na kuyataka kwa sifa ilizonazo. Hili ni jambo muhimu sana.

Kuna watu vigogo ambao hawaangalii Aayah za Qur-aan na Hadiyth za kinabii waliopotea katika mambo haya. Wao wanategemea akili na fikira zao. Hivyo matokeo yake wakachanganya mambo hali ya kutia aibu katika Qadhwaa´ na Qadar. Upande mwingine Allaah akawaongoza Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Wakaiamini kwa njia ambayo Allaah ameitaka na ameiwajibisha juu ya waja Wake kwa mujibu wa dalili za Qur-aan na Sunnah. Hii ndio ada yao katika milango yote inayohusiana na ´Aqiydah.

## 58. Utafiti juu ya Qadhwaa´ na Qadar

Utafiti juu ya Qadhwaa´ na Qadar ndani yake kuna mambo mengi:

Mosi: Ni kuhusu maana ya Qadhwaa´ na Qadar. Qadar ni Allaah (Jalla wa ´Alaa) kuyakadiria, kuyataka na kuyaumba mambo katika wakati wake. Hii ndio maana ya Qadar. Mara nyingi kunaposemwa Qadhwaa´ na Qadar hakuna tofauti kati yake. Hata hivyo Qadhwaa´ imeenea zaidi kuliko Qadar. Kwa sababu wakati mwingine Qadhwaa´ inakuja ikiwa na maana ya Qadar. Wakati mwingine inakuja ikiwa na maana ya kwamba Allaah amevikadiria vitu na kuvipanga. Vilevile wakati mwingine inakuja ikiwa na maana ya kuwahukumu watu kati ya yale waliyotofautiana:

إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ

**Hakika Mola wako atahukumu baina yao siku ya Qiyaamah katika yale waliyokuwa wakikhitilafiana nayo." (45:17)**

Kwa hivyo Qadhwaa´ imeeneza zaidi kuliko Qadar.

Pili: Kuhusu kuamini Qadhwaa´ na Qadar. Kuamini Qadhwaa´ na Qadar ni wajibu na ni faradhi juu ya muumini. Kwa kuwa ni nguzo miongoni mwa nguzo za imani sita. Jengine ni kwa sababu ni kuamini uwezo wa Allaah (Jalla wa ´Alaa). Kwa ajili hii ndio maana amesema:

"Qadar ni uwezo wa Allaah. Mwenye kuipinga basi amepinga uwezo wa Allaah (Jalla wa ´Alaa)."[42]

Katika baadhi ya ibara vilevile imekuja:

"Qadar ni siri ya Allaah kwa viumbe Wake."[43]

---

[42] Ibn Battwah katika "al-Ibaanah" (02/231) na "al-Minhaaj as-Sunnah an-Nabawiyyah" (03/254)

[43] al-Laalakaa´iy katika "I´tiqaad Ahl-is-Sunnah" (1122) (03/1122) na Abu Na´iym katika "al-Hilyah" (06/181)

Haijuzu kutafiti Qadhwaa´ na Qadar mtu akavuka zile dalili zilizokuja katika Qur-aan na Sunnah na akajikakamua. Haya hatimae yanapelekea katika upotevu na kuchanganyikiwa. Kwa sababu ni siri ya Allaah kwa waja Wake. Pindi utapojikakama na kufanya utafiti hutofikia natija yoyote. Kwa kuwa utakuwa ni mwenye kutafiti jambo ambalo Allaah (Jalla wa ´Alaa) ameliwaficha viumbe Wake. Inatosha kwako kuamini peke yake. Hakuna yeyote aliyejikakama akafikia natija yoyote. Bali kinyume chake alifikia katika kuchanganyikiwa. Kwa ajili hiyo inatosheleza kwako kutembea kwa mujibu wa dalili zilizothibiti katika Qur-aan na Sunnah juu ya kuthibitisha Qadar na kuiamini. Haya yanakutosheleza.

## 59. Utafiti juu ya Qadhwaa´ na Qadar II

Tatu: Kuhusu ngazi za kuamini Qadhwaa´ na Qadar. Kuamini Qadhwaa´ na Qadar ndani yake mna ngazi nne:

Ngazi ya kwanza: Kuamini kuwa Allaah aliyajua yaliyopo na yatayokuwepo kutokana na elimu Yake ya milele ambayo anasifika nayo daima na milele. Hakuna kitu, kilichopo na kitachokuwepo, isipokuwa Allaah (Jalla wa ´Alaa) anakijua. Amesema (Ta´ala):

وَمَا تَسْقُطُ مِن وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلُمَاتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ

**"Halianguki jani lolote ila Hulijua, na wala punje katika viza vya ardhi, na wala kilichorutubika na wala kikavu isipokuwa [kimedhibitiwa] katika Kitabu kinachobainisha" (06:59)**

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۖ مَا يَكُونُ مِن نَّجْوَىٰ ثَلَاثَةٍ إِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ وَلَا أَدْنَىٰ مِن ذَٰلِكَ وَلَا أَكْثَرَ إِلَّا هُوَ مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُوا

**"Je, huoni kwamba Allaah anajua yaliyomo mbinguni na yaliyomo ardhini? Hauwi mnong'ono wa watu watatu isipokuwa Yeye ni wa nne wao, na wala wa watu watano isipokuwa Yeye ni wa sita wao, na wala wa chini kuliko ya hivyo na wengi zaidi isipokuwa Yeye Yu pamoja nao [kiujuzi] popote watakapokuwa." (58:07)**

Hakika Yeye anayajua yale mazungumzo na minong´ono inayokuwa kati ya watu. Vilevile Yeye (Subhaanah):

لَا جَرَمَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ

**"Hapana shaka kwamba Allaah anajua wanayoyafanya siri na wanayayoyadhihirisha." (16:23)**

وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ

**"Allaah anayajua yaliyomo vifuani." (03:154)**

وَيَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

**"Anajua yale yaliyomo katika mbingu na yale yaliyomo katika ardhi." (03:29)**

إِنَّ اللَّهَ لَا يَخْفَىٰ عَلَيْهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ

**"Hakika Allaah hakifichiki Kwake chochote katika ardhi wala katika mbingu." (03:05)**

Elimu ya Allaah imekusanya yaliyokuwepo, yatayokuwepo na yasiyokuwepo lau yangelikuwepo vipi yangalikuwa. Hivyo elimu ya Allaah (Jalla wa ´Alaa) imekusanya na imekizunguka kila kitu. Inahusiana na yaliyokuwepo hapo kale, yaliyopo hivi sasa na yatayokuwepo huko mbeleni.

Ngazi ya pili: Uamini na kuitakidi kuwa Allaah ameandika kwenye Ubao uliohifadhiwa kila kitu. Ubao uliohifadhiwa ni kitu kilichoumbwa. Hakuna anayejua namna ilivyo na ukubwa wake isipokuwa Allaah (Jalla wa ´Alaa). Ubao huo uko huko Kwake (Jalla wa ´Alaa). Tunauamini na vilevile tunaamini kuhusu uandikwaji huu. Imekuja katika Hadiyth:

**"Kitu cha kwanza alichoumba Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) ni kalamu kisha Akaiambia: "Andika!" Ikasema: "Niandike nini?" Akasema: "Andika yatayokuwepo hadi Qiyaamah kisimame.""[44]**

Hivyo ikawa imeandika yatayokuwepo mpaka siku ya Qiyaamah.

Vilevile imekuja katika Hadiyth ya kwamba:

**"Allaah aliandika makadirio ya viumbe miaka elfu khamsini kabla ya kuumba mbingu na ardhi na ´Arshi Yake ilikuwa juu ya maji."[45]**

´Arshi na kalamu ni kipi kilichotangulia kuwepo? Kuna kundi lililosema kuwa ´Arshi ndio ilitangulia kabla ya kalamu. Kundi lingine likasema kuwa kalamu

[44] Abu Daawuud (4700), at-Tirmidhiy (2155) na (3319), Ahmad (05/317) na wengieno

[45] Muslim (16) na (2653)

ndio ilitangulia kabla ya ´Arshi. Kundi lingine likapambanua. Ibn-ul-Qayyim (Rahimahu Allaah) amesema:

*Watu wametofautiana juu ya kalamu ambayo*

*imeandika Qadhwaa´ kutoka kwa Allaah*

*Je, ilikuwa kabla ya ´Arshi au baada yake?*

*kuna maoni mawili kwa Abu ´Alaa al-Hamadhaaniy*

*Maoni sahihi ni kuwa ´Arshi ndio ilikuwa kabla yake [kalamu]*

*kwa kuwa kipindi cha maandiko ilikuwa iko na nguzo*

Uandishi ulitokea sambamba ilipopatikana kalamu. Pindi Allaah alipoiumba ndipo akaiambia:

"Andika."

Kwa mtazamo wa kupatikana, ´Arshi ndio ilitangulia kuwepo. Haya ndio maoni sahihi. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Allaah alikadiria makadirio ya viumbe miaka elfu khamsini kabla ya kuumba mbingu na ardhi na ´Arshi Yake ilikuwa juu ya maji."**

Aliyakadiria kabla ya uandishi kisha ndio akayaandika. Uandishi ulitokea baada ya kupatikana kwa kalamu. Kupatikana kwa kalamu kulikuja nyuma baada ya ´Arshi. ´Arshi ndio ilitangulia. Ni lazima kuyatambua mambo haya kwa sababu yanaingia katika ngazi ya uandishi. Inahusiana na uandishi wa jumla ulioenea ambapo kuliandikwa kila kitu.

Pengine mtu akauliza Allaah si anamuamrisha Malaika ambaye amewakilishwa kuandika riziki, muda wa kueshi na kama atakuwa mla khasara au mwenye furaha wale watoto walio tumboni mwa mama zao, kama alivyosema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Hakika umbo la kila mmoja wenu linakusanywa pamoja katika tumbo la mama yake kwa muda wa siku arobaini, kisha inakuwa mbegu kwa muda**

**kama huo, kisha inakuwa kama tone la damu kwa muda kama huo, halafu anatumiwa Malaika ambaye humpulizia roho na huamrishwa mambo mane: kuandika riziki yake, muda wake wa kueshi, matendo yake na kama atakuwa mla khasara au mwenye furaha."[46]**

Jibu ni kuwa huu ni upambanuzi wa yale yaliyoandikwa hapo kabla. Haya yamechukuliwa kutoka katika yale yaliyotangulia kuandikwa kwenye Ubao uliohifadhiwa.

Vilevile imekuja ya kwamba usiku wenye cheo Allaah hukadiria yatayopitika katika mwaka katika uhai, kufa, vita na mengineyo. Yote haya yanapitika katika usiku wenye cheo. Kwa ajili hii ndio maana ukaitwa kuwa ni usiku wenye cheo kwa kuwa ndani yake kunakadiriwa yatayopitika katika mwaka:

فِيهَا يُفْرَقُ كُلُّ أَمْرٍ حَكِيمٍ

**"Humo hubainishwa kila jambo la hikmah." (44:04)**

Jibu ni kama lililotangulia ya kwamba uandishi huu unaopitika katika usiku wenye cheo umechukuliwa kutoka katika ule uandishi ulioenea katika Ubao uliohifadhiwa. Kwa hivyo hakuna mgongano kati ya dalili. Dalili ya daraja hizi mbili - ambayo ni elimu na uandishi - ni maneno Yake (Ta´ala):

مَا أَصَابَ مِن مُّصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّن قَبْلِ أَن نَّبْرَأَهَا

**"Hausibu msiba wowote katika ardhi au katika nafsi zenu isipokuwa umo katika Kitabu kabla hatujauumba." (57:22)**

Bi maana kuumba. Ni dalili yenye kuonesha kuwa misiba yote inayopitika imeandikwa katika Ubao uliohifadhiwa.

Ngazi ya tatu: Utashi na matakwa. Kila chenye kupitika basi Allaah amekitaka. Hakupitiki kitu katika ufalme Wake (Subhaanahu wa Ta´ala) Asichokitaka. Amesema (Ta´ala):

[46] al-Bukhaariy (3208), (3332) na Muslim (01) na (2643)

فَعَّالٌ لِّمَا يُرِيدُ

**"Mwingi wa kufanya Atakalo." (85:16)**

إِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ

**"Hakika Allaah anafanya atakavyo." (22:18)**

وَمَا تَشَاؤُونَ إِلَّا أَن يَشَاء اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**"Wala nyinyi hamtataka isipokuwa atake Allaah, Mola wa walimwengu wote." (81:29)**

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا اقْتَتَلُوا وَلَكِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ

**"Na lau Allaah angelitaka wasingelipigana, lakini Allaah anafanya alitakalo." (02:253)**

Kila chenye kupitika basi Allaah amekitaka baada ya kukijua na kukiandika kwenye Ubao uliohifadhiwa.

Ngazi ya nne: Kuumba. Amesema (Ta´ala):

اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ

**"Allaah ndiye muumbaji wa kila kitu - Naye juu ya kila kitu ni mtegemewa." (39:62)**

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ

**"Na hali Allaah amekuumbeni na yale mnayoyatenda." (37:96)**

مِّن قَبْلِ أَن نَّبْرَأَهَا

**"... kabla hatujauumba." (57:22)**

Bi maana kabla ya Sisi kuumba. Aayah hizi zimetolea dalili kuthibitisha ngazi ya uandishi, uumbaji na utashi. Hizi ndio ngazi nne ambazo ni wajibu kuziamini:

Ya kwanza: Elimu.

Ya pili: Kuyaandika katika Ubao uliohifadhiwa.

Ya tatu: Kulitaka jambo pale linapotokea.

Ya nne: Kukiumba kitu.

Hizi ndio ngazi za Qadhwaa´ na Qadar. Ambaye anapinga moja wapo hawi mwenye kuamini Qadhwaa´ na Qadar.

## 60. Utafiti juu ya Qadhwaa´ na Qadar III

Nne: Kuhusu walioenda kinyume na Qadhwaa´ na Qadar. Kuna mapote mawili yaliyoenda kinyume na Qadhwaa´ na Qadar na yote mawili yanagongana:

La kwanza: Qadariyyah. Hawa ni wale wanaopinga Qadar. Wameitwa Qadariyyah. Mtu wa kwanza kusema hayo ni ´Amr bin ´Ubayd na Waaswil bin ´Atwaa' na akaepuka katika kikao cha Hasan al-Baswriy. Qadariyyah ambao wanapinga Qadar ni Mu´tazilah. Wamesema kuwa mja mwenyewe ndiye anaumba matendo yake na kwamba mambo hayakukadiriwa na Allaah. Wamesema kuwa matendo ya waja wao wenyewe ndio wanafanya yapatikane. Wanasema kuwa Allaah hana lolote, si utashi wala matakwa, kuhusiana nayo. Ndio maana wakaitwa "Qadariyyah". Hii ina maana kuwa mja ndiye anayeumba matendo yake mwenyewe. Kwa hali hii mtu anakuwa amethibitisha waumbaji wawili. Allaah (Jalla wa ´Alaa) ndiye muumbaji na kila kisichokuwa Yeye vimeumbwa. Wao wanapinga haya na kusema kuwa Allaah yuko pamoja Naye waumbaji wengine ambao ni wale waja wanaoumba matendo yao wenyewe. Huku ni kushirikisha katika uola. Kwa ajili hii Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amewaita:

**"Waabudu moto wa Ummah huu."**[47]

Kwa sababu wamethibitisha kuwepo kwa waumbaji wawili kama walivyofanya waabudu moto. Waabudu moto wamesema kuwa kuna waumbaji wawili; nuru ambayo inaumba mambo mazuri na giza mambo ya shari. Qadariyyah wakawazidi ambapo wamesema kuwa kila mmoja anaumba matendo yake mwenyewe. Hivyo wakawa ni wenye kuthibitisha waumbaji wengi pamoja na Allaah (´Azza wa Jall). Huku ni kushirikisha katika Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah.

[47] Abu Daawuud (3691), at-Twabaraaniy katika "al-Awsatw" (03/65) na wengineo

La pili: Jabriyyah. Hawa ni wafuasi wa Jahm bin Swafwaan. Wamesema kuwa mja hana khiyari wala matakwa yoyote. Wanaona kuwa ametenzwa nguvu kwa yale anayofanya pasi na yeye kuwa na khiyari. Wanasema ni kama chombo kilicho kwenye mikono ya yule mwenye kukiendesha. Ni kama upepo angani. Ni kama maiti kwenye mikono ya muoshaji. Wanaonelea kuwa mja ametenzwa nguvu katika matendo yake. Ni kama chombo chenye kuendeshwa.

Jabriyyah wamepindukia katika kuthibitisha utashi na matakwa ya Allaah na wakati huo huo wakapinga utashi na matakwa ya mja. Mu´tazilah wao ni kinyume wamepindukia katika kuthibitisha utashi na matakwa ya mja na wakati huo huo wakapinga utashi wa Allaah (´Azza wa Jall). Kila pote limoja katika hayo mawili yamekosea katika kitu kimoja:

Qadariyyah wamepindukia katika kuthibitisha utashi na matakwa ya mja mpaka wakafikia kusema kuwa amejitosheleza na Allaah na anaumba kila anachotaka.

Jabriyyah wamepindukia katika kuthibitisha utashi na matakwa ya Allaah mpaka hilo likawapelekea kupinga utashi na matakwa ya mja.

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wamekaa kati na kati. Wamesema kuwa kila kitu kinakuwa kwa Qadhwaa´ na Qadar ya Allaah kukiwemo matendo ya waja. Yameumbwa na Allaah na wakati huo huo ni matendo ya waja walioyafanya kwa khiyari na kupenda kwao wenyewe. Waja wana utashi na khiyari ya kufanya jambo lakini hata hivyo hayakujitosheleza na Allaah, kama wanavyosema Qadariyyah, na hawakutenzwa nguvu, kama wanavyosema Jabriyyah. Bali wanafanya mambo kwa khiyari na utashi wao msafi. Kwa ajili hiyo ndio maana wanalipwa thawabu kwa kutenda kheri na wanaadhibiwa kwa kutenda shari. Si kwa jengine ni kwa sababu wamefanya kwa khiyari na kwa kupenda kwao wenyewe. Lau wangelikuwa wametenzwa nguvu hawaadhibiwi. Ni vipi wataadhibiwa kwa mambo ambayo hawana kwayo khiyari wala utashi? Kwa ajili hiyo ndio maana Allaah (Jalla wa ´Alaa) hamchukulii mwendawazimu ambaye hana khiyari. Kadhalika hamchukulii

ambaye katenzwa nguvu kwa sababu hana khiyari. Vilevile hamchukulii mwenye kulala ambaye hana kufikiria na wala hana akili. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Kalamu imesimamishwa kutoka kwa watu watatu; mdogo mpaka abaleghe, mwendawazimu mpaka apate akili na mwenye kulala mpaka aamke."[48]**

Kwa nini? Kwa sababu watu hawa hawana utashi na matakwa. Kwa hiyo hawachukuliwi kwa muda ule ambao fahamu zao zimepotea na matakwa. Kuhusu yule ambaye ana utashi, matakwa na khiyari analipwa kwa kutenda jema na anaadhibiwa kwa kutenda maasi. Kwa sababu ametenda kwa khiyari na matakwa yake. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

**"Hakika wale walioamini na wakatenda mema." (02:277)**

Ameyanasibisha matendo kwao. Amesema (Ta´ala):

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا

**"Hakika wale waliokufuru." (02:06)**

Ameunasibisha ukafiri kwao kwa sababu ni kitendo walichokifanya kwa kutaka kwao. Amesema (Ta´ala):

وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَإِنَّ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ

**"Na yule atakayemwasi Allaah na Mtume Wake, basi hakika atapata Moto." (72:23)**

Ameyanasibisha maasi kwao kwa sababu ni kitendo chao.

[48] Ibn Maajah (2045), Ibn Hibbaan (143) na wengineo

Kwa mtazamo wa kitendo ni cha mja. Kwa mtazamo wa Qadar kimekadiriwa na Allaah (Jalla wa ´Alaa). Kwa hivyo inakuwa ni makadirio ya Allaah na wakati huo huo ni kitendo cha mja. Huku ndio kuoanisha baina ya maandiko. Dalili ya hilo maneno Yake (Ta´ala):

لِمَن شَاء مِنكُمْ أَن يَسْتَقِيمَ وَمَا تَشَاؤُونَ إِلَّا أَن يَشَاء اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**"Kwa yule miongoni mwenu anayetaka anyooke. Wala nyinyi hamtataka isipokuwa atake Allaah, Mola wa walimwengu." (81:28-29)**

Maneno Yake:

لِمَن شَاء مِنكُمْ

**"Kwa yule miongoni mwenu anayetaka anyooke."**

Hapa wanaraddiwa Jabriyyah ambao wanapinga mja kuwa na utashi. Ni dalili inayofahamisha kuwa mja ananyooka kwa kupenda kwake. Kisha akasema:

وَمَا تَشَاؤُونَ إِلَّا أَن يَشَاء اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**"Wala nyinyi hamtataka isipokuwa atake Allaah, Mola wa walimwengu."**

Hapa wanaraddiwa Qadariyyah ambao wanasema matakwa ya waja yamejitosheleza na kwamba mja anatenda kivyake. Aayah hii inaraddi mapote yote mawili na sambamba na hilo inathibitisha madhehebu ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Mema na maasi yote mawili ni kitendo cha mja na wakati huo huo ni Qadhwaa´ na Qadar ya Allaah. Allaah amewakadiria navyo na wao wameyafanya kwa kupenda na kutaka kwao. Kwa ajili hiyo mtu mwenye akili anaweza kufanya, anaweza kuacha, anaweza kuamka na kuswali, anaweza kutoa swadaqah na anaweza kupigana Jihaad katika njia ya Allaah. Kadhalika anaweza kuacha swalah, anaweza kuacha kuamrisha mema na kukataza maovu na anaweza kuacha kupigana Jihaad katika njia ya Allaah. Anaweza akayaacha yote haya kwa kupenda na kutaka kwake. Anaweza kufanya kama ambavyo vilevile anaweza kuacha. Anaenda kuzini, kunywa pombe na kula ribaa kwa khiyari yake mwenyewe. Anaweza kuacha kula ribaa, kuzini na

mambo mengine ya haramu. Anafanya yote haya kwa khiyari na kupenda kwake mwenyewe. Hakuna asiyejua haya.

## 61. Kujigonga kwa Jabriyyah

Jabriyyah hawatekelezi maneno haya waliyosema katika mambo yote. Lau kutakuwepo mtu ambaye atawafanyia uadui sawa iwe kwa kumpiga au kumuua mmoja wao, hawatoomba kulipiza kisasi? Kwa nini waombe kufanya hivo ilihali wao wanasema kuwa ametenzwa nguvu na hakufanya kwa khiyari yake? Huku ni kujigonga.

Jengine ni kuwa wao wanatafuta riziki na wanaoa. Iwapo kweli wametenzwa nguvu, kama wanavyodai, ni kwa nini basi wanafanya mambo haya na wanatafuta kupatikana kwa mambo yasiyokuwepo? Wao hawatendei kazi madhehebu haya machafu katika uhalisia wa maisha. Kwa ajili hiyo wanaomba kulipiza kisasi, wanaoa na wanatafuta riziki. Haya ni maneno batili. Hii ndio natija ya kutegemea fikira, akili mbovu, maneno au maoni ya watu pasi na kurejea katika Qur-aan na Sunnah.

## 62. Kuamini Qadhwaa´ na Qadar hakupingani na kufanya sababu

Kuamini Qadhwaa´ na Qadar na kufanya sababu ni mambo mawili yasiyopingana. Wewe unachotakiwa ni kuamini anayotaka Allaah huwa na asiyotaka hayawi. Lakini hata hivyo usiache kufanya sababu. Bali unatakiwa kutafuta riziki, kuoa, kufanya biashara na kuhangaika na kutafuta riziki. Usisemi kuwa wewe unategemea Qadhwaa´ na Qadar na kwamba ikiwa kitu kimeshaandikwa kwako basi kitakujia na kama hukuandikiwa nacho hakitokujia. Haya hayasemwi na mtu mwenye akili. Hata wanyama - kwa maumbile yao - wanatoka na kwenda kutafuta riziki. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi ´alayhi wa sallam):

**"Lau kweli mngelikuwa mnamtegemea Allaah ukweli wa kumtegemea, basi angalikuruzukuni kama anavyomruzuku ndege: inatoka asubuhi haina kitu na anarudi jioni tumbo limejaa."[49]**

Ndege haibaki kwenye chicha lake. Inaruka na kwenda kutafuta riziki.

Kwa hivyo hakuna mgongano kati ya kuamini Qadhwaa´ na Qadar na kufanya sababu. Wenye kusema hivi ni Jabriyyah.

Lakini pamoja na haya yote sababu haipwekeki katika kuleta natija. Msababishi ni Allaah (Jalla wa ´Alaa). Hii ni Radd kwa Qadariyyah. Hatupindukii katika kuthibitisha sababu kama walivyofanya Qadariyyah na wala hatupindukii katika kuikanusha kama walivyofanya Jabriyyah. Kufanya sababu ni jambo linalotakikana. Amesema (Ta´ala):

فَابْتَغُوا عِندَ اللَّهِ الرِّزْقَ

**"Basi tafuteni riziki kwa Allaah." (29:17)**

[49] at-Tirmidhiy (2344), Ibn Maajah (4164), Ahmad (01/30) na wengineo. Ni nzuri kwa mujibu wa at-Tirmidhiy

وَابْتَغُوا مِن فَضْلِ اللَّهِ

**"Tafuteni kutoka katika fadhila za Allaah." (62:10)**

Allaah ameamrisha swalah, swawm na kufanya mema mbalimbali. Haya ni katika kufanya sababu. Kadhalika amekataza sababu za shari kama kufuru, maasi na machafu.

Kuamini Qadhwaa´ na Qadar haina maana kwamba sasa unatakiwa kuacha kufanya sababu. Unatakiwa kuendelea kutafuta na wakati huo huo kuamini ya kwamba ikiwa Allaah amekuandikia jambo, basi litakujia. Hutojiwa na jambo ilihali umekaa tu. Ni lazima ufanye sababu. Kwa ajili hii amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Pupia lile lenye kukufaa na umtake msaada Allaah na wala usikate tamaa. Endapo utafikwa na jambo usisemi "lau ningefanya kadhaa ingelikuwa kadhaa na kadhaa". Badala yake unatakiwa kusema "Allaah ameshakadiria. Anafanya alitakalo.""[50]**

Wewe unachotakiwa ni kufanya sababu. Ukifikia natija himdi zote zinamrudilia Allaah, na usipofikia natija mshukuru Allaah na ujisalimishe ya kwamba Allaah alikuwa hakukuandikia jambo hilo. Hadiyth hii iko wazi katika kufanya sababu na kwamba kuamini Qadhwaa´ na Qadar haina maana mtu aache kufanya sababu au kwamba kufanya sababu kunatosheleza katika kuleta natija ya mambo kama wanavyosema Mu´tazilah. Mja hufanya sababu - mema au maasi - na natija inakuwa mikononi mwa Allaah. Yeye ndiye ambaye huzalisha natija na msababishaji wa sababu zinazofanywa.

[50] Muslim (34) na (2667)

## 63. Baadhi ya faida za kuamini Qadhwaa´ na Qadar

Tano: Kuhusu faida ya kuamini Qadhwaa´na Qadar. Kuamini Qadhwaa´ na Qadar kuna faida nyingi:

Ya kwanza: Faida kubwa kuliko zote ni kukamilisha nguzo za imani. Anayepinga Qadhwaa´ na Qadar hakukamilisha nguzo za imani ambazo amefasiri Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) mtu kuziamini:

"Kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake na kuamini Qadar kheri na shari yake."

Ya pili: Mja anakuwa si mwenye kujali dhana na woga. Anakuwa ni mwenye kwenda zake na huku akitambua kuwa kile alichomkadiria Allaah kitakuja tu, ni mamoja akae au asikae. Kwa ajili hii pindi wanafiki siku ya Uhud waliposema:

الَّذِينَ قَالُوا لِإِخْوَانِهِمْ وَقَعَدُوا لَوْ أَطَاعُونَا مَا قُتِلُوا ۗ قُلْ فَادْرَءُوا عَنْ أَنفُسِكُمُ الْمَوْتَ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ

**"Wale waliowaambia ndugu zao nao wakakaa [hawakwenda vitani]: "Lau wangelitutii basi wasingeliuawa." Sema: "Basi ziondoleeni nafsi zenu mauti mkiwa ni wakweli." (03:168)**

Kukaa nyumbani hakumzuii mtu kutokana na kufa kama ambavyo vilevile kutoka kwenda katika Jihaad hakumfanyi mtu akafa au kuleta kifo ikiwa Allaah hakukikadiria. Ni kweli kwamba ni sababu, lakini ikiwa Allaah hakukikadiria hakina athari na wala hakileti natija yoyote. Ni wangapi wametoka kwenda vitani na wamerudi wakiwa salama salimina. Khaalid bin Waliyd (Radhiya Allaahu ´anh) yalipomfika mauti alisema:

"Mwilini mwangu hakuna shibri hata moja isipokuwa kuna kovu la kipigo."[51]

[51] Taariykh Dimashq (16/273) ya Ibn ´Asaakir

Alikuwa ni mtu anatamani sana kufa shahidi. Alishuhudia vita vikubwa na akatamani sana auawe katika njia ya Allaah. Lakini hata hivyo Allaah hakumwandikia hivo.

Kuamini Qadhwaa´ na Qadar kunamfanya mtu kuwa na ushujaa, kutangulia na kumtegemea Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Kukaa hakumfidishi mtu kitu. Amesema (Ta´ala):

قُل لَّوْ كُنتُمْ فِي بُيُوتِكُمْ لَبَرَزَ الَّذِينَ كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقَتْلُ إِلَىٰ مَضَاجِعِهِمْ

**"Sema: "Lau mngelikuwa majumbani mwenu, bila shaka wangejitokeza wale walioandikiwa kuuwawa kwenye mahali pa kuangukia wafe." (03:15)**

أَيْنَمَا تَكُونُوا يُدْرِككُّمُ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّشَيَّدَةٍ

**"Popote mtakapokuwa yatakufikieni mauti, japo mkiwa katika ngome zilizo na nguvu." (04:78)**

Qadhwaa´ ni lazima itekelezeke na itokee.

Kwa hivyo hakuna faida yoyote ya mtu kukaa na kuacha kufanya sababu za faida na kuepuka sababu mbaya. Haya yanamfanya mtu kuwa na ujasiri na ushujaa wa kumuamini Allaah (´Azza wa Jall). Vilevile kunamfanya mtu asiwe na mashaka, wasiwasi na kuamini mikosi inayowapata watu wengi. Kunamuondoshea mtu kuwa na wasiwasi. Kwa ajili watu wa imani hawakuwa wakichelewa katika kutafuta mambo yaliyo na kheri na faida. Kwa sababu walikuwa ni wenye kuamini Qadhwaa´ na Qadar. Hawakuwa ni wenye kuogopa kufa na kuuawa. Ikiwa kifo kimeshaandikwa kwako kitakujia tu hata kama hutokiendea, na kama hujaandikiwa hakitokufika hata kama utakuwa katika khatari ilio kubwa.

Ya tatu: Mtu havunjiki moyo pindi anapofikwa na tatizo. Kwa sababu anaamini kuwa limepitika kwa Qadhwaa´ na Qadar ya Allaah. Hili linasahilisha kukabiliana na matatizo. Hivyo mtu anakuwa si mwenye kukata tamaa hajipigi kwenye mashavu, hapasui nguo na haiti kwa wito wa kipindi

cha washirikina. Kinyume chake anakuwa na subira na kutarajia malipo kutoka kwa Allaah. Amesema (Ta´ala):

وَبَشِّرِ الصَّابِرِينَ الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُم مُّصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ أُولَٰئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ ۖ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُهْتَدُونَ

**"Wabashirie wenye kusubiri - wale ambao unapowafika msiba husema: "Hakika sisi ni wa Allaah na hakika sisi Kwake ni wenye kurejea." - [wafikishie ya kwamba] hao zitakuwa juu yao barakah kutoka kwa Mola wao na rahmah; na hao ndio wenye kuongoka." (02:155-157)**

Ni wale ambao wanapofikwa na matatizo hawazilaumu nafsi zao na kusema ni kwa sababu hii na ile. Wanaridhia Qadhwaa´ na Qadar ya Allaah na kwamba tatizo hilo lilikuwa lenye kutokea kwa hali yoyote ile aliyokuwa Allaah kishakadiria. Kilichokadiriwa kinatokea kwa idhini ya Allaah. Wanasema:

إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

**"Hakika sisi ni wa Allaah na hakika sisi Kwake ni wenye kurejea."**

Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**Endapo utafikwa na jambo usisemi "lau ningefanya kadhaa ingelikuwa kadhaa na kadhaa". Badala yake unatakiwa kusema "Allaah ameshakadiria. Anafanya alitakalo.""[52]**

Haya yanamsahilishia mtu matatizo yake na badala yake anaridhia na kujisalimisha na Qadhwaa´ na Qadar ya Allaah. Hizi ni faida tatu zinazopatikana kwa kuamini Qadhwaa´ na Qadar:

Kwanza: Kukamilisha nguzo za imani.

Pili: Kuamini Qadhwaa´ na Qadar kunamfanya mtu kuwa na nguvu, ushujaa na kuwa msitari wa mbele katika kufanya mambo ya kheri.

[52] Muslim (34) na (2667)

Tatu: Kuamini Qadhwaa´ na Qadar kunamuwepesishia muislamu yale matatizo yanayomfika.

Kuhusiana na ambaye haamini Qadhwaa´ na Qadar utamuona ni mwenye kuvunjika moyo, kukasirika na hufika na yakumfika.

## 64. Mwenye kujilipua na kujiua haamini Qadhwaa´ na Qadar

Leo hii mnasikia sana yale yanayoitwa "kujilipua/kujiua" na kwamba ni jambo limeenea kati ya watu wenye dini zengine. Sababu yake ni nini? Sababu yake ni kutoamini Qadhwaa´ na Qadar. Pindi mmoja wao anapohisi dhiki anajilipua. Kwa sababu haamini Qadhwaa na Qadar. Hasemi kuwa ni jambo alilokadiriwa na kuandikiwa na akaamini kuwa faraja iko karibu na akamdhania Allaah vyema:

فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا

**"Hakika pamoja na kila gumu kuna mepesi." (94:05)**

أَلَا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ قَرِيبٌ

**"Tanabahi! Hakika nusura ya Allaah iko karibu." (02:214)**

Ambaye anajilipua na kujiua haamini Qadhwaa´ na Qadar. Hawezi kustahamili matatizo na misiba.

## 65. Utafiti juu ya Qadhwaa´ na Qadar IV

Tano: Kuhusu mambo yanayopelekea madhehebu ya Jabriyyah na Qadariyyah. Yanapelekea katika mambo ya khatari yafuatayo:

La kwanza: Madhehebu ya Qadariyyah yanapelekea katika kuthibitisha waungu wengi pamoja na Allaah. Hii ni shirki katika uola. Kwa ajili hii ndio maana wameitwa kuwa ni waabudu moto wa Ummah huu.

La pili: Madhehebu ya Jabriyyah yanapelekea kumsifu Allaah kwa dhuluma na kwamba anawaadhibu waja kwa kitu ambacho hawakufanya wao bali kimefanya Allaah. Allaah anawaadhibu kwa kitu ambacho wao hawakufanya. Wao wanaendeshwa tu pasi na khiyari wala kutaka kwao. Huku ni kumsifu Allaah (Jalla wa ´Alaa) kwa dhuluma ya kwamba anawaadhibu waja kwa kitu ambacho hawakufanya wao bali kimefanya Yeye Mwenyewe. Uharibifu wa madhehebu haya batili haufichikani. Allaah (´Azza wa Jall) amesema:

وَلَا تُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ

**"Na wala hamtalipwa isipokuwa yale mliyokuwa mkiyatenda." (36:54)**

Amefungamanisha adhabu kwa kufuru, maasi na madhambi kama ambavyo vilevile amefungamanisha utiifu kwa mambo ya utiifu na ya kheri. Allaah hamdhulumu yeyote.

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ۖ وَإِن تَكُ حَسَنَةً يُضَاعِفْهَا

**"Hakika Allaah hadhulumu [kiumbe yeyote] uzito wa atomu na ikiwa ni [ʻamali] njema huizidisha." (04:40)**

Huu ndio uadilifu Wake (Subhaanahu wa Ta´ala). Miongoni mwa uadilifu Wake ni kuwa hayaongezi madhambi. Analipa kwa mfano wake. Katika fadhila Zake ni kuwa analiongeza jema moja kwa kupenda Kwake Mwenyewe (Subhaanahu wa Ta´ala).

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ۖ وَإِن تَكُ حَسَنَةً يُضَاعِفْهَا

**"Hakika Allaah hadhulumu [kiumbe yeyote] uzito wa atomu na ikiwa ni [ʻamali] njema huizidisha."**

Huku kuongezewa ni fadhila kutoka kwa Allaah mpaka kufikia kumi mfano wake mpaka kufikia mia saba na zaidi ya hivyo. Kuhusu maovu Allaah analipa mfano wake na hazidishi juu yake. Haya ni kutokana na uadilifu Wake (Subhaanahu wa Ta´ala). Lakini Jabriyyah wanamsifu Allaah kwa dhuluma ya kwamba anawaadhibu waja kwa matendo Aliyofanya Mwenyewe. Wanasema kuwa wao hawakufanya kitu wanapelekwa kama chombo na kama upepo hewani. Haya ni madhehebu batili.

La tatu: Madhehebu yao yanapelekea kuacha kufanya sababu na mtu akasema kuwa midhali Ameshakadiria na kupanga basi mimi nakaa na nilichokadiriwa kitanijia.

La nne: Madhehebu ya Mu´tazilah, kama tulivyotangulia kusema, yanapelekea katika kushirikisha katika uola.

La tano: Madhehebu yao yanapelekea katika madhara makubwa ambayo ni kumfanya Allaah (´Azza wa Jall) kutoweza na kwamba kunapitika katika ufalme Wake kile asichokitaka na kukipenda. Huku ni kumsifu Allaah (´Azza wa Jall) kutokuwa na uwezo. Hii ni khatari kubwa.

Madhehebu yote mawili ni batilifu na yanapelekea katika madhara makubwa. Kuhusu madhehebu ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah yako kati kwa kati na adilifu katika mambo yote.

## 66. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah - watu wa kati na kati siku zote

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah siku zote wanakuwa kati kwa kati. Kwa ajili hii ndio maana wanasema kuwa Ummah huu uko kati na kati baina ya nyumati zingine na Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wako kati na kati baina ya mapote potevu. Inahusiana na haya na mengineyo. Wanamthibitishia Allaah matendo, utashi, matakwa yake, aliyopanga na kukadiria na wakati huo huo wanawathibitishia viumbe matendo, utashi na matakwa yao. Wanafanya hivo kwa mujibu wa Qur-aan na Sunnah. Hawapingi Qadhwaa´ na Qadar, kama wanavofanya Mu´tazilah, na wala hawapetuki mpaka katika kuthibitisha Qadhwaa´ na Qadar na kumpokonya mja utashi na matakwa yake, kama wanavofanya Jabriyyah.

## 67. Utafiti juu ya Qadhwaa´ na Qadar V

Kuna masuala: Wale wanaopinga Qadhwaa´ na Qadar wahukumiwe ukafiri? Wanachuoni walipambanua suala hili na wakasema ambaye atapinga ngazi ya kwanza - ambayo ni ya elimu - na akasema kuwa Allaah hayajui mambo isipokuwa baada ya kutokea kwake kwa njia ya kwamba pale yanapotokea ndio huyajua, mtu huyu anakufuru. Kwa sababu amepinga elimu ya Allaah (Jalla wa ´Alaa). Lakini hata hivyo wanasema kuwa wale wenye kupinga elimu wametokomea. Hivi ndivyo alivyosema Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (Rahimahu Allaah) katika "al-Waasitwiyyah"[53]. Mu´tazilah waliobaki wanathibitisha elimu ya Allaah (´Azza wa Jall) ya milele. Lakini hata hivyo wanapinga Qadar. Hivyo wao ni wapotevu. Hawafikii kiwango cha ukafiri. Kwa sababu watu hawa wanathibitisha elimu ya Allaah (´Azza wa Jall) na kuandikwa kwenye Ubao uliohifadhiwa. Wanachopinga ni utashi na matakwa. Bi maana wamethibitisha elimu na uandishi na wakachupa mipaka katika matendo ya waja na wakasema kuwa yanatokea pasi na utashi na matakwa ya Allaah (Jalla wa ´Alaa). Haya bado mpaka sasa yapo na yanaendelea kwa Mu´tazilah na yale mapote mengine yaliyochukua madhehebu yao.

Huu ni ufupisho juu ya suala hili likubwa. Lakini inatosheleza kwa muislamu kuijua misingi hii na kusimama kwayo na wala asivuke mipaka katika kutafiti masuala ya Qadhwaa´ na Qadar. Asijifungulie kwenye nafsi yake mlango wa kuchukulia wepesi. Kwa kuwa hatofikia natija yoyote. Kwa kuwa Qadhwaa´ na Qadar ni siri ya Allaah (Jalla wa ´Alaa) kwa waja Wake. Huwezi kufikia natija yoyote kwa kuchukulia wepesi. Ni juu yako kutembea pamoja na dalili za Qur-aan na Sunnah na uthibitishe Qadhwaa´ na Qadar na utambue dalili zake na hukumu ya mwenye kuyapinga.

[53] Tazama "al-´Aqiydah al-Waasitwiyyah", uk. 164 kwa sharh ya mwandishi (Hafidhwahu Allaah)

## 68. Kutumia Qadhwaa´ na Qadar kama hoja?

Kuna masuala mengine yaliyotajwa na wanachuoni. Masuala yanayohusiana na kuitumia Qadar kama hoja. Hilo ni kwa sababu Muusa (´alayhis-Salaam) alipokutana na baba wa watu ambaye ni Aadam (´alayhis-Salaam) kwa Ummah wake alimwambia:

"Ni kwa nini ulisababisha sisi na wewe tukatolewa Peponi?" Akasema: "Wewe ni Muusa msemezwa wa Allaah. Ni kwa muda kiasi gani ulikutana haya yameandikwa kwangu kwenye Ubao uliohifadhiwa?" Muusa akasema maneno yakiwa na maana ifuatayo: "Allaah aliyaandika hayo kwenye Ubao uliohifadhiwa."

Jabriyyah wamelichukua hili na wakalitumia kama hoja ya kwamba Aadam ametumia kama hoja juu ya Muusa ya kwamba yaliyompitikia sio kwa khiyari yake. Wanasema kuwa ni kitendo cha Allaah (Jalla wa ´Alaa). Hawakufahamu Hadiyth. Muusa hakumlaumu Aadam juu ya Qadhwaa´ na Qadar. Alimlaumu kwa ajili ya kutolewa Peponi pindi aliposema:

"Ni kwa nini ulisababisha sisi na wewe tukatolewa Peponi?" Aadam akatumia hoja dhidi yake kwa Qadhwaa´ na Qadar. Kutumia hoja Qadhwaa´ na Qadar katika misiba ni jambo linajuzu. Ni jambo linamsahilishia mtu na anakuwa sio mwenye kuvunjika moyo wala kukasirika. Muusa hakumuuliza kuhusu Qadhwaa´ na Qadar. Hakumwambia:

"Ni kwa nini Allaah alikukadiria hivi?"

Bali alisema:

"Ni kwa nini ulisababisha tukatolewa?"

Alimuuliza kutokana na msiba uliopelekea katika yale yaliyomtokea Aadam kula kwenye mti. Muusa hakumlaumu juu ya dhambi. Hakumwambia:

"Ni kwa nini ulikula kwenye mti?"

Kwa sababu alitubu kutokana na dhambi yake na Allaah akamsamehe. Mwenye kutubia halaumiwi kwa yaliyomtokea baada ya kutubia. Alimlaumu kwa sababu ya kutolewa Peponi. Huu ni msiba uliowafika dhuriya ya Aadam.

Aadam alitumia hoja dhidi ya Muusa (´alayhimaas-Salaam) kwa Qadhwaa´ na Qadar. Kutumia hoja kwa Qadhwaa´ na Qadar katika misiba ni jambo limewekwa katika Shari´ah. Kwa ajili hii ndio maana Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

**"Utapofikwa na jambo usisemi "lau ningefanya kadhaa ingelikuwa kadhaa na kadhaa" badala yake sema "amekadiria Allaah na alitakalo huwa."**

Qadhwaa´ na Qadar inatumiwa kama hoja katika misiba. Kwa sababu wewe huna khiyari katika hayo. Allaah ndiye amefanya hivo. Kuhusu maasi ni dhambi yako wewe. Hivyo usitumie hoja kwa Qadhwaa´ na Qadar. Kwa ajili hii wanachuoni wamesema:

"Qadhwaa´ na Qadar inatumiwa kama hoja katika misiba na haitumiwi kama hoja katika mambo ya aibu."[54]

Huu ndio upambanuzi katika masuala haya makubwa.

***Yakinisha makadirio yaliyopangwa -*** Kwamba ni kutoka kwa Allaah (Jalla wa ´Alaa).

***Yakinisha... -*** Bi maana itakidi.

***hakika ndio nguzo ya dini... -*** Ni nguzo. Kuiamini ni nguzo ya sita katika nguzo za imani.

***... nguzo ya dini... -*** Kwa sababu dini imegawanyika katika daraja tatu:

Ya kwanza: Daraja ya nguzo za Uislamu tano.

Ya pili: Daraja ya imani kwa nguzo zake sita.

[54] Majmuu´-ul-Fataawaa (08/454)

Ya tatu: Daraja ya *Ihsaan* kwa nguzo yake moja.

***... dini imeenea -*** Ni sehemu pana. Dini ni pana na ni yenye kuenea.

## 69. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya kuamini siku ya Mwisho

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

29- *Usimpinge kwa ujinga Nakiyr na Munkar*

*wala [usipinge] hodhi na mizani - hakika wewe unanasihiwa*

**MAELEZO**

Shairi hili na ya baada yake ni kuhusu kuamini juu ya siku ya Mwisho. Nayo ni siku inayokuwa baada ya dunia. Ndio siku ya malipo na hesabu. Kuiamini ni moja katika nguzo za imani sita ambayo ilikuja katika Hadiyth ya ´Umar (Radhiya Allaahu ´anh) katika kisa pindi Jibriyl (´alayhis-Salaam) alipomjia Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akiwa pamoja na Maswahabah zake akimuuliza kuhusu Uislamu, imani, *Ihsaan* na Qiyaamah. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akajibu kwamba:

**"Imani ni kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, siku ya Mwisho na kuamini Qadar kheri na shari yake."**

Nguzo hizi sita wakati fulani zinatajwa zote kwa pamoja katika Qur-aan na wakati mwingine zinatajwa baadhi yake. Mara nyingi kumuamini Allaah na siku ya Mwisho vinatajwa pamoja. Amesema (Ta´ala):

مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

**"Mwenye kumuamini Allaah na siku ya Mwisho." (02:62)**

يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

**"Waliomwamini Allaah na siku ya Mwisho." (09:44)**

Wakati mwingine yanatajwa yote kwa pamoja. Amesema (Ta´ala):

لَّيْسَ الْبِرَّ أَن تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَٰكِنَّ الْبِرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ

**"Si wema pekee kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi, lakini wema khasa ni ambaye anamuamini Allaah na siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii." (02:177)**

آمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِن رَّبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ ۚ كُلٌّ آمَنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ

**"Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake na waumini - wote wamemwamini Allaah na Malaika Wake na Vitabu Vyake na Mitume Wake." (02:285)**

## 70. Radd kwa makafiri wenye kupinga kufufuliwa

Kuamini siku ya Mwisho ni nguzo moja wapo ya imani. Ambaye ataikanusha amekufuru. Mwenye kusema kuwa hakuna kufufuliwa na kwamba kuna maisha ya dunia peke yake, huyu ni kafiri kwa kuwa amemkadhibisha Allaah, Mtume Wake, maafikiano ya waislamu na jambo ambalo linajulikana katika Uislamu fika. Hakuna shaka juu ya ukafiri wa anayepinga kufufuliwa. Amesema (Ta´ala):

زَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَن لَّن يُبْعَثُوا ۚ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ ۚ وَذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

**"Waliokufuru wamedai kwamba hawatofufuliwa. Sema: "Bali hapana! Naapa kwa Mola wangu, bila shaka mtafufuliwa kisha mtajulishwa kwa yale mliyoyatenda - na hayo kwa Allaah ni mepesi."" (64:07)**

Allaah alimuamrisha Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aape kwa Mola Wake ya kwamba atawafufua. Maneno Yake:

Madai maana yake ni uongo. Bi maana wamesema uongo katika maneno yao haya. Amesema (Ta´ala):

وَقَالُوا إِنْ هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوثِينَ

**"Walisema: "Haya si chochote isipokuwa ni uhai wetu wa dunia tu na wala sisi hatutofufuliwa."" (06:29)**

وَقَالُوا مَا هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا يُهْلِكُنَا إِلَّا الدَّهْرُ

**"Wakasema: "Huu si chochote isipokuwa ni uhai wetu wa dunia, tunakufa na tunahuika, na hakuna cha kutuangamiza isipokuwa dahari."" (45:24)**

أَيَعِدُكُمْ أَنَّكُمْ إِذَا مِتُّمْ وَكُنتُمْ تُرَابًا وَعِظَامًا أَنَّكُم مُّخْرَجُونَ هَيْهَاتَ هَيْهَاتَ لِمَا تُوعَدُونَ إِنْ هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوثِينَ

**"Je, anakuahidini kwamba nyinyi mtakapokufa mkawa mchanga na mifupa kuwa hakika mtatolewa? Mbali kabisa, mbali kabisa! Hayo mnayoahidiwa.**

**Hakuna lolote isipokuwa tu uhai wetu wa hapa duniani tunakufa na tunahuika na wala sisi hatutofufuliwa." (23:35-37)**

Hivi ndivyo walivyokuwa wakisema makafiri tangu hapo mwanzo hadi sasa ambapo wanapinga kufufuliwa. Hawana hoja yoyote. Kinachowashangaza ni vipi watu watakufa wawe udongo halafu wafufuliwe. Wanasema kuwa ni kitu kisichowezekana kabisa:

قَالَ مَن يُحْيِي الْعِظَامَ وَهِيَ رَمِيمٌ

**"Akasema: "Ni nani atakayehuisha mifupa hii na hali imeshasagika na kuwa kama vumbi."" (36:78)**

Ametakasika Allaah. Hapo kabla asli ni kwamba hawakuwepo na baada ya hapo ndipo Allaah (Jalla wa ´Alaa) akawaumba. Ambaye aliwaumba mara ya kwanza ana haki zaidi ya kuwarudisha:

وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلْقَهُ ۖ قَالَ مَن يُحْيِي الْعِظَامَ وَهِيَ رَمِيمٌ قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ

**"Akatupigia mfano akasahau kuumbwa kwake; akasema: "Ni nani atakayehuisha mifupa hii na hali imeshasagika na kuwa kama vumbi." Sema: "Ataihuisha Yule aliyeianzisha mara ya kwanza Naye ni mjuzi wa kila [namna ya] kuumba."" (36:78-79)**

Ndani ya Qur-aan kumejaa Radd juu ya ambaye anapinga kufufuliwa.

Jengine ni kuwa lau kusingekuwa kufufuliwa na kulipwa juu ya matendo, kuumbwa kwa viumbe ingelikuwa ni mchezo. Vipi atawaumba na wafanye ima matendo mema au matendo ya kikafiri kisha wafariki na kuachwa hivi hivi? Hili halistahiki juu ya uadilifu wa Allaah (Jalla wa ´Alaa):

أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ فَتَعَالَى اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ ۖ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ

**"Je, mlidhania kwamba Sisi tulikuumbeni bila kusudio na kwamba nyinyi Kwetu hamtorejeshwa?" Ametukuka Allaah mfalme wa haki [ambaye] hapana mungu wa haki ila Yeye. Mola wa 'Arshi tukufu."" (23:115-116)**

Allaah ametakasika kutokamana na hili. Ni lazima kwa Allaah (Jalla wa ´Alaa) awafufue watu na awapambanue waumini kutokamana na makafiri na amlipe muumini kwa imani yake na kafiri kwa ukafiri wake:

أَمْ نَجْعَلُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ كَالْمُفْسِدِينَ فِي الْأَرْضِ أَمْ نَجْعَلُ الْمُتَّقِينَ كَالْفُجَّارِ

**"Je, Tuwafanye wale walioamini na wakatenda mema kuwa sawa kama wenye kueneza ufisadi katika ardhi au Tuwafanye wachaji Allaah sawa na waovu?" (38:28)**

Hivi kweli wote wafe na wasifufuliwe na wala wasilipwe juu ya matendo yao? Haiwezekani kabisa.

Isitoshe Allaah amewatisha makafiri, washirikina na watenda maovu ya kwamba [ipo siku] watarejea kwa Mola Wao ili awafanyie hesabu na kuwalipa. Ni jambo linalofahamisha kuwa kufufuliwa ni jambo lazima litokee na hakuna njia ya kulikwepa. Dunia ni pahali pa kufanya matendo na Aakhirah ni pahali pa malipo. Hii ni hekima ya Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).

## 71. Maana ya kuamini siku ya Mwisho

Imani ya kuamini siku ya Mwisho ina maana ya kuamini yale yote yatayokuwa baada ya kufa. Kuanzia maswali watayohoji Malaika wawili, adhabu au neema za ndani ya kaburi, kufufuliwa kutoka ndani ya makaburi, kusimama kwenye kiwanja cha kukusanyika na yatayopitika baada ya hapo. Kumethibiti dalili nyingi kuhusu hayo kutoka katika Qur-aan na Sunnah. Hivyo ni wajibu kuyaamini.

Kuamini siku ya Mwisho kunaingia katika kuamini mambo yaliyofichikana. Kuamini mambo yaliyofichikana ni moja katika nguzo za imani. Bali ndio imani yenyewe. Inahusiana na kumuamini Allaah kwa majina na sifa Zake. Haya ni kuamini mambo yaliyofichikana. Kwa sababu sisi hatujamuona Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).

Kuwaamini Malaika ni katika kuamini mambo yaliyofichikana. Kuamini majini na mashaytwaan ni katika kuamini mambo yaliyofichikana. Kuamini mambo aliyoelezea Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika mambo yatayopitika katika zama za mwisho ni katika kuamini mambo yaliyofichikana. Kuamini mambo yaliyowapitikia watu waliokuwa hapo kabla - japo hatukuyaona - lakini hata hivyo ni katika kuamini mambo yaliyofichikana. Mambo yaliyofichikana yanahusiana ima na mambo yaliyopita au yaliyoko huko mbele. Ni wajibu kuyaamini. Kwa ajili hii amesema (Subhaanahu wa Ta´ala) mwanzoni mwa Suurah "al-Baqarah":

الم ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ ۛ فِيهِ ۛ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْغَيْبِ وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ

**"Alif Laam Miym. Hiki ni Kitabu kisicho na shaka ndani yake ni mwongozo kwa wenye kumcha Allaah [ambao] huamini ghaibu na husimamisha swalah na katika vile Tulivyowaruzuku hutoa." (02:01-03)**

Ameanza kwa kuamini mambo yaliyofichikana.

Kwa hivyo kitendo cha kukanusha kufufuliwa kinapelekea kukanusha kumuamini Allaah (Jalla wa ´Alaa), Malaika na yale yote yasiyoonekana hapa

duniani. Haya ndio maoni ya watu wa mazingira, wakanamungu na washirikina ambao wanakanusha mambo yenye kufichikana.

Kwa hivyo imani ya kumuamini Allaah kunaingia ndani yake yale yote yatayopitika baada ya kufa. Jambo la kwanza katika hayo ni kuwa pale ambapo maiti atawekwa ndani ya kaburi na kufukiwa udongo na watu wakamuacha, husikia mlio wa viatu vyao. Hujiwa na Malaika wawili ambao wanamrudishia roho yake kwenye kiwiliwili chake. Wanamkaza na kumuuliza: "Ni nani Mola Wako? Ni ipi dini yako? Ni nani Mtume Wako?"[55]

Ni maswali matatu. Akijibu majibu sahihi huokoka, kufuzu na kufaulu, na asipoweza kujibu amekula khasara na amepoteza nguvu zake.

[55] al-Bukhaariy (1338) na (1374) na Muslim (70) na (287)

## 72. Nasaha za Imaam Ibn Abiy Daawuud

Amesema mwandishi (Rahimahu Allaah):

*Usimpinge kwa ujinga Nakiyr na Munkar*

Bi maana usipinge kitu usichokijua. Sio kila usichokijua unakipinga. Unachotakiwa ni kuamini yale yaliyosihi na kuthibiti hata kama hutoyajua na kuyadiriki. Amesema (Ta´ala):

بَلْ كَذَّبُوا بِمَا لَمْ يُحِيطُوا بِعِلْمِهِ وَلَمَّا يَأْتِهِمْ تَأْوِيلُهُ ۚ كَذَٰلِكَ كَذَّبَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ

**"Bali wamekadhibisha yale wasiyoyaelewa vyema elimu yake na wala haujawafikia uhakika wake halisi." (10:39)**

Lililo la wajibu ni muumini aamini yale yaliyosihi kutoka kwa Allaah na Mtume Wake hata kama hakuyajua na kuyafikiria. Hakika jambo hilo lina wakati wake litatokea:

لِّكُلِّ نَبَإٍ مُّسْتَقَرٌّ ۚ وَسَوْفَ تَعْلَمُونَ

**"Kwa kila habari ina wakati wake maalumu na mtakuja kujua." (06:67)**

Maelezo na simulizi mnazoelezwa kila kitu kina wakati wake. Utapofika wakati wake kitadhihiri. Wajibu wetu ni sisi kukiamini. Kwa sababu ni maneno ya Allaah (Jalla wa ´Alaa) ambayo:

لَّا يَأْتِيهِ الْبَاطِلُ مِن بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ

**"Haitokifikia ubatili mbele yake na wala nyuma yake." (41:42)**

Vilevile ni maneno ya Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambaye hazungumzi kwa matamanio yake:

وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ

**"Na wala hatamki kwa matamanio yake. Hayo ayasemayo si chochote isipokuwa ni *Wahy* unaofunuliwa kwake." (53:03-04)**

Tusitegemee akili zetu. Inapokuja katika mambo yaliyofichikana tunatakiwa tutegemee *Wahy* wenye kuteremshwa na wala tusiingize akili na fikira zetu.

Mambo ya ndani ya kaburi yanahusiana na mambo ya Aakhirah. Endapo tutamfukua mtu baada ya kuwekwa ndani ya kaburi lake tutamkuta kama alivyowekwa. Lakini yuko katika hukumu za ulimwengu mwingine na yale yanayompitikia hatuyaoni na wala hatuwezi kuyahisi. Si kwa jengine ni kwa sababu yuko katika ulimwengu mwingine uliyofichikana kwetu.

***Nakiyr na Munkar -*** Haya ni majina ya Malaika wawili wanaomjia maiti pale tu anapofukiwa. Roho yake inarudishwa kiwiliwilini mwake halafu wanamkaza hai. Inahusiana na uhai wa ndani ya kaburi na si kama mfano wa uhai wa ardhini. Ni uhai wa Aakhirah na mwingine asioutambua yeyote isipokuwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Wanaitwa hivi kama ilivyokuja katika Hadiyth isiokuwa na neno katika mlolongo wa wapokezi wake[56]. Ni majina yaliyothibiti. Kwa sababu muonekano wa Malaika wawili hawa ni wenye kutisha na mtu atawakana na kufazaika nao. Watamjia kwa sura ambayo alikuwa haijui katika uhai wake. Hii ndio sababu wameitwa Munkar na Nakiyr. Hapa kuna Radd kwa wale wenye kupinga majina haya na kusema kuwa ni kuwatukana Malaika. Tunasema kuwa sio kuwatukana Malaika. Hili ni kwa sababu yule watayemjia atawakana. Ndio maana wakaitwa Munkar na Nakiyr.

***hakika wewe unanasihiwa -*** Bi maana unanasihiwa usiyapinge mambo haya. Dini ni kupeana nasiha. Hivi ndivyo alivyosema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

[56] at-Tirmidhiy (1071) na at-Twabariy katika "al-Mu´jam al-Awsatw" (05/44). at-Tirmidhiy amesema:

"Ni nzuri (Hasan) na geni."

**"Dini ni kupeana nasaha." Tukasema: "Ni kwa nani?" Akasema: "Ni kwa Allaah, Kitabu Chake, Mtume Wake, viongozi wa waislamu na kwa watu wa kawaida."[57]**

Mwandishi (Rahimahu Allaah) anasema kwamba anakunasihi usipinge yaliyothibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), katika Qur-aan na katika Sunnah. Mu´tazilah na wapotevu ambao wanategemea akili na fikira zao wameyapinga hayo. Tahadhari na mwenendo wao na fuata maandiko. Amini yaliyokuja katika maandiko sahihi. Huku kunaingia katika kumuamini Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).

[57] Muslim (95) na (55)

## 73. Uhalisia wa hali ndani ya kaburi

Mambo yanayompitikia maiti ndani ya kaburi ambayo ni wajibu kwa mtu kuyaamini ni yafuatayo:

**La kwanza:** Kujiwa na Munkar na Nakiyr. Malaika hawa wawili wanamjia maiti. Ikiwa mtu atauliza ni vipi wanamjia ndani ya kaburi ilihali sisi hatuwaoni? Jibu ni kuwa Allaah juu ya kila kitu ni muweza. Hakika umefichikiwa vitu vingi. Malaika wawili hawa wanamjia ilihali wewe huwaoni. Hivi wewe unaiona roho yako inayoingia kwenye mwili wako? Wewe unaona kila kitu? Kuna vitu vingi usivyoviona. Je, wewe unaiona akili yako inayokupambanua wewe na vyengine? Sio kila usichokiona si sahihi. Haya ni maneno ya watu wa mazingira. Kuhusu watu wa imani; imani yao inawawezesha kuamini yale yote yaliyopokelewa kwa mapokezi sahihi na hawayaingizii ndani yake akili zao. Malaika hao wawili wanamjia na kumkaza na kumtamkisha: "Ni nani Mola Wako? Ni ipi dini yako? Ni nani Mtume Wako?" Muumini atajibu: "Mola Wangu ni Allaah, dini yangu ni Uislamu na Mtume wangu ni Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)." Anadi mwenye kunadi: "Amesema kweli mja Wangu, muandalieni makazi Peponi, mpanulieni kaburi lake upeo wa macho yake na mfungulieni mlango Peponi." Baada ya hapo ajiwe na harufu na manukato yake na aone makazi yake Peponi. Aseme: "Ee Mola! Lete Qiyaamah ili niweze kurejea kwa familia na mali yangu."[58]

Pepo yake igeuke kuwa ni bustani miongoni mwa mabustani ya Peponi. [Tunayaamini] hata kama hatuyaoni. Kuna baadhi ambao wanaweza kuyaona ambao Allaah amependa kuwaonyesha nayo. Lakini hata hivyo sio jambo la lazima.

Kuhusu mnafiki na mwenye mashaka - ambaye aliishi juu ya shirki duniani - atakufa juu ya shaka. Atapoulizwa: "Ni nani Mola Wako?" Atasema: "Sijui." Atapoulizwa: "Ni ipi dini yako?" Atasema: "Sijui. Niliwasikia watu wanasema

[58] Abu Daawuud (4753), Ahmad (04/287) na at-Twayaalisiy (01/102) na wengineo

kitu na mimi nikakisema." Atapoulizwa: "Ni nani Mtume wako?" Atasema: "Sijui." Huyu ni kwa sababu duniani hakuamini kwa moyo wake isipokuwa alitamka tu kwa ulimi wake. Yeye aliwasikia watu wanasema kitu na yeye akakisema kwa ajili ya kuwapaka mafuta. Huyu ndiye mnafiki. Ni yule anayesema yale yanayosemwa na wenye kuswali na anaswali na kufunga, lakini pamoja na hivyo moyoni mwake hakuna imani. Anafanya haya kwa ajili tu ya kutaka kuwapaka watu mafuta na unafiki. Anafanya hivi ili tu aweze kueshi pamoja na waislamu na wakati huo huo haamini ndani ya moyo wake. Hata kama alikuwa ni mfaswaha, amehifadhi vitabu na vitabu na milolongo ya wapokezi, ndani ya kaburi lake hatoweza kuzungumza na jibu litampotea na kusema kwamba hajui. Lakini hata hivyo niliwasikia watu wakisema kitu na mimi nikakisema pasi na kukijua kitu hicho na kukiamini. Anadi mwenye kunadi: "Amesema uongo mja wangu. Muandalieni makazi Motoni, mfungulieni mlango Motoni na ajiwe na moto na vuke lake na kaburi lake limbane mpaka mbavu zake zikutane - tunaomba Allaah atukinge - na kaburi lake ligeuke kuwa ni shimo miongoni mwa mashimo ya Motoni." Aseme: "Ee Mola! Usilete Qiyaamah." Kwa kuwa anajua kuwa Qiyaamah kikisimama, basi hali inayokuja baadaye ni mbaya zaidi kuliko aliyomo hivi sasa. Haya yanaashiriwa na maneno Yake (Ta´ala):

يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ

**"Allaah huwathibitisha wale walioamini kwa kauli thabiti katika maisha ya dunia na Aakhirah... "**

Allaah atawathibitisha ndani ya kaburi na wakati wa kuhojiwa kama ambavyo waliishi juu ya kauli thabiti duniani na imani ya kweli.

وَيُضِلُّ اللَّهُ الظَّالِمِينَ

**"... na Allaah huwaacha wakapotea madhalimu." (14:27)**

Hawatoweza kujibu.

Hadiyth kuhusu haya zimepokelewa kwa mapokezi mengi kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ahl-us-Sunnah wameafikiana juu yake. Hakuna walioyapinga isipokuwa Mu´tazilah ambao wanategemea akili yao. Hali kadhalika watu wa mantiki hii leo, ambao ni vifaranga vya Mu´tazilah, nao pia wanafuata madhehebu haya.

## 74. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya hodhi ya Mtume

Mwandishi (Rahimahu Allaah) amesema

*wala [usipinge] hodhi na mizani - hakika wewe unanasihiwa*

**La pili:** Hodhi. Inahusu hodhi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ni jambo limepokelewa kwa mapokezi mengi ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) yuko na hodhi. Urefu wake ni mwendo wa mwezi na upana wake ni mwendo wa mwezi. Maji yake ni meupe sana kuliko maziwa na ni matamu zaidi kuliko asali. Vikombe vyake ni idadi ya nyota zilizoko mbinguni[59]. Itaendewa na Ummah wake, wanywe humo na atazuiwa kila mzushi na kila mwenye mashaka. Mwenye mashaka atazuiwa na wala hatomwendea Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Atapouliza sababu ya kuzuiwa - yaani hawa wenye mashaka - ataambiwa:

**"Ni kwa sababu hawakuacha kuendelea kuwa ni wenye kuritadi kwenye visigino vyao."[60]**

Kwa watu aina ya pili - yaani kuhusu wazushi - ataambiwa:

**"Hakika wewe hujui yale waliyoyazua baada yako."[61]**

Kila ambaye alizua Bid´ah katika dini, kama Mu´tazilah, Khawaarij, Shiy´ah na mapote mengine ya upotevu ambayo yamezua ndani ya dini yasiyokuwemo watazuiwa na hodhi siku ya Qiyaamah. Atazuiwa kila mzushi na kila mwenye mashaka na dini yake. Hakuna wataoifikia isipokuwa watu wa imani ya kweli walio imara juu ya imani ya kweli duniani na wakafa juu yake. Hawa ndio wataifikia hiyo hodhi na watakunywa kutoka humo kiasi

[59] al-Bukhaariy (6579) na Muslim (27) na (2292)

[60] al-Bukhaariy (6593) na Muslim (26) na (2293)

[61] al-Bukhaariy (6576) na Muslim (28) na (2294)

cha kwamba hawatohisi kiu tena baada yake. Hii ndio hodhi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

## 75. Wataokunywa na kuzuiwa na hodhi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)

Ambaye alishikamana na Sunnah za Mtume duniani na akazitendea kazi ndiye ambaye ataifikia hodhi yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) siku ya Qiyaamah na atakunywa kutoka humo. Kuhusu ambaye aliipuuza Sunnah na akazua Bid´ah au akaritadi kutoka katika dini yake, atatimuliwa na kufukuzwa kutoka kwenye hiyo hodhi ilihali kipindi hicho ndio atakuwa na haja kubwa kabisa ya maji.

## 76. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya mizani

Mwandishi (Rahimahu Allaah) amesema

*wala [usipinge] hodhi na mizani - hakika wewe unanasihiwa*

**La tatu:** Mizani. Ni mizani ya kihakika ilio na masahani mawili. Mema yatawekwa kwenye sahani moja na maovu kwenye sahani lingine. Allaah (Ta´ala) amesema:

فَمَن ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ وَمَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ فِي جَهَنَّمَ خَالِدُونَ

**"Basi yule ambaye mizani yake itakuwa nzito - hao ndio wenye kufaulu, na yule ambaye mizani yake itakuwa khafifu - basi hao ni wale ambao wamekhasirika nafsi zao [watakuwa] kwenye [Moto wa] *Jahannam* ni wenye kudumu." (23:102-103)**

فَأَمَّا مَن ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَّاضِيَةٍ وَأَمَّا مَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُمُّهُ هَاوِيَةٌ

**"Basi yule itakayekuwa mizani yake nzito, basi huyo atakuwa katika maisha ya kuridhisha, na yule itakayekuwa mizani yake khafifu, basi makazi yake [itakuwa] ni *Haawiyah."* (101:06-09)**

Mizani hapa bi maana matendo yake. Mame yake yatawekwa kwenye sahani moja na maovu yake yatawekwa kwenye sahani lingine. Atalipwa kutegemea na ule upande utaokuwa na uzito zaidi. Haya ni kutokana na uadilifu wa Allaah. Hamdhulumu yeyote. Bali anamlipa mwanaadamu kwa matendo yake. Ni mizani ya kihakika.

## 77. Mtazamo wa Mu´tazilah juu ya mizani siku ya Qiyaamah

Mu´tazilah wanasema kuwa sio mizani ya kihakika. Wanasema kuwa maana yake ni kusimamisha uadilifu. Wanaona kuwa ni mizani ya kimaana na kwamba maana yake ni kusimamisha uadilifu kati ya waja. Wao hawana mashiko mengine zaidi ya akili zao. Wao wanaipinga kwa sababu hawajaiona. Wao ni watu wasioamini mambo yaliyofichikana. Haya ndio maradhi ya kuitegemea akili. Kwa sababu muumini haitegemei akili yake. Akili ni dalili, lakini sio katika mambo yote. Kuna mambo yasiyodhibitiwa na akili. Mambo yaliyofichikana akili haiwezi kuyadhibiti. Hivyo usiihukumu akili yako kwa mambo hayo. Mambo hayo yanategemea dalili peke yake. Hili ndilo lililowafanya kuipinga. Madhehebu yao yamejengwa juu ya kupinga kile wasichokiona au wanakipindisha maana kinyume na maana yake. Hawawezi kupinga mizani kwa kuwa ni kitu kilichothibiti katika Qur-aan. Amesema (Ta´ala):

وَالْوَزْنُ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ ۚ فَمَن ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ وَمَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَٰئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُم بِمَا كَانُوا بِآيَاتِنَا يَظْلِمُونَ

**"Na mizani siku hiyo itakuwa ni haki. Basi ambao mizani yao itakuwa nzito - hao ndio watakaofaulu, na ambao mizani yao itakuwa khafifu - basi hao ni wale waliokhasirika nafsi zao kwa yale waliyokuwa wakizifanyia dhulma *Aayaat* Zetu." (07:08-09)**

فَأَمَّا مَن ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَّاضِيَةٍ وَأَمَّا مَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُمُّهُ هَاوِيَةٌ

**"Basi yule itakayekuwa mizani yake nzito, basi huyo atakuwa katika maisha ya kuridhisha, na yule itakayekuwa mizani yake khafifu, basi makazi yake [itakuwa] ni *Haawiyah."* (101:06-09)**

Hawapingi tamko la mizani. Lakini hata hivyo wanaifasiri na kuipotosha kinyume na maana yake. Hivi ndivyo ilivyo hali yao katika maandiko mengine yote ambapo wanaikengeusha kinyume na maana yake sahihi.

Kuhusu Ahl-ul-Haqq wao wanaiamini  juu ya uhakika wake. Kuhusu namna yake hakuna anayeijua isipokuwa Allaah (Jalla wa ´Alaa).

## 78. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya waislamu waliokufa katika dhambi kubwa

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

30- *Sema "Allaah mtukufu atawatoa kwa fadhila Zake*

*kutoka Motoni viwiliwili vilivyoungua*

31- *[Viwekwe] kwenye mto wa Firdaws ambapo vitapata uhai kwa maji yake*

*kama kokwa lililobeba mbegu*

**MAELEZO**

Haya ni masuala kuhusu watenda maasi wanaomuabudu Allaah peke yake ambao wana madhambi makubwa chini ya shirki. Hawa wanazingatiwa kuwa ni waumini na wapwekeshaji. Lakini imani na Tawhiyd yao ni pungufu. Licha ya hivyo hawatoki katika Uislamu tofauti na wanavyoonelea Khawaarij na Mu´tazilah. Wako chini ya matakwa; iwapo Allaah atataka atawasamehe na hatowaadhibu na wataingia Peponi kipindi kile cha kwanza, na Allaah vilevile akitaka atawaadhibu. Lakini ikibidi hivo hawatodumishwa Motoni milele kama watavyodumishwa makafiri na washirikina. Watatolewa ndani ya Moto baada ya kuadhibiwa. Hilo litapitika ima kutokana na uombezi wa waombezi, fadhila za Allaah (´Azza wa Jall) au kwa kuisha kwa adhabu yao. Hawatodumishwa Motoni milele kabisa.

Motoni ataingia kafiri na mshirikina. Kuna uwezekano vilevile muumini na muislamu anayemuabudu Allaah peke yake akaingia humo kutokana na madhambi yake. Lakini kafiri na mshirikina watadumishwa Motoni. Kuhusu mpwekeshaji na muumini hawatodumishwa humo milele ikiwa kama wataingia. Hii ndio ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah tofauti na wanavyoonelea Khawaarij na Mu´tazilah.

## 79. Mtazamo wa Khawaarij na Mu´tazilah juu ya mtenda dhambi kubwa

Khawaarij wanasema kuwa mtenda dhambi kubwa ni kafiri na kwamba ametoka katika Uislamu. Wanaona kuwa akifa pasi na kutubia atadumishwa Motoni kama makafiri.

Mu´tazilah wanasema kuwa anatoka katika imani na wakati huo huo hawaonelei kuwa ameingia katika ukafiri. Wanaona kuwa yuko katika manzilah ilio kati ya manzilah mbili. Lakini akifa pasi na kutubia atadumishwa Motoni milele. Madhehebu yote mawili ni batili na yanatofautiana na dalili. Allaah (Jalla wa ´Alaa) anasema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ

**"Hakika Allaah hasamehi kushirikishwa na anasamehe yaliyo chini ya hayo kwa Amtakae." (04:48)**

Kadhalika imekuja katika Hadiyth:

**"Ambaye ndani ya moyo wake mna imani ndogo ndogo ndogo kabisa sawa na mbegu ya hardali atatolewa Motoni."[62]**

Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Na hiyo ni imani dhaifu kabisa."[63]**

Atatoka baada ya kuungua na hali ya kuwa ameshakuwa mkaa. Halafu atawekwa kwenye mto wa Peponi na uchipuke mwili wake kama inavyochipuka mbegu. Baada ya hapo ataingizwa Peponi.

[62] al-Bukhaariy (7510) na Muslim (193)

[63] Muslim (78) na (49)

***kutoka Motoni viwiliwili vilivyoungua -*** Viwiliwili vyao vitaungua na kuwa makaa kutokana na adhabu. Allaah (Jalla wa ´Alaa) atavirudishia viwiliwili hivyo uhai na baada ya hapo waingie Peponi.

***[Viwekwe] kwenye mto wa Firdaws.. -*** Firdaws ndio Pepo ilio juu kabisa na katikati ya Pepo ambapo kunapita mto huu.

***kama kokwa lililobeba mbegu -*** Kama ilivyokuja katika Hadiyth Swahiyh:

**"Mpaka watapokuwa makaa wataidhinishwa uombezi. Yaje makundi kwa makundi yaliyoungua ambapo yatawekwa kwenye mito ya Peponi. Kisha kusemwe: "Enyi watu wa Peponi! Wapeni [nafasi]." Ndipo watachipuka kama mbegu inavyokuwa kwenye kokwa lake.""[64]**

Watawekwa kwenye mto miongoni mwa mito ya Peponi unaoitwa "mto wa uhai." Wahuike kama inavyohuika mbegu iliyobebwa kwenye kokwa lake.

[64] Muslim (306) na (185)

## 80. Tofauti ya uombezi kwa Allaah na kati ya viumbe

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

32- *Hakika Mtume wa Allaah ana uombezi juu ya watu*

*Sema kuhusu adhabu ya kaburi kwamba ni haki na imewekwa wazi*

**MAELEZO**

Mwandishi (Rahimahu Allaah) katika shairi hili ametaja mambo mengi:

La kwanza: Maswali ya Malaika wawili.

La pili: Adhabu na neema ya ndani ya kaburi.

La tatu: Kupimwa kwa matendo.

La nne: Hodhi ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

La tano: Masuala kuhusu waislamu wenye kutenda dhambi kubwa.

La sita: Masuala kuhusu uombezi. Uombezi pia umetajwa katika shairi hili.

Uombezi maana yake ni ule ukati kati unaokuwepo katika kutatua haja mbalimbali kutoka kwa yule mwenye nao. Uombezi unakuwa kwa Allaah na kadhalika kwa watu. Uombezi uliyopo kwa Allaah unatofautiana na uombezi uliyopo kati ya watu. Unaweza kuombea mbele ya mtu hata kama mtu huyo hakukupa idhini. Kuhusu Allaah (Jalla wa ´Alaa) hakuna yeyote awezae kuombea mbele Yake isipokuwa baada ya kupata idhini Yake:

مَن ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِندَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ

**"Nani huyu ambaye anashufai mbele Yake bila ya idhini Yake." (02:255)**

Yeye ndiye humpa idhini muombeaji aombee. Ni lazima yule muombewaji awe ni katika watu wa Tawhiyd au kwa msemo mwingine awe ni katika wale

waislamu watenda madhambi waliokuwa wakimuabudu Allaah peke Yake. Ama kuhusu kafiri hana uombezi wowote juu yake na uombezi haukubaliwi kwake:

مَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ حَمِيمٍ وَلَا شَفِيعٍ يُطَاعُ

**"Madhalimu hawatokuwa na rafiki wa dhati na wala mwombezi anayetiiwa." (40:18)**

فَمَا تَنفَعُهُمْ شَفَاعَةُ الشَّافِعِينَ

**"Basi hautowafaa uombezi wowote wa waombezi." (74:48)**

Kafiri uombezi juu yake haukubaliwi:

وَاتَّقُوا يَوْمًا لَّا تَجْزِي نَفْسٌ عَن نَّفْسٍ شَيْئًا وَلَا يُقْبَلُ مِنْهَا عَدْلٌ وَلَا تَنفَعُهَا شَفَاعَةٌ و

**"Na iogopeni siku ambayo nafsi haitoifaa nafsi nyingine chochote wala haitokubaliwa kutoka kwake kikomboleo wala hautamfaa uombezi" (02:123)**

Lau kafiri atatoa mali zote za duniani anataka fidia hazitokubaliwa kwake:

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَاتُوا وَهُمْ كُفَّارٌ فَلَن يُقْبَلَ مِنْ أَحَدِهِم مِّلْءُ الْأَرْضِ ذَهَبًا وَلَوِ افْتَدَىٰ بِهِ

**"Hakika wale waliokufuru na wakafa nao wakiwa makafiri, basi haitakubaliwa kutoka kwa mmoja wao [fidia ya] dhahabu ya kujaza dunia nzima lau wakitaka kujikombolea nayo." (03:91)**

Fidia ili wazikomboe nafsi zao haitokubaliwa kutoka kwao. Hakuna uombezi wa yeyote utakubaliwa juu yao. Wao bila ya shaka yoyote kabisa ni katika watu wa Motoni ambapo watadumishwa humo milele. Uombezi mbele ya Allaah hauthibiti isipokuwa kwa kutimia sharti mbili:

Ya kwanza: Allaah ampe idhini muombeaji aombee.

Ya pili: Muombewaji awe ni katika waislamu watenda maasi waliokuwa wakimuabudu Allaah peke Yake.

Kuhusiana na viumbe unaweza kuombea mbele yao hata kama hawakukupa idhini ya kufanya hivo na hata kama mtu huyo hayuko radhi kwa yule unayemuombea. Bali kuna uwezekano mtu huyo akawa na chuki kwa yule unayemuombea na anatamani hata kumuua au kumpatiliza. Lakini hata hivyo akawa hana budi kukubali uombezi juu yake kwa kutenzwa nguvu kutokana na ile haja alio nayo kwa watu, mawaziri na wasaidizi. Endapo hatokubali uombezi wao watamkaripia. Kwa hivyo anakuwa hana budi kuwafanyia upole na kukubali uombezi wao japokuwa hakutoa idhini na hayuko radhi kwa yule muombewaji. Ama Allaah (Jalla wa ´Alaa) hakuna yeyote awezae kuombea mbele Yake isipokuwa kwa idhini Yake na hakuna yeyote anayeombewa Kwake isipokuwa tu wale waislamu watenda dhambi wenye kumuabudu Yeye peke yake. Hii ndio tofauti kati ya nyombezi hizo aina mbili.

## 81. Aina mbili ya uombezi

Uombezi kwa Allaah kwa kutimia sharti hizi mbili ni haki. Huu ndio uombezi wenye kuthibitishwa. Kuhusu uombezi wenye kukanushwa ni uombezi juu ya makafiri. Kwa msemo mwingine ni ule uombezi unaokuwa pasi na idhini ya Allaah. Wanachuoni wamesema kuwa kuna uombezi aina mbili:

Ya kwanza: Uombezi wenye kuthibitishwa.

Ya pili: Uombezi wenye kukanushwa. Amesema (Ta´ala):

فَمَا تَنفَعُهُمْ شَفَاعَةُ الشَّافِعِينَ

**"Basi hautowafaa uombezi wowote wa waombezi." (74:48)**

مَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ حَمِيمٍ وَلَا شَفِيعٍ يُطَاعُ

**"Madhalimu hawatokuwa na rafiki wa dhati na wala mwombezi anayetiiwa." (40:18)**

Anaweza akaja mtu na kukwambia kuwa uombezi haukubaliwi kutokana na dalili hizi mbili. Mjibu kwa kumwambia kuwa kuna Aayah zinazotolea dalili kuthibitisha uombezi. Amesema (Ta´ala):

مَن ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِندَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ

**"Nani huyu ambaye anashufai mbele Yake bila ya idhini Yake." (02:255)**

وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنِ ارْتَضَىٰ

**"Na wala hawamuombei uombezi yeyote isipokuwa kwa yule ambaye Amemridhia." (21:28)**

وَكَم مِّن مَّلَكٍ فِي السَّمَاوَاتِ لَا تُغْنِي شَفَاعَتُهُمْ شَيْئًا إِلَّا مِن بَعْدِ أَن يَأْذَنَ اللَّهُ لِمَن يَشَاءُ وَيَرْضَىٰ

**"Malaika wangapi mbinguni hautowafaa chochote uombezi wao isipokuwa baada ya kuwa Allaah ametolea idhini kwa amtakaye na akaridhia." (53:26)**

Hizi ni dalili zinazofahamisha kuwa uombezi unakubaliwa kwa kutimia sharti mbili; idhini ya Allaah na amridhie yule mwenye kuombewa. Sio uombezi wote ni wenye kuthibitishwa kama ambavyo vilevile sio uombezi wote ni wenye kukanushwa. Mambo yanatakiwa kupambanuliwa kwa mujibu wa vile zilivyofahamisha dalili.

Qur-aan haigonganishwi sehemu kwa nyingine. Kinachotakiwa ni kuoanisha baina ya Aayah, kufasiri baadhi kwa zengine, kuzipa nguvu baadhi kwa zengine. Huu ndio mfumo wa wale waliobobea katika elimu. Hakuchukuliwi upande mmoja na kusema kuwa uombezi umethibiti kwa watu wote. Hivi ndivyo wanavosema waabudu makaburi na washirikina wa hapo kale. Amesema (Ta´ala):

وَيَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنفَعُهُمْ وَيَقُولُونَ هَٰؤُلَاءِ شُفَعَاؤُنَا عِندَ اللَّهِ

**"Wanaabudu badala ya Allaah visivyowadhuru na wala kuwanufaisha na wanasema: “Hawa ni waombezi wetu mbele ya Allaah."" (10:18)**

Wanaomba uombezi ilihali wanamshirikisha Allaah. Huu ndio uombezi batili wenye kukataliwa.

## 82. Khawaarij na Mu´tazilah ndio wanaopinga uombezi

Kuna ambao wanapinga uombezi kabisa kama Mu´tazilah na Khawaarij. Ahl-us-Sunnah ndio wako kati na kati katika mlango huu. Wanaona kuwa kuna sampuli mbili za uombezi:

Ya kwanza: Uombezi uliokataliwa.

Ya pili: Uombezi uliothibitishwa.

Sisi hatupingi uombezi moja kwa moja kama ambavyo vilevile hatuuthibitishi moja kwa moja. Ni lazima kupambanua kwa minajili ya kuoanisha baina ya Aayah katika mlango huu. Huku ndio kuwa na uelewa katika dini ya Allaah (´Azza wa Jall) na ndio njia ya wale waliobobea katika elimu.

## 83. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah kuhusu uombezi

Amesema mwandishi (Rahimahu Allaah):

*Hakika Mtume wa Allaah ana uombezi juu ya watu wazi*

Uombezi uliothibitishwa umegawanyika aina mbili:

Aina ya kwanza: Kuna uombezi ambao ni maalum kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

**Uombezi wa kwanza** ni ule uombezi mkubwa. Atawaombea (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) viumbe uombezi mkubwa pale ambapo watu watakuwa wamekusanyiwa na kusimamishwa kisimamo kirefu hali ya kuwa wamesimama kwa miguu yao, macho ya kukodoka, wakiwa miguu peku, wakiwa uchi, jua litateremshwa juu yao na watakuwa na majasho:

فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ أَلْفَ سَنَةٍ

**"Katika siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu." (32:05)**

Watasogea mbele waombe mtu wa kuwaombea kwa Allaah ili awastareheshe kutokana na kisimamo hicho. Watamwendea Aadam (´alayhis-Salaam), kisha wamwendee Nuuh (´alayhis-Salaam), kisha wamwendee Ibraahiym (´alayhis-Salaam), kisha wamwendee Muusa (´alayhis-Salaam) na kisha wamwendee ´Iysaa (´alayhis-Salaam) ambapo wote watataka udhuru na waseme:

"Hakika Allaah amekasirika leo khasira ambayo hajapatapo kukasirika kabla yake na hatokasirika tena mfano wake baada yake."

Wataomba udhuru kushufaia mbele ya Allaah kutokamana na kisimamo hichi. Hatimaye watamwendea Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambapo atasema:

**"Mimi ndiye mwenye nayo."**

Atasogea mbele ya Mola Wake (Subhaanah), asujudu mbele Yake, amhimidi kwa himdi nyingi, amuombe na kunyenyekea Kwake mpaka aambiwe:

"Ee Muhammad! Inua kichwa chako! Omba utapewa! Shufaia utasikizwa!"

Awaombee waliosimamishwa na Allaah atakubali uombezi wake. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hatoombea isipokuwa baada ya kupewa idhini ilihali yeye ndiye kiongozi wa viumbe (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Baada ya hapo ndio atashufaia uombezi huu mkubwa. Uombezi huu ndio kile cheo kinachosifiwa alichokitaja Allaah pindi aliposema:

وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰ أَن يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا

**"Katika usiku amka uswali, huenda Mola wako Akakuinua cheo kinachosifika." (17:79)**

Kwa sababu kwa uombezi huo atasifiwa na wa mwanzo na wa mwisho[65].

**Uombezi wa pili** ni pale atapowaombea watu wa Peponi waingie Peponi. Watapofika Peponi hawatofunguliwa mlango moja kwa moja. Watapitia kwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ili awaombee ufunguliwe mlango wa Peponi ambapo atafanya hivo. Amesema (Ta´ala):

وَسِيقَ الَّذِينَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ إِلَى الْجَنَّةِ زُمَرًا ۖ حَتَّىٰ إِذَا جَاءُوهَا وَفُتِحَتْ أَبْوَابُهَا

**"Waliomcha Mola wao watapelekwa kuelekea Peponi kwa makundi, mpaka watakapoifikia na ikafunguliwa milango yake." (39:73)**

Hakusema:

"... mpaka watakapoifikia ikafunguliwa milango yake."

kama ilivyokuja kuhusu watu wa Motoni[66].

[65] al-Bukhaariy (4718)

[66] Tazama Suurah "az-Zumar" (39) Aayah ya 71

Bali amesema:

وَفُتِحَتْ أَبْوَابُهَا

**"... na ikafunguliwa milango yake."**

Kuja ni kitu na kufunguliwa milango ni kitu kingine. Hilo litafanyika kupitia Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

**Uombezi wa tatu** ni pindi (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) atapowaombea watu wa Peponi zinanyanyuliwa manzilah zao Peponi.

**Uombezi wa nne** ni kwa ami yake Abu Twaalib pamoja na kuwa [asli ni kuwa] uombezi hauwafai makafiri. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema kuhusu makafiri:

فَمَا تَنفَعُهُمْ شَفَاعَةُ الشَّافِعِينَ

**"Basi hautowafaa uombezi wowote wa waombezi." (74:48)**

Abu Twaalib alikufa juu ya ukafiri. Lakini kwa mtazamo wa kwamba Abu Twaalib alimhami Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), akamtetea, akasubiri pamoja naye juu ya dhiki na akamtendea wema Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), lakini pamoja na haya yote hakuwafikishwa kuingia katika Uislamu. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimuonyesha Uislamu na alikuwa na pupa aingie katika Uislamu, lakini hata hivyo akakataa. Alikuwa anaona kuwa kuingia katika Uislamu kuna kuitukana dini ya mababa zake. Mori wa kipindi cha kikafiri ndio uliomfanya kukataa. Vinginevyo alikuwa anatambua kuwa Muhammad yuko katika haki na kwamba dini yake ndio ya haki. Lakini kilichomzuia ni mori. Alikuwa anaonelea kuwa lau atasilimu hilo - kwa madai yake - lingehesabika kuwa ni kuwatukana watu wake.

Alichochelea ni lawama na akaogopa kuwatukana watu wake. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimjia pindi alipokuwa katika hali ya kukata roho akamwabia:

"Ee ami yangu! Sema "hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah" ni tamko nitalokutetea nalo mbele ya Allaah.""

Abu Jahl na ´Abdullaah bin Abiy Umayyah walikuwepo hapo. Wakamwambia: "Hivi kweli unataka kuipa mgongo mila ya ´Abdul-Muttwalib?" Mwishoni akasema: "Yeye yuko katika mila ya ´Abdul-Muttwalib.""

Hatimaye akafa juu ya hali hiyo na akakataa kusema "hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah." Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema:

**"Nitakuombea msamaha midhali sijakatazwa."**[67]

Ndipo Allaah (Ta´ala) akateremsha:

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ آمَنُوا أَن يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ وَلَوْ كَانُوا أُولِي قُرْبَىٰ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُمْ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ

**"Haimpasi Nabii na wale walioamini kuwaombea maghfirah washirikina japokuwa ni jamaa zao wa karibu baada ya kuwabainikia kwamba wao ni watu wa [Moto wa] *al-Jahiym."* (09:113)**

Akateremsha kuhusu Abu Twaalib:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَن يَشَاءُ ۚ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ

**"Hakika wewe huwezi kumhidi umpendaye lakini Allaah humhidi amtakaye - Naye anawajua zaidi waongokao." (28:56)**

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakumuombea atolewe Motoni. Kwa sababu atadumishwa Motoni kama watavyodumishwa milele makafiri wengine wote. Alichomuombea ni Amkhafifishie adhabu peke yake. Atawekwa katika ule moto mwepesi ambapo chini ya miguu yake kuna makaa mawili yanayounguza mpaka kwenye ubongo wake. Haoni kama kuna

[67] al-Bukhaariy (1360) na Muslim (39) na (24)

ambaye yuko na adhabu kali kumshinda[68] pamoja na kuwa yeye ndiye mtu wa Motoni aliye na adhabu nyepesi kabisa.

Hizi ndio nyombezi maalum kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Aina ya pili: Uombezi anaoshirikiana yeye pamoja na Malaika, wapenzi wa Allaah, waja wema na watoto waliokufa kabla ya kubaleghe[69]. Inahusu ule uombezi kwa watenda madhambi makubwa ili watolewe ndani ya Moto au wasiingie kabisa. Ni uombezi ulioenea kwa Malaika, Manabii, Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), wapenzi wa Allaah wataowaombea ndugu zao na watoto waliokufa kabla ya kubaleghe ambao watawaombea wazazi wao. Huu ni uombezi ulioenea. Unamuhusu yeye (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wengine pia.

Huu ndio ufupisho unaoweza kusemwa kuhusu uombezi.

***Sema kuhusu adhabu ya kaburi... -*** Haya yameshatangulia kubainishwa katika masuala yanayohusiana na adhabu ya kaburi.

---

[68] al-Bukhaariy (3885) na Muslim (210) na (360)

[69] al-Bukhaariy (334) na (4712) na Muslim (327) na (194)

## 84. Mtazamo wa Khawaarij, Mu´tazilah na Murji-ah juu ya mtenda dhambi

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

33- *Usiwakufurishe wenye kuswali hata kama watatenda maasi*

*wote wanatenda dhambi na Mwenye ´Arshi anasamehe*

**MAELEZO**

Haya ni masuala kuhusu kuwakufurisha watenda madhambi makubwa yaliyo chini ya shirki. Kumetokea tofauti kubwa kati ya Khawaarij, Mu´tazilah na Murji-ah na Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.

Khawaarij wanakufurisha kwa kutenda dhambi kubwa ilio chini ya shirki na wanaonelea kuwa wenye nayo watadumishwa Motoni milele. Kadhalika wanahalalisha damu na mali zao kwa kujengea kwamba ni makafiri. Wanatumia dalili kwa Aayah zilizothibiti zinazokemea juu ya madhambi na maasi na wanazifasiri kwamba zinamkufurisha mwenye madhambi hayo.

Mu´tazilah wanasema kuwa sio kafiri wala muumini. Bali yuko katika manzilah ilio kati ya manzilah mbili.

Kuhusu Murji-ah wanatofautiana nao. Hawaonelei kuwa dhambi kubwa inaidhuru imani kitu wala kuipunguza. Mtenda dhambi kubwa kwa mujibu wao ni muumini mwenye imani kamilifu. Wanaona kuwa imani haidhuriki kitu ikiambatana na madhambi kama ambavyo utiifu haunufaishi kitu ukiambatana na ukafiri. Haya ndio madhehebu ya Murji-ah kwa njia ya ufupi. Kwa sababu hawayaingizi matendo ndani ya imani. Wanaona kuwa mwenye kuacha jambo la wajibu, akafanya jambo la haramu au akafanya dhambi kubwa ilio chini ya shirki ni mwenye imani kamilifu na haipungui kwa maasi kama ambavyo haiongezeki kwa utiifu. Kwa mujibu wao imani ni kitu kimoja kisichozidi na kisichopungua. Haya ndio madhehebu ya Murji-ah

yanayopingana na madhehebu ya Khawaarij. Murji-ah wamechukua Aayah za ahadi na matarajio na wakaacha Aayah za matishio.

## 85. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya mtenda dhambi

Kuhusu Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wao wako juu ya haki na uadilifu. Hawamkufurishi mtenda dhambi kubwa na wala hawasemi kuwa ana imani kamilifu. Wanasema kuwa ni muumini mwenye imani pungufu au kwamba ni muumini mtenda dhambi kubwa. Ni muumini kwa imani yake na ni mtenda dhambi kwa dhambi yake kubwa aloitenda. Mtu kama huyu yuko chini ya matakwa kwa njia ya kwamba Allaah akitaka atamsamehe na akitaka pia atamuadhibu. Amesema (Ta´ala):

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ

**"Hakika Allaah hasamehi kushirikishwa na anasamehe yaliyo chini ya hayo kwa Amtakae." (04:48)**

Ikibidi kuadhibiwa hatodumishwa Motoni milele kama wanavyoonelea Khawaarij na Mu´tazilah.

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wameoanisha baina ya Aayah za ahadi na za matishio. Hawasemi kuwa maasi hayadhuru kitu, kama wanavyosema Murji-ah, na wala hawasemi kuwa yanakufurisha, kama wanavyosema Khawaarij. Bali wanasema kuwa maasi yanadhuru na kuipunguza imani. Lakini hata hivyo hayamtoi mwenye nayo katika dini. Wameyaoanisha maandiko. Haya ndio madhehebu ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah kuhusu mtenda dhambi kubwa. Hii ndio maana ya maneno ya mwandishi (Rahimahu Allaah):

*Usiwakufurishe wenye kuswali hata kama watatenda maasi*

Bi maana watu wa Qiblah kati ya waumini na waislamu.

***hata kama watatenda maasi... -*** Bi maana maadamu maasi yao yako chini ya kufuru na shirki.

***wote wanatenda dhambi* -** Hakuna yeyote aliyesalimika na maasi. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Nyote ni wenye kukosea sana. Wabora wa wenye kukosea ni wale wenye kutubia."[70]**

***Mwenye ´Arshi anasamehe* -** Bi maana anaghufiri. Amesema (Ta´ala):

وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ

**"... na anasamehe yaliyo chini ya hayo kwa Amtakae."**

Katika Hadiyth ya kiungu imekuja:

**"Lau utanijia na ardhi nzima imejaa makosa kisha ukakutana na Mimi na hukunishirikisha na chochote nitakujia na msamaha kiasi hicho."[71]**

Ikiwa mtu ni katika watu wenye kumuabudu Allaah peke yake na hakufanya shirki, bali ana madhambi yaliyo chini ya shirki, mtu kama huyu kuna matumaini juu yake kupata msamaha wa Allaah (´Azza wa Jall). Amesema (Ta´ala):

قُلْ يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا ۚ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

**"Sema: "Enyi waja Wangu ambao wamepindukia mipaka juu ya nafsi zao: “Msikate tamaa na huruma wa Allaah, hakika Allaah anasamehe dhambi zote, hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu."" (39:53)**

Anaweza kuwasamehe kama ambavyo vilevile anaweza akawaadhibu kwa madhambi yao. Lakini ikibidi kuwaadhibu hatowadumisha Motoni milele.

Haya ndio madhehebu yaliyo kati na kati baina ya kupetuka mipaka na kuzembea juu ya watenda madhambi.

[70] at-Tirmidhiy (2499), Ibn Maajah (4251), Ahmad (03/198) na wengineo

[71] Ahmad (05/147) na al-Haakim (04/241)

## 86. Tahadhari na maoni ya Khawaarij yatakuangamiza

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

34- *Usiitakidi maoni ya Khawaarij kwani hakika*

*ni maoni ya mwenye kupenda yanayomwangamiza na kumfedhehi*

**MAELEZO**

Khawaarij ni pote miongoni mwa mapote potevu. Wameitwa Khawaarij kwa sababu walijivua kutoka katika utiifu wa watawala. Wa kwanza ambaye walimfanyia uasi ni ´Aliy bin Abiy Twaalib (Raadhiya Allaahu ´anh) katia kipindi cha uongozi wake na wakasema ni kwa nini amewafanya wanaume kuhukumu ilihali Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema:

إِنِ الْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ

**"Hakuna hukumu isipokuwa ya Allaah."? (12:40)**

Kwa ajili hiyo pindi ´Abdullaah bin ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anhumaa) alipojadiliana nao wakamletea utata huu ya kwamba amewatumia wanaume katika hukumu. Akawajibu kwa kuwaambia kwamba Allaah si Yeye ndiye ambaye amehukumu kwa kutumia wanaume pindi muhrim atapomuua mnyama pale aliposema:

يَحْكُمُ بِهِ ذَوَا عَدْلٍ مِّنكُمْ هَدْيًا بَالِغَ الْكَعْبَةِ

**"Ahukumu kwacho watu wawili walio waadilifu miongoni mwenu. Mnyama huyo afikishwe Ka'bah [kuchinjwa]? (05:95)**

Kadhalika amehukumu kwa kutumia wanaume katika masuala yanayohusiana na uasi pale aliposema (Ta´ala):

وَإِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَابْعَثُوا حَكَمًا مِّنْ أَهْلِهِ وَحَكَمًا مِّنْ أَهْلِهَا إِن يُرِيدَا إِصْلَاحًا يُوَفِّقِ اللَّهُ بَيْنَهُمَا

**"Mkikhofu kutengana baina yao [mke na mume], basi pelekeni mwamuzi kutoka watu wake mume na mwamuzi kutoka watu wake mke. Wakitaka sulhu, basi Allaah atawawafikisha baina yao."? (04:35)**

Amehukumu kwa kutumia wanaume. ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) kuhukumu kwa kutumia wanaume inahusiana na sura kama hii.

***ni maoni ya mwenye kupenda*** - Bi maana anayapenda na kuyafuata.

***... yanayomwangamiza -*** Yanamwangamiza yule mwenye kushikamana nayo. Kwa sababu ni maoni ya khatari yanayowakufurisha waislamu, kuhalalisha damu na mali zao na kuwafanyia uasi watawala.

Madhehebu ya Khawaarij ni yenye kutoa matawi mabaya. Kwa hivyo usiyaitakidi au ukamili kwayo. Unachotakiwa ni wewe kuyazingatia kuwa ni madhehebu batili. Hili linahusiana na yule ambaye anaonelea maoni yao hata kama hakufanya matendo wanayofanya wao. Vipi kuhusu yule ambaye anaonelea maoni yao na kuyatendea kazi?

## 87. Ndio maana mafusaki wanayapenda madhehebu ya Murji-ah

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

35- *Usiwe Murjiy anayecheza na dini yake*

*hakika Murjiy kweli anacheza na dini yake*

36- *Sema kuwa imani ni maneno na nia*

*na kitendo kutokana na [ushahidi wa] maneno ya Mtume yaliyo wazi*

37- *Inapungua kwa maasi wakati fulani, na wakati mwingine*

*inaongezeka kwa utiifu na inakuwa na uzito kwenye mizani*

**MAELEZO**

Murji-ah ndio kundi la pili linalokabiliana na Khawaarij. Wameitwa "Murji-ah" kutokamana na neno "Irjaa´" ambalo maana yake ni kuchelewesha. Kwa kuwa wao wamechelewesha matendo katika imani na wakasema kuwa matendo hayaingii katika imani. Wao wanaonelea kuwa iwapo mtu ataamini kwa moyo wake lakini asifanye kitu; asiswali, asitoe zakaah, asifanye maamrisho na kujiepusha na mambo ya haramu ni muumini mwenye imani kamilifu. Haya ni madhehebu batili yanayokana matendo kabisa.

***Usiwe Murjiy anayecheza na dini yake -*** Kwa sababu madhehebu ya Murji-ah ni kucheza na dini. Wanaona kuwa mja anakuwa muumini hata kama hakufanya kitu; hata kama ataacha swalah, ataacha kufunga, ataacha kutoa zakaah, kuhiji hata kama hatofanya kitu katika maisha yake yote. Sivyo tu bali hata kama atafanya ya haramu yote. Haya ni madhehebu batili. Kwa ajili hii

watenda madhambi na maasi wanafurahi kwa madhehebu haya na kuyasapoti. Kwa sababu yanaendana nao kwa njia ya kwamba wanapata kufanya wanachokitaka na wakati huo huo bado wako na imani zao kwa mujibu wa Murji-ah. Wanaofuata hawaa, matamanio na maasi wanafurahi kwa madhehebu haya. Ni madhehebu yamejengwa juu ya kucheza na dini.

***hakika Murjiy kweli anacheza na dini yake* -** Bi maana Murji-ah wanacheza na dini na wanayaharibu maamrisho na makatazo. Kujengea juu ya madhehebu yao wanaonelea kuwa hakuna haja ya maamrisho na makatazo. Huku ni kucheza na dini ya Allaah (´Azza wa Jall).

## 88. ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah juu ya imani na Radd kwa wanaoonelea kinyume

Mwandishi (Rahimahu Allaah) amesema:

36- *Sema kuwa imani ni maneno na nia*

*na kitendo kutokana na [ushahidi wa] maneno ya Mtume yaliyo wazi*

Haya ni maneno ya tatu. Anachomaanisha ni kwamba achana na madhehebu ya Khawaarij na achana vilevile na madhehebu ya Murji-ah na badala yake sema maoni ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah ya kwamba: imani ni kutamka kwa ulimi, kuamini kwa moyo na matendo ya viungo na kwamba inazidi kwa kufanya utiifu na inapungua kwa kufanya maasi. Hii ndio maana kamilifu iliyochukuliwa kutoka kwenye dalili. Haikuchukuliwa kutoka katika matamanio na fikira. Imani inapatikana kwa kuwepo mambo mane:

La kwanza: Kutamka kwa ulimi.

La pili: Kuamini kwa moyo.

La tatu: Matendo ya viungo.

La nne: Inazidi kwa utiifu na inapungua kwa maasi.

- Imani sio [kuamini] kwa moyo peke yake kama wanavyosema Ashaa´irah.
- Imani sio kuamini kwa moyo na kutamka kwa ulimi peke yake kama wanavyosema Ahnaaf.
- Imani sio kutamka kwa ulimi peke yake kama wanavyosema Karraamiyyah.
- Imani sio kutambua ndani ya moyo kama wanavyosema Jahmiyyah. Madhehebu yao khabithi yanapelekea juu ya kwamba Fir´awn ni muumini. Kwa sababu alitambua kwa moyo wake [ukweli wa] yale aliyokuja nayo Muusa (´alayhis-Salaam):

قَالَ لَقَدْ عَلِمْتَ مَا أَنزَلَ هَٰؤُلَاءِ إِلَّا رَبُّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ

**"Hakika umekwishajua kwamba hakuna aliyeteremsha haya isipokuwa Mola wa mbingu na ardhi." (17:102)**

Alikuwa akiyatambua haya kwa moyo wake. Lakini hata hivyo aliyakana kwa sababu ya kiburi tu na ili aweze kubaki juu ya ufalme wake. Hivyo ndio maana akawa ametilia jeuri yale aliyokuja nayo Muusa (´alayhis-Salaam).

Vilevile washirikina wanatambua kwa mioyo yao ya kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah na kwamba yuko juu ya haki. Amesema (Ta´ala):

قَدْ نَعْلَمُ إِنَّهُ لَيَحْزُنُكَ الَّذِي يَقُولُونَ ۖ فَإِنَّهُمْ لَا يُكَذِّبُونَكَ وَلَٰكِنَّ الظَّالِمِينَ بِآيَاتِ اللَّهِ يَجْحَدُونَ

**"Kwa hakika Tunajua kuwa yanakuhuzunisha yale wanayoyasema. Hakika wao hawakukadhibishi wewe, lakini madhalimu wanakanusha *Aayaat* za Allaah." (06:33)**

Wao si kwamba wanamkadhibisha Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kilichofanya kumkhalifu ni ukanushaji, kiburi, kuwa na jeuri juu ya haki na kasumba juu ya batili. Haya haya ndiyo yalifanya Abu Twaalib, ambaye ni ami yake Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Alitambua kuwa Mtume ndiye yuko katika haki. Amesema:

*Hakika nimejua kuwa dini ya Muhammad*

*ndio dini bora kabisa*

Pindi alipokuwa si mwenye kumfuata na akafa juu ya mila ya ´Abdul-Muttwalib - ambayo ilikuwa juu ya shirki - akawa ni katika watu wa Motoni. Pamoja na kwamba alikuwa akitambua kuwa dini ya Muhammad ni haki. Amesema:

*Lau si lamawa au kuchelea kutukanwa*

*basi mgeniona kwa hayo ni mwenye kujisalimisha waziwazi*

Hakuna kilichomzuia kumfuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) isipokuwa kuwa na mori juu ya dini za mababa na mababu zake. Mori ndio ukamzuia na matokeo yake akafa juu ya ukafiri. Vinginevyo anajua kuwa Muhammad yuko katika haki na anaamini hili. Kujengea juu ya madhehebu ya Ashaa´irah yanapelekea kwamba ni muumini.

Imani sio kutamka kwa ulimi peke yake bila ya kuamini ndani ya moyo kama wanavyosema Karraamiyyah. Kwa sababu kujengea juu ya maoni haya wanafiki watakuwa ni waumini. Wanatambua kwa ndimi zao lakini hata hivyo wanapinga kwa mioyo yao. Pamoja na hivyo Allaah amewahukumu kwamba wako katika tabaka ya chini kabisa Motoni chini ya washirikina. Amesema:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ

**"Miongoni mwa watu wako wanaosema... "**

Bi maana wanatamka.

آمَنَّا بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا هُم بِمُؤْمِنِينَ

**"Tumemuamini Allaah na siku ya Mwisho" hali ya kuwa si wenye kuamini." (02:08)**

Bi maana wanatamka kwa ndimi zao. Katika Aayah nyingine anasema:

يَقُولُونَ بِأَفْوَاهِهِم مَّا لَيْسَ فِي قُلُوبِهِمْ

**"Wanasema kwa midomo yao yale yasiyokuwemo katika nyoyo zao." (03:167)**

Kutamka kwa ulimi peke yake haitoshi. Bali Allaah amesema juu yao:

إِذَا جَاءَكَ الْمُنَافِقُونَ قَالُوا نَشْهَدُ إِنَّكَ لَرَسُولُ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّكَ لَرَسُولُهُ وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَكَاذِبُونَ اتَّخَذُوا أَيْمَانَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۚ إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

**"Watakapokujia wanafiki wakisema: "Tunashuhudia kwamba wewe bila shaka ni Mtume wa Allaah" na Allaah anajua fika kuwa hakika wewe ni Mtume Wake na Allaah anashuhudia kuwa hakika wanafiki bila shaka ni waongo. Wamefanya viapo vyao kuwa ni kinga... "**

Bi maana sitara.

فَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۚ إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ آمَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا فَطُبِعَ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَفْقَهُونَ

**"... hivyo wakazuia [watu na] njia ya Allaah - hakika ni uovu mbaya mno waliokuwa wakitenda. Hayo ni kwa kuwa wao waliamini, kisha wakakufuru." (63:01-02)**

Wamesema kuwa wameamini kwa ndimi zao kisha wakakufuru kwa nyoyo zao. Kutamka kwa ulimi peke yake haitoshi hata kama mtu atatambua kwa ulimi. Sivyo tu, hata kama mtu atapigana vita na akapambana bega kwa bega akiwa pamoja na waislamu. Haitoshi hata kama ataswali na kufunga mpaka aamini kwa moyo wake yale yaliyotamkwa kwa ulimi wake.

Vilevile imani sio kutamka kwa ulimi na kuamini kwa moyo kama wanavyosema Fuqahaa´ wa Murji-ah. Mambo yangalikuwa hivyo basi maamrisho na makatazo visingelikuwa na faida yoyote. Ingelitosha kwa mtu kuamini kwa moyo wake na kutamka kwa ulimi wake hata kama hatoswali, hatofunga n.k. Ni jambo halina shaka kuwa haya ni madhehebu batili. Ni madhehebu yanatokomeza matendo yote. Allaah (Jalla wa ´Alaa) katika Aayah nyingi ameambatanisha matendo pamoja na imani:

آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

**"Wameamini na wakatenda mema." (11:23)**

Hakusema wale walioamini peke yake au wale waliotenda matendo mema peke yake. Ni lazima yapatikane yote mawili kwa pamoja. Matendo peke yake pasi na imani hayatoshi na wala imani peke yake pasi na matendo haitoshi. Ni lazima kupatikane imani na matendo mema vyote viwili. Haya ndio yaliyokuja katika Aayah nyingi.

## 89. Dalili juu ya kwamba imani ni maneno, kuamini na vitendo na kwamba inazidi na kupungua

Miongoni mwa mambo yanayofahamisha kuwa imani ni kutamka kwa ulimi, kuamini kwa moyo na matendo ya viungo ni ile Hadiyth iliyopokelewa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambapo amesema:

**"Imani ni tanzu sabini na kitu. Ya juu yake kabisa ni "hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah" na ya chini yake ni kuondosha chenye kuudhi njiani na kuwa na hayaa ni tanzu katika imani."**[72]

**Hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah** ni kutamka kwa ulimi.

**Kuwa na hayaa ni tanzu katika imani** ni kitendo cha moyo.

**Kuondosha chenye kuudhi njiani** ni kitendo cha viungo.

Ni dalili inayofahamisha kuwa imani ni maneno, kuamini na matendo.

Kitendo cha kwamba inazidi kwa utiifu ni jambo limetajwa wazi katika Qur-aan:

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ حَقًّا

**"Hakika waumini ni wale ambao anapotajwa Allaah nyoyo zao zinajaa khofu na wanaposomewa *Aayaat* Zake huwazidishia imani na kwa Mola wao wanategemea. [Hao ni wale] ambao wanasimamisha swalah na katika yale Tuliyowaruzuku hutoa - hao ndio waumini wa kweli! Wana daraja kwa Mola wao na maghfirah na riziki karimu." (08:02-04)**

Amefanya swalah na kujitolea ni katika imani. Hivi ni vitendo vya viungo. Kumdhukuru Allaah ni maneno ya ulimi. Maneno Yake:

زَادَتْهُمْ إِيمَانًا

[72] al-Bukhaariy (09) na Muslim (35) na (57)

**"... huwazidishia imani... "**

ni dalili yenye kuonesha kuwa imani inazidi. Amesema (Ta´ala):

وَإِذَا مَا أُنزِلَتْ سُورَةٌ فَمِنْهُم مَّن يَقُولُ أَيُّكُمْ زَادَتْهُ هَٰذِهِ إِيمَانًا ۚ فَأَمَّا الَّذِينَ آمَنُوا فَزَادَتْهُمْ إِيمَانًا

**"Inapoteremshwa Suurah, basi miongoni mwao wako wanaosema: "Nani kati yenu [Suurah] hii imemzidishia imani?" Ama wale walioamini huwazidishia imani nao wanafurahia."" (09:124)**

وَيَزْدَادَ الَّذِينَ آمَنُوا إِيمَانًا

**"Na iwazidishie imani wale walioamini." (74:31)**

Ni dalili zinazofahamisha kuwa imani inazidi kwa kufanya utiifu. Kadhalika imani inashuka kwa kufanya maasi kutokana na dalili ya Hadiyth inayosema:

**"Ambaye ataona maovu katika nyinyi ayaondoshe kwa mkono wake, asipoweza afanye hivo kwa ulimi wake, asipoweza afanye hivo kwa moyo wake - na hiyo ni imani dhaifu kabisa."**

Ni dalili yenye kuonesha kuwa imani inakuwa dhaifu. Ambaye hakemei maovu si kwa mkono wala ulimi wake ana imani dhaifu. Na yule asiyekemea si kwa mkono wake, ulimi wake wala moyo wake hana imani kabisa kutokana na maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Nyuma na hilo hakuna imani yoyote sawa na mbegu ya hardali."**

Vilevile imekuja katika Hadiyth ya kwamba:

**"Allaah atamtoa Motoni yule ambaye ndani ya moyo wake mna imani ndogo ndogo ndogo kabisa sawa na mbegu ya hardali."**

Hii ni dalili inayoonesha kuwa imani inadhoofika kiasi cha kwamba inakuwa sawa na uzani wa mbegu ya hardali au chini ya hapo. Vilevile amesema (Ta´ala):

هُمْ لِلْكُفْرِ يَوْمَئِذٍ أَقْرَبُ مِنْهُمْ لِلْإِيمَانِ

**"Wao siku ile walikuwa karibu na ukafiri kuliko imani." (03:167)**

Ni dalili inayoonesha kuwa imani inakuwa dhaifu mpaka inamfanya mwenye nayo kukaribia ukafiri:

هُمْ لِلْكُفْرِ يَوْمَئِذٍ أَقْرَبُ مِنْهُمْ لِلْإِيمَانِ

**"Wao siku ile walikuwa karibu na ukafiri kuliko imani."**

Hii ni dalili ya upunguaji wa imani.

## 90. Muumini mwenye nguvu ndiye anapendwa zaidi na Allaah kuliko dhaifu

Murji-ah wanapinga na kusema haizidi na wala haipungui. Wanasema kuwa imani ni kitu kiko moyoni na ni kitu kimoja tu. Hawaoni kuwa watu wanashindana katika imani. Wanaonelea kuwa imani ya Abu Bakr (Radhiya Allaahu ´anh) ni sawa na imani ya mtenda dhambi mkubwa kabisa. Haya ni maneno batili. Baadhi ya waumini imani zao ni zenye nguvu zaidi kuliko wengine. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Muumini mwenye nguvu ni bora na anapendwa zaidi na Allaah kuliko muumini dhaifu - na kwa wote wawili kuna kheri."**[73]

Inahusiana na nguvu za kiimani, za kimwili na za kimatendo.

Imani inazidi na kupungua bila ya shaka. Maasi yanaipunguza imani ilihali mambo ya utiifu yanaiongeza. Hii ndio maana ya imani kwa mujibu wa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah.

***Sema kuwa imani ni maneno... -*** Bi maana kutamka kwa ulimi.

***... na nia -*** Bi maana kuamini kwa moyo

***na kitendo... -*** Matendo ya viungo.

Kwa hivyo imani ni maneno, kuamini na matendo. Haya ndiyo yenye kufahamishwa na maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kama ilivyo katika Hadiyth ya tanzu za imani na nyenginezo.

***Inapungua kwa maasi wakati fulani... -*** Hii ni Radd kwa Murji-ah wanaosema kuwa imani haizidi na wala haipungui. Wanasema kuwa ni kitu kimoja na watu wake katika msingi wake wako sawasawa. Haya ni maneno batili. Uhalisia ni kuwa imani inazidi kwa utiifu na inashuka kwa kufanya maasi.

---

[73] Muslim (2667)

## 91. Ni yepi marejeo wakati wa mizozo na tofauti?

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

38- *Achana na maoni na maneno ya wanaume*

*hakika maneno ya Mtume wa Allaah ni yenye haki zaidi*

**MAELEZO**

Haya ni masuala mengine. Ni lazima kati ya wanachuoni kuwepo tofauti katika mambo mbalimbali. Mmoja anasema kitu fulani kuwa ni halali ilihali mwengine anasema kuwa ni haramu. Kati ya wanachuoni kunatokea tofauti katika masuala yanayohusiana na ´Aqiydah, kimatendo na miamala. Ni jambo lisilokuwa na shaka kwamba tofauti hutokea. Haya ndio maumbile ya mwanaadamu:

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَجَعَلَ النَّاسَ أُمَّةً وَاحِدَةً ۖ وَلَا يَزَالُونَ مُخْتَلِفِينَ إِلَّا مَن رَّحِمَ رَبُّكَ

**"Kama angetaka Mola wako, basi angejaalia watu wote kuwa ni ummah mmoja. Na hawatoacha kukhitilafiana - isipokuwa yule aliyemrehemu Mola wako." (11:118-119)**

Lakini pamoja na hivyo haijuzu kwetu kuchukua yale maoni tunayoyataka na yanayoafikiana na matashi na matamanio yetu. Tunachotakiwa ni sisi kuchukua yale maoni yaliyosimama juu ya dalili kutoka katika Qur-aan na Sunnah. Amesema (Ta´ala):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنكُمْ ۖ فَإِن تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا

**"Enyi mlioamini! Mtiini Allaah na mtiini Mtume na wale wenye madaraka katika nyinyi. Mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Allaah na Mtume mkiwa mnamwamini Allaah na siku ya Mwisho. Hivyo ni njia bora na matokeo mazuri zaidi." (04:59)**

فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ

**"... basi lirudisheni kwa Allaah... "**

Katika Kitabu cha Allaah ambacho ni Qur-aan.

وَالرَّسُولِ

**"... na Mtume." (04:59)**

Kurejea kwake katika uhai wake (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) na kumuuliza. Kuhusu baada ya kufa kwake mtu arejee katika Sunnah zake. Uwepo wa Sunnah zake ni kana kwamba bado yupo (´alayhis-Swalaatu was-Salaam). Kwa ajili hii ndio maana amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Hakika yeyote atakayeishi katika nyinyi basi atakuja kuona tofauti nyingi. Hivyo basi, jilazimieni na Sunnah zangu na Sunnah za makhaliyfah wangu waongofu baada yangu."**

**"Hakika mimi nimekuacheni yale ambayo lau mtashikamana nayo, basi hamtopotea baada yangu: Kitabu cha Allaah na Sunnah zangu."[74]**

Haijuzu kwetu kuchukua yale maoni tunayoyapenda au yanayoafikiana na matashi au matamanio yetu na tukasema:

"Haya ni yenye nafasi na mepesi kwa watu na kwamba kunatakikana mabadiliko."

Haya ni maneno batili. Haya ndio maneno yanayosemwa na waandishi na watu wengi wanaofuata matamanio hii leo. Wanasema kuwa tofauti ni rahmah. Tunasema kuwa tofauti sio rahmah. Kujumuika na umoja ndio rahmah. Ama tofauti ni adhabu na shari. Hivyo ndivyo alivyosema ´Abdullaha bin Mas´uud (Radhiya Allaahu ´anh) ya kwamba tofauti ni shari[75].

[74] al-Haakim (01/93)

[75] Abu Daawuud (1960), al-Bayhaqiy (03/143) na wengineo

Tofauti ipi. Lakini haina maana sasa ndio tuseme kuwa ni katika wasaa wa dini. Dini haiko kwa maoni ya wanachuoni. Dini iko kwa dalili. Amesema (Ta´ala):

فَإِن تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ

**"Mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Allaah na Mtume." (04:59)**

Hii ndio mizani ilio kati yetu. Allaah hatukuacha kwenye tofauti wala kwenye maneno na maoni ya fulani na fulani. Bali ametuamrisha kurejea katika mizani: Qur-aan na Sunnah.

Yule ambaye ni katika wanachuoni na anaweza kujua ni maoni yepi yaliyo na nguvu juu ya mengine, haimfai kwake kuchukua maoni yoyote mpaka ayapime na Qur-aan na Sunnah. Ama akiwa ni katika watu wasiokuwa wasomi au ndiye sasa kaanza kujifunza elimu, huyu anatakiwa kuwauliza wanachuoni. Amesema (Ta´ala):

فَاسْأَلُوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِن كُنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

**"Basi waulizeni watu wenye Ukumbusho ikiwa hamjui." (16:43)**

## 92. Msimamo wa maimamu wa nne pale maoni yao yatatofautiana na dalili II

Maimamu wanatahadharisha kuchukua maoni yao pasi na kujua dalili.

Imaam Maalik (Rahimahu Allaah) amesema:

"Kila mmoja wetu anarudiwa isipokuwa mtu mwenye kaburi hili."

Bi maana Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Amesema vilevile:

"Kila ambapo kutakuja mtu binjwa katika kujadili kuliko mwengine tuache yale Jibriyl aliyoteremka nayo kwa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa sababu ya mijadala ya watu hawa!"

Imaam ash-Shaafi´iy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Inaposihi Hadiyth basi hayo ndio madhehebu yangu."

Amesema vilevile:

"Maoni yangu yakitofautiana na maneno ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), yachukueni maneno ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na yatupeni maoni yangu kando."

Amesema tena:

"Waislamu wameafikiana juu ya kwamba yule atayebainikiwa na Sunnah ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) haifai akaiacha kwa ajili ya maneno ya yeyote."

Imaam Ahmad (Rahimahu Allaah) amesema:

"Ninastaajabishwa na watu wanaojua elimu ya mlolongo wa wapokezi na usahihi wake halafu wanaenda katika maoni ya Sufyaan ilihali Allaah (Ta´ala) amesema:

فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

**"Na watahadhari wale wanaokhalifu amri yake, isije ikawapata *fitnah* au ikawapata adhabu iumizayo." (24:63)**

Unajua ni ipi fitina? Fitina ni shirki. Huenda ataporudisha baadhi ya maneno yake kukaingia ndani ya moyo wake kitu katika upindaji akaangamia."

Hakuna maneno ya yeyote yanayosimama pamoja na maneno ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ni wajibu juu yetu wakati wa tofauti turejee katika mizani. Huu ni huruma wa Allaah kwetu ya kwamba hakutuacha juu ya tofauti na maoni ya watu. Kinyume chake ametuamrisha kuyapima maoni mbalimbali na Qur-aan na Sunnah. Hili linawahusu wanachuoni. Kuhusu wasiokuwa wasomi wanachotakiwa ni kuwauliza wanachuoni:

فَاسْأَلُوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِن كُنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

**"Basi waulizeni watu wenye Ukumbusho ikiwa hamjui." (16:43)**

Amuulize yule mwanachuoni anayeamini elimu na dini yake na atendee kazi maneno yake. Kwa ajili hii ndio maana wanasema:

"Madhehebu ya asiye msomi ni madhehebu ya yule anayemjibu."

Hiki ndicho kidhibiti katika masuala haya.

## 93. Radd kwa watu wa vyombo vya khabari wenye kuonelea kurudi katika dalili kuna neno na ni kuwabana watu

Leo magazeti na waandishi [wa khabari] wanatangaza kuchukua maoni mbalimbali na kuwapanulia watu na kuwa wakirudishwa katika dalili kuna neno na kwamba ni kuwabana. Wanasema namna hii. Hii ni kufuru. Kwa sababu mwenye kuyasema anaonelea kuwa kutendea kazi dalili kuna neno. Mwenye kusema hivi anakufuru. Kutendea kazi dalili ni faraja na sio neno. Ni wepesi kutoka kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala).

Haya ndio maneno juu ya masuala haya yanayohusiana na tofauti za wanachuoni na ni maoni yepi yanayotakiwa kutendewa kazi juu ya masuala yenye tofauti.

***hakika maneno ya Mtume wa Allaah... -*** Maneno ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndio yenye kuzingatiwa. Yeye ndiye ambaye tumeamrishwa kumfuata. Hatukuamrishwa kufuata maoni ya yeyote. Wanachuoni wanatadharisha haya kweli kweli.

## 94. Usiwatukane Ahl-ul-Hadiyth

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

39- *Usiwe katika watu waliofanya dini yao ni pumbao*

*ukawatukana na kawaponda Ahl-ul-Hadiyth*

**MAELEZO**

Usiifanye dini kuwa ni mzaha na mchezo. Hichi ni kitendo cha wanafiki na watenda madhambi. Ni juu yako kuiheshimu dini na kuyaadhimisha maamrisho yake na watu wake. Allaah (Jalla wa ´Alaa) amesema kuhusu wanafiki na watenda madhambi:

اتَّخَذُوا دِينَهُمْ لَهْوًا وَلَعِبًا وَغَرَّتْهُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا

**"Ambao wameifanya dini yao pumbao na mchezo na ukawadanganya uhai wa dunia." (07:51)**

## 95. Watu walioifanya dini yao kuwa ni pumbao na mchezo

Wanaingia katika haya Suufiyyah ambao wamefanya kuchezacheza, ngoma na nyimbo kuwa ni sehemu katika dini. Wanaita kuwa ni Anaashiyd na Qaswiydah. Wanaziimba na huku wakijikurubisha kwa Allaah. Uhakika wa mambo ni nyimbo na taarabu za haramu. Ni pumbao zilizo za haramu.

Wanaingia vilevile katika haya - nao ni msitari wa kwanza - wale ambao wamepinda katika matamanio na yale yanayopendwa na nafsi zao na wanazipa nafsi zao vile inavyovipenda ijapokuwa vitu hivyo vitakuwa vinaenda kinyume na dalili. Huku ni kuifanya dini kuwa pumbao na mchezo. Wanaingia ndani yake watenda madhambi ambao hawayajali maamrisho ya dini na wanafuata yale yanayopendwa na nafsi na matamanio yao.

Kadhalika wanaingia Suufiyyah wafanya ´ibaadah ambao wameingiza ndani ya ´ibaadah yasiyokuwemo. Bali wameingiza ndani mambo ya ngoma na kucheza ambayo yanapingana nayo. Wameyafanya haya kuwa ni dini na wanaimba Qaswiydah za nyimbo kama wanavyofanya manaswara wanapoimba nyimbo zao. Yote haya ni katika kuifanya dini kuwa ni pumbao na mchezo.

## 96. Sampuli ya kwanza ya Ahl-ul-Hadiyth

Mwandishi (Rahimahu Allaah) amesema:

39- *Usiwe katika watu waliofanya dini yao ni pumbao*

*ukawatukana na kawaponda Ahl-ul-Hadiyth*

Ni juu yako kuwaheshimu Ahl-ul-Hadiyth. Ahl-ul-Hadiyth ndio watu wa mapokezi ambao wamezitilia umuhimu Sunnah za Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kuzihifadhi mpaka wakawafikishia nazo watu kama zilivyokuja kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wakazisafisha kutokana na kasoro zote. Wamezitilia umuhimu kikamilifu. Wamegawanyika sampuli mbili:

**Sampuli ya kwanza:** Ahl-ur-Riwaayah. Hawa ni wale wenye kuhifadhi mlolongo wa wapokezi wake, wakawa bingwa kwazo, wakapambanua baina ya wapokezi wake na wakabainisha hali za wapokezi. Kadhalika wakatilia umuhimu zile matini, wakazihifadhi na kuzifikisha kwa matamshi yake. Hali imekuwa namna hii kiasi cha kwamba mpaka pale ambapo yule mwenye kuhifadhi akitilia shaka juu ya tamko anasema:

"Au amesema hivi na vile."

Anataja uwezekano wa pili na wala hakati moja kwa moja. Wakati mwingine husema:

"Fulani ametilia shaka."

Anasema hivi hata kama tamko la pili litakuwa na maana ya lile tamko alilokomeka nalo. Haijalishi kitu hata kama maana itakuwa ni ile ile. Wanaheshimu matamko kwa njia ya kwamba wanaifikisha Hadiyth kwa tamko lake kama ilivyokuja kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Huku ni kutendea kazi maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Allaah ampe nuru mtu ambaye atasikia maneno yetu akayafikisha kama alivyoyasikia. Huenda mfikishawaji anaelewa zaidi kuliko aliyesikia."**[76]

Wanahifadhi matini ya zile Hadiyth na mlolongo wa wapokezi wake ili kusiingie ndani yake matamshi yasiyokuwa ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Endapo watakuwa na shaka, basi wataibainisha. Vilevile wanazidurusu sanadi zake na kutambua hali za wapokezi mmoja baada ya mwengine. Hivyo wanabainisha kati ya ilio Swahiyh, nzuri, dhaifu na iliyotungwa. Hii ndio kazi kubwa ya wenye kuhifadhi. Wanaitwa "wakosoaji wa matini na mlolongo wa wapokezi." Ni kama wakaguzi wa dhahabu na fedha. Ni kama sonara. Masonara wanajua dhahabu na fedha ya kweli na ya feki. Pale tu anaposikia sauti ya pesa anajua kuwa ni ya kweli au feki. Wasomi wa Hadiyth wanakuwa kama wao. Pindi tu wanaposikia Hadiyth na wakasikia mlolongo wa wapokezi wake wanakwambia hali yake. Hawa ndio wanachuoni wa mapokezi.

[76] Abu Daawuud (3660), at-Tirmidhiy (2656), Ibn Maajah (230), Ahmad (01/437) na wengineo

## 97. Sampuli ya pili ya Ahl-ul-Hadiyth

**Sampuli ya pili:** Ahl-ur-Riwaayah wa Diraayah. Hawa ni wale wanachuoni ambao wamezielewa Hadiyth na wananyofoa hukumu kutoka katika Hadiyth hizo na vilevile kutaja uelewa wa Hadiyth. Mfano wa hawa ni kama al-Bukhaariy, Muslim, Maalik na Ahmad. Hawa ni wanachuoni wa Hadiyth. Wamezihifadhi na kuzielewa.

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amewapigia mfano watu hawa pale aliposema:

**"Mfano wa yale niliyotumilizwa na Allaah katika uongofu na haki ni kama mfano wa mvua nyingi iliyonyesha katika ardhi ambapo ikawa nzuri, ikakubali maji na kuotesha nyasi na majani mengi. Sehemu nyingine ikawa ni kavu na ngumu inayozuia maji, Allaah akawanufaisha watu kwa mvua hiyo ambapo wakanywa [mifugo yao] na wakalima [kwa maji hayo]. Ikanyesha sehemu nyingine ambayo ni kame haizuii maji na wala haioteshi nyasi. Basi mifano hiyo ni mfano wa mtu aliyefahamu katika dini ya Allaah, Allaah akamnufaisha na yale aliyonituma kwayo, akajua na akafundisha [wengine]. Na mfano [wa aina hii ya mwisho] wa ambaye hakuliinulia hilo kichwa na wala hakuukubali uongofu wa Allaah niliotumwa nao."**[77]

**Kundi la kwanza:** ... ni kama mfano wa mvua nyingi iliyonyesha... - Hawa ndio kama mfano wa  wenye kuhifadhi. Wamezidhibiti, wakazipokea na kuzihifadhi. Ambaye anahitajia dalili anaenda kwa wale walioziandika na wakazikusanya. Wanachota kutoka humo.

**Kundi la pili:** ... Sehemu nyingine ikawa ni kavu na ngumu inayozuia maji... - Hawa ni kama mfano wa wasomi wa Hadiyth ambao wamezihifadhi Hadiyth, kuzidhibiti na wakanyofoa hukumu kutoka humo. Hawa wameotesha majani na watu wakanywa kutoka humo. Hawa ni bora zaidi kuliko kundi lililo kabla

[77] al-Bukhaariy (79) na Muslim (15) na (2282)

yake. Hawa ni bora zaidi kuliko wale waliohifadhi. Kwa sababu hawa ndio Ahl-ur-Riwaayah wa Diraayah.

**Kundi la tatu:** ... Ikanyesha sehemu nyingine ambayo ni kame... - Huu ndio mfano wa yule ambaye hakukubali uongofu wa Allaah na hakuliinulia hilo kichwa. Watu wamegawanyika mafungu haya matatu:

1- Wamekubali. Hawaoteshi, lakini hata hivyo wamezuia maji. Hawa ndio wale wenye kuhifadhi.

2- Kundi lililozuia maji na kuotesha. Huu ndio mfano wa wale wenye kuhifadhi na wanachuoni.

3- Kundi lisilokuwa na kheri yoyote kabisa. Halioteshi majani na hawa halizuii maji. Huu ni kama mfano wa wanafiki ambao hakuna kheri yoyote ndani yao na wala hawainulii kichwa Sunnah za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Watu bora katika Ummah ni Ahl-ul-Hadiyth. Wao ndio kundi lililookoka. Imaam Ahmad (Rahimahu Allaah) amesema:

"Ikiwa kundi lililookoka sio Ahl-ul-Hadiyth basi sijui ni wepi."[78]

Ahl-ul-Hadiyth ndio kundi lililookoka. Kadhalika anaingia katika wao yule ambaye atawafuata na akapita juu ya mfumo wao.

[78] "Sharaf  Aswhaab-il-Hadiyth", uk. 25 ya al-Khatwiyb al-Baghdaadiy

## 98. Uwajibu wa kuamini ´Aqiydah hii mwanzo wa maisha hadi mwisho

Imaam Ibn Abiy Daawuud (Rahimahu Allaah) amesema:

40- *Midhali utaendelea daima kuyaitakidi haya*

*basi wewe utakuwa katika kheri jioni na asubuhi*

**MAELEZO**

Hii ni hitimisho. Ukiendelea kuyaamini yale yote yaliyomo kwenye shairi hili katika uhai wako wote na mwisho wa uhai wako, basi wewe uko katika kheri duniani na Aakhirah. Ama ukiyaamini kwa kipindi fulani halafu ukayaacha na kuyapuuza, hayatokufaa kitu. Ni lazima uendelee kuonelea ´Aqiydah hii katika maisha yako yote mpaka pale utapokufa. Kuhusu yule ambaye atayaamini mara ya kwanza kisha akajireje kwayo, huyu ataangamia pamoja na wenye kuangamia.

## 99. Uwajibu wa kutendea kazi yaliyotajwa na mwandishi

Ukitendea kazi aliyotaja mwandishi katika shairi hili na ukayaamini kama yalivyotajwa, basi wewe uko katika njia sahihi. Ambaye ataonelea kinyume na yaliyotajwa humu, atakuwa ni katika wakhalifu kutegemea na vile ukhalifu wake ulivyo. Hilo sio kwa sababu ya shairi au mshairi mwenyewe. Hilo ni kwa sababu shairi hili limechukuliwa kutoka katika Qur-aan na Sunnah. Haina maana kwamba analisifu shairi lake. Ni kusifu yale yaliyomo ambayo yana maana ya Qur-aan na Sunnah.

## 100. Hitimisho

Mwandishi (Rahimahu Allaah) amesema:

*Midhali utaendelea daima kuyaitakidi haya*

*basi wewe utakuwa katika kheri jioni na asubuhi*

**MAELEZO**

Hutokuwa miongoni mwa wale wanaoamka asubuhi hali ya kuwa ni waumini na ikifika jioni ni makafiri au wanaingiliwa na jioni wakiwa ni waumini na wanapambazukiwa wakiwa ni makafiri. Yote haya kwa sababu ya fitina. Usiwe hivyo kwa sababu uko katika mfumo wa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Hili ndio kundi lililookoka. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Utafarikiana Ummah huu katika mapote sabini na tatu. Yote yataingia Motoni isipokuwa moja."**[79]

Limeitwa kuwa "limeokoka" kwa sababu limeokoka na Moto na halikuanguka na mapote yanayoenda kinyume. Wameitwa Ahl-us-Sunnah kwa sababu wanazitendea kazi Sunnah za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kutokamana na maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

**"Jilazimieni na Sunnah zangu."**

Wameitwa "al-Jamaa´ah" kwa sababu ni wenye kukusanyika wala hawatofautiani. Miongoni mwa sifa za Ahl-ul-Haqq ni kuwa wanakusanyika na miongoni vilevile mwa sifa za watu wa batili ni kuwa wanafarikiana na kutofautiana.

[79] Abu Daawuud (4597) na wengineo

Allaah amjaze kheri mshairi juu ya Uislamu na waislamu. Tunamuomba Atunufaishe na yale aliyoyataja, atuthibitishe sisi, nyinyi na waislamu katika neno la haki na kulitendea kazi mpaka siku tutakutana Naye.

Mpaka hapa ndio mwisho wa upambanuzi wa shairi hili lililobarikiwa. Na Allaah ndiye mjuzi zaidi.

Swalah na salaam zimwendee Muhammad, kizazi chake na Maswahabah zake. Himdi zote zinamstahikia Allaah, Mola wa walimwengu.